ZANZIBAR MPYA

MAMLAKA KAMILI, NEEMA KWA WOTE

MANIFESTO 2015

CUF



Karibu Tuijenge Zanzibar Mpya

Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 25 Oktoba 2015 si uchaguzi wa kawaida kwa Zanzibar. Ni uchaguzi wa kihistoria. Utatupa Wazanzibari fursa ya kihistoria kufanya mabadiliko ya msingi ya jinsi tunavyoongozwa. Ni uchaguzi utakaoamua mwelekeo wa Zanzibar yetu. Ndiyo maana tunasema huu si mwaka wa uchaguzi; bali ni mwaka wa maamuzi.

Tarehe 25 Oktoba, 2015 Wazanzibari tutakuwa na chaguo la wazi la kuamua iwapo tunataka Zanzibar iendelee na mkwamo huu ulioletwa na uongozi usio na dira na sera zisizo na mwelekeo za Chama Cha Mapinduzi au tunataka mabadiliko yatayotuletea Zanzibar Mpya inayoangaza mbele kwenye maendeleo ya haraka na ukuaji wa kasi wa uchumi wetu na huduma za jamii.

Mimi naamini sote tumechoka na mkwamo huu. Wazanzibari kwa maumbile yetu kama wananchi wa nchi ya kisiwa ni watu tunaopenda kujituma na kutumia fursa zilizopo katika mazingira ya nchi za kisiwa kujiletea maendeleo na kubadilisha maisha yetu. Binafsi kama mtu mliyeniamini kuwa kiongozi wenu natambua uwezo huo tulio nao na naamini sasa wakati wa kuutumia kikamilifu kwa manufaa ya nchi yetu na watu wake umefika. Tunachohitaji ni uongozi makini, wenye dira na unaowajibika na sera bora zilizotungwa Zanzibar kwa ajili ya Zanzibar. CUF inakupa fursa hizo.

Mwaka 2010 tulifanya maamuzi sahihi ya kuanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya kuchoshwa na migogoro ya kisiasa iliyodumu visiwani mwetu kwa zaidi ya miaka 50 sasa. Kinachohitajika sasa ni kuipatia Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa uongozi unaojiamini na unaojituma ili kuwaletea Wazanzibari maendeleo waliyoyatarajia. CUF tumejiandaa kuwapa Wazanzibari uongozi huo.

Katika kurasa za Ilani ya Uchaguzi hii mtaona ni kiasi gani tumejiandaa kukutimizia hayo. Tupe ridhaa yako na kwa pamoja tuijenge Zanzibar Mpya yenye **Mamlaka Kamili** na **Neema kwa Wote.**

Twende Pamoja.

Seif Sharif Hamad



ZANZIBAR YENYE MAMLAKA KAMILI NA NEEMA KWA WOTE

Imani kubwa ya kihistoria tunayoendelea kupewa kupitia ridhaa ya wananchi inaturejesha tena kwao na mpango kazi uliotayarishwa kuirejeshea hadhi na heshima kwa nchi yetu pamoja na kuleta mabadiliko ya haraka ya kisiasa na kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya jamii nzima na taifa letu kuanzia tarehe 25 Oktoba 2015.

1. Tutayarejesha Mamlaka Kamili ya Zanzibar kwa kuimarisha Muungano utakaozingatia Misingi ya Haki, Usawa na Heshima kwa nchi zote mbili zinazounda Muungano huu.

3. Tutajenga Uongozi Mwema kwa Kuimarisha Misingi ya Uhuru, Haki na Maridhiano kwa wananchi wa Zanzibar

4. Tutailinda, kuienzi, kuendeleza, kuijenga na kuiboresha misingi yote ya Umoja wetu wa Kitaifa ulioasisiwa na viongozi wetu wa kisiasa wa Zanzibar, Dkt. Amani Abeid Amani Karume na Maalim Seif Sharif Hamad tarehe 5 Novemba, 2009 na kupewa ridhaa na wananchi kupitia Kura ya Maoni ya tarehe 31 Julai 2010.

5. Tutapambana kuondosha rushwa, ufisadi, upendeleo, uonevu, ubaguzi na woga ndani ya taasisi zetu pamoja na jamii kwa kurekebisha muundo wetu wa utawala, uwajibikaji, na utendaji katika kazi na utoaji wa huduma sambamba na kupanua viwango vya elimu na uelewa wa kutosha kwa jamii.

6. Tutayaendeleza mashirikiano yetu ya kimataifa (*International Relations and Cooperation*) na majirani zetu, washirika wa maendeleo, taasisi, nchi wahisani na jumuiya mbali mbali za kimaendeleo kwa lengo la kuifanya Zanzibar inufaike na mahusiano na mashirikiano hayo. Mafanikio ya mashirikiano haya yatatokana na Zanzibar yenye mamlaka kamili ndani ya muungano wa haki, heshima na usawa.

7. Tutatetea haki ya Zanzibar kushirikishwa katika Shirika la Kimataifa la Bahari (International Maritime Organization) pamoja na kusimamia kwa uwazi na kwa mujibu wa sheria za kimataifa mikataba na itifaki mbali mbali za Shirika la IMO ikiwemo suala la usajili wa meli (*International Shipping Registry*) na fursa zaidi kwa Wazanzibari katika uajiri melini.

8. Tutasimamia na kuitetea haki ya Zanzibar katika sera, mipango na matumizi ya maeneo maalum ya kiuchumi ya bahari kuu (*Exclusive Economic Zone*) na yale ya madini ya chini ya bahari (*Extended Constinental Shelf*) kwa faida ya wananchi wa Zanzibar.

9. Tutaingia kwenye uongozi tukiwa na dira ya mabadiliko itakayotupeleka kujenga mashirikiano ya kikanda katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu (*Regional Deep Sea Fisheries Management*).

10. Tutauondoa uonevu na ukiritimba unaofanywa na viongozi na watendaji wachache juu ya haki za msingi za wavuvi wetu wa mwambao na kuhakikisha haki na usawa kwa wavuvi wote ikiwemo wazalishaji wa mwani.

11. Tutahakikisha tunapiga hatua kubwa mbele katika kuijenga nchi, uchumi na jamii yenye fursa ya maendeleo yanayoongozwa na sayansi na teknolojia yakiwemo matumizi endelevu na ya gharama ndogo kwa wananchi ya teknolojia ya taarifa na mawasiliano (*Information and Communications Technology*).

12. Tutasimamia sera, sheria, na mfumo wa uendeshaji bora wa sekta ya mafuta na gesi (*Oil and Gas for Development*) ikiwemo ugawaji wa mipaka ya baharini, utafutaji, uzalishaji na mapato yanayotokana na maliasili hizo na kuhakikisha ajira na maslahi kwa wananchi wa Zanzibar.

13. Tutausimamia na kuuendesha uchumi utakaozingatia malengo ya Uchumi Endelevu (*Sustainable Development Goals*) inayozingatia vipaumbele kwa nchi za visiwa vidogo vidogo na kuendeleza mashirikiano na washirika wetu wa maendeleo katika kufikia malengo hayo.

14. Tutajenga uchumi imara unaokua kwa kasi na unaotoa ajira na tija kwa misingi ya haki na uwiano kwa wote.

15. Tutahakikisha upatikanaji wa ajira kwa wananchi wetu katika sekta zote za kiuchumi za utalii, kilimo, uvuvi, biashara, viwanda, na kukuza huduma za ujasiriamali kwa ajili ya sekta binafsi na sekta isiyokuwa rasmi.

16. Tutaunga mkono na kuusimamia utalii endelevu (Sustainable Tourism) unaojali maslahi ya wananchi, na sio viongozi tu, na kuhakikisha uwiano baina ya wawekezaji na wananchi wa maeneo husika katika utoaji wa huduma za maji, nishati, matumizi ya ardhi, ajira, na fursa nyingine za sekta hii.

17. Tutakuza biashara kwa kupunguza viwango vya ushuru na kodi na kuitangaza Zanzibar kuwa Bandari Huru sambamba na kuimarisha viwanda na miundombinu ya maendeleo ikiwemo ya ujenzi na makaazi, barabara, umeme, maji mawasiliano ya simu, bandari na viwanja vya ndege vya kisasa.

18. Tutaendeleza uzalishaji wa zao la karafuu na usimamizi endelevu wa sekta hii na kutekeleza programu za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji wa mpunga na miwa katika mabonde yetu.

19. Tutaunga mkono na kushirikiana na wawekezaji na wananchi kuharakisha huduma mbali mbali muhimu (*Service Providers*) katika uzalishaji wa mazao mbali mbali ya chakula na biashara yakiwemo matunda, mboga mboga, na nafaka kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

20. Tutaanzisha Benki ya Uwekezaji ya Zanzibar (*Zanzibar Investment Bank*) pamoja na kuunda mazingira bora ya kisera na kisheria katika uwekezaji wa mabenki ya kimataifa *(Offshore Banking)* na makampuni ya kimataifa *(Offshore Companies)*.

21. Tutaufanyia marekebisho ya kitaasisi na kiuendeshaji mfumo mzima wa utoaji wa elimu Zanzibar ili uende sambamba na haja ya kutoa elimu bora na yenye viwango vya kikanda vya Afrika Mashariki na vya kimataifa itakayokuza vipaji na vipawa vya wanafunzi wetu na kuwafanya waweze kushindana katika soko la ajira la kikanda na kimataifa.

22. Tutaboresha maslahi ya wafanyakazi na kuongeza kima cha chini cha mishahara kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji pamoja na kuhakikisha maslahi zaidi na bora kwa wastaafu (*Pensioners*) na wazee (*Senior Citizens*).

23. Tutawekeza zaidi katika usimamizi bora, upanuzi wa miundombinu, pamoja na viwango vya uhakika vya huduma katika sekta ya afya kwa ajili ya wananchi wetu na kuifanya iwe sekta bora na iliyoimarika.

24. Tutaendelea kupambana na Malaria, UKIMWI, ugonjwa wa presha, moyo, kisukari, kansa, na maradhi mengine yanayoambukiza, yaliyodharauliwa na yasiyoambukiza.

25. Tutapambana vikali na janga la dawa za kulevya kwa kuhakikisha uimarishaji ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege

na bandari zetu, viwango na miundombinu bora katika upekuzi na upelelezi, huduma bora za tiba kwa walioathirika na dawa za kulevya pamoja na elimu ya jamii kuhusu madhara yake.

26. Tutasimamia hifadhi ya mazingira yetu pamoja na kuijenga jamii iliyo tayari na uchumi wenye uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi (*Climate Change Adaptation*).

27. Tutawekeza katika mipango ya maendeleo ya uchumi na maendeleo ya jamii inayojali utayari wa kujikinga na hatari za majanga ya kimaumbile (*Disaster Risk Reduction*).

28. Tutatengeneza mpango kazi wa kuanzishwa kwa miundombinu ya kitaifa ya nishati mbadala (*Renewable Energy*) ikiwemo ya jua, upepo, takataka na biogas itakayochangia katika suala zima la mageuzi katika sekta ya nishati Zanzibar.

29. Tutahakikisha kuwa hifadhi zote za misitu zinalindwa na kuhifadhiwa pamoja na kushajiisha matumizi endelevu ya misitu.

30. Tutatunga sera na sheria mpya za usimamizi wa hifadhi za baharini (*Marine Conservation Areas*) na kuweka mipaka maalum (*zonation*) katika matumizi ya maeneo haya ya bahari kwa ajli ya wavuvi, watalii, na shughuli nyingine.

31. Tutaondoa kodi zote kandamizi zinazouathiri utalii wa hifadhi za mazingira na kuweka viwango vipya vya kodi vinavyokubalika kwa maslahi na faida ya wahusika wote.

32. Tutahakikisha utekelezaji kwa ukamilifu wa matamko yote ya kimataifa kuhusiana na haki, wajibu, na dhamana za taifa na jamii kwa wanawake, watoto, na watu wenye ulemavu.

33. Tutaendelea kuuthamini utamaduni na urithi wetu wa kihistoria *(Culture and Heritage)* na kusaidia katika kukuza malezi bora kwa vijana wetu pamoja na utunzaji wa wazee wetu.

34. Tutatilia mkazo katika uwekezaji na uimarishwaji wa michezo mbali mbali na kutoa fursa kwa vijana wetu katika ngazi zote za ushirikishwaji katika michezo yote.

35. Kwa ridhaa ya wananchi, tutahakikisha tunaiongoza Zanzibar yenye Mamlaka Kamili na inayotoa fursa, haki, na usawa kwa lengo la kujenga nchi yenye neema kwa wote ndani ya Muungano wa haki, heshima na usawa.

1. MUUNGANO WA HAKI, HESHIMA NA USAWA.

Tume ya Jaji Warioba iliasisiwa mwaka 2012 kwa ajili ya kuandika Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano. Katika maoni yaliyochukuliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa upande wa Zanzibar asilimia 60% walipendekeza Muungano wa Mkataba. Rasimu ya Jaji Warioba ilipendekeza Muundo wa Serikali Tatu. Utawala uliopo uliikataa Rasimu hii na kuipachika yao bila ya uhalali. Matokeo yake ni kusababisha migogoro mikubwa zaidi ya kikatiba na muundo utakayoimeza zaidi Zanzibar.

Katiba pendekezwa ambayo ni zao la Bunge Maalum la Katiba imepindua maoni ya wananchi yaliyokusanywa na Tume ya Jaji Warioba bila ya kutatua matatizo ya msingi na kero za Muungano zilizopo sasa; na badala yake inaanzisha matatizo mapya ya Muungano yatakayodumu muda mrefu endapo katiba hiyo itapitishwa. Katiba inayopendekezwa na watawala wa CCM imeingiza mambo ya uchumi, mafuta, na ardhi yanayohusu Zanzibar sasa kuwa ni mambo ya muungano. CUF inaamini kuwa mazungumzo ya kina na heshima baina ya pande mbili zinazounda Muungano huu ndiyo njia sahihi ya kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayoukabili Muungano. Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itahakikisha Zanzibar inarejesha Mamlaka Kamili ili Serikali ipate uwezo wa kutosha wa kuwaletea maendeleo wananchi na kuziendeleza sekta zote za maendeleo na huduma za jamii za Nchi yetu.*
- *Itaendelea kuheshimu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kuzingatia misingi ya haki, heshima na usawa baina ya nchi mbili zinazounda Muungano wetu.*
- *Itawasiliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa madhumuni ya kuifuta Katiba Pendekezwa na kuandika Katiba mpya inayoheshimu misingi ya usawa, haki na heshima baina ya nchi mbili zinazounda Muungano wetu.*
- *Itaanzisha mazungumzo ya dhati na ya kina kwa lengo la kutatua matatizo yaliyopo ambayo yanadhoofisha Muungano pamoja na kuweka misingi madhubuti itakayouimarisha zaidi kwa kuujengea uhalali mpya kutoka kwa wananchi wenyewe.*
- *Itahakikisha wananchi wa Zanzibar wanashirikishwa kwenye hatua zote katika kuamua mustakbali wa muundo wa Muungano wanaoutaka.*

1.2. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

Pamoja na kutotajwa katika orodha ya mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ushirikiano wa kimataifa limefanywa kuwa ni suala la Muungano chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na hivyo kuinyima Zanzibar fursa na uhuru wa kujiendeleza kwa kuwa na mahusiano ya kiuchumi na nchi na mashirika mbali mbali ya kimataifa kwa yale mambo yasiyo ya Muungano. Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Tutayaendeleza mashirikiano yetu ya kimataifa na majirani zetu, washirika, wafadhili, taasisi, na washiriki mbali mbali wa kimaendeleo kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar.*
- *Itafanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kuweka utaratibu utakaoipa uwezo Zanzibar wa kushughulikia wenyewe masuala yote ya ushirikiano wa kimataifa katika nyanja za uchumi na biashara ili kuziwezesha pande zote mbili za Muungano kunufaika kikamilifu na mikataba inayogusa maeneo hayo hasa kwa yale mambo yasiyo ya Muungano.*



1.3. FEDHA NA SARAFU

Benki ya Tanzania (BoT) ina mamlaka ya jumla kwa Tanzania Bara na pia kwa Zanzibar kuhusiana na masuala yote ya fedha na sarafu. Hivi sasa Benki inashughulikia hesabu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ndiyo kiungo kwa mikopo ya sekta ya umma. Inashiriki pia katika usimamizi wa mikopo na ugawaji fedha za kigeni. Kwa miaka mingi sera za Benki Kuu zimekuwa zikisababisha mfumko mkubwa wa bei na kuanguka sana kwa thamani ya sarafu Tanzania. Uchumi wa Zanzibar umekuwa ukiathirika sana kutokana na hali hii bila kulipwa fidia.

Mgao unaolipwa na BoT kwa Zanzibar ni pungufu sana ukilinganisha na hisa ya asilimia 11.02 ya Zanzibar wakati wa uundaji wa Benki hiyo. Pamoja na suala hili kuibuliwa mara kadhaa na hata ushahidi wa nyaraka kutolewa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano imelinyamazia tatizo hili na masuala mengine yaliyohusiana nalo, mambo ambayo yana athari kubwa kwa maendeleo ya Zanzibar. Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo

- *Itafuatilia matatizo haya na malalamiko mengineyo ili kupata haki zote ambazo Zanzibar inastahiki kuzipata kutoka Benki Kuu ikiwemohaki zetu za hisa za asilimia 11.02 za Benki Kuu na kuhakikisha uadilifu katika utendaji wa Benki Kuu kwa maslahi ya Zanzibar.*
- *Itaitangaza Zanzibar kama ni 'off-shore banking and off-shore companies centre' kwa lengo la kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha huduma katika eneo la Afrika Mashariki (Off-shore Investment Hub).*

- *Kabla ya kufikia lengo hilo, hatua zitachukuliwa kuhakikisha kuwa mahitaji yote muhimu ya msingi yanayopaswa kuwepo katika nchi inayoruhusu mfumo wa aina hiyo kama vile miundombinu ya kibenki, mfumo wa usimamizi (regulatory framework), uwepo wa mifumo ya bima inayoeleweka na inayoaminika, kuinua na kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, na vituo vya upokeaji na uchanbuzi wa data na takwimu yanakuwepo.*

1.4. UHURU WA MAHAKAMA NA MUUNGANO

Mbali ya Zanzibar kuwa na Mahakama zake ambazo zipo kikatiba na kisheria kutoa hukumu kwa makosa mbali mbali kwa Zanzibar, kumejengeka tabia kutoka kwa Mahakama za Tanzania Bara kuingilia na kusahihisha mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mamlaka ya kutafsiri katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ni mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Pia tabia ya mamlaka za dola kukiuka matakwa ya kikatiba na kisheria ya Zanzibar na kuwasafirisha kwa nguvu Wazanzibari kupelekwa Tanzania Bara ili kushtakiwa ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kitendo hiki kimewadhalilisha na kuwafedhehesha kwa kiasi kikubwa wananchi wa Zanzibar. Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:



- *Itasimamia matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya kuhakikisha uhuru na Mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar vinalindwa.*
- *Itahakikisha kuwa uamuzi wowote wa kuwasafirisha watuhumiwa nje ya Zanzibar utaendana na matakwa ya Sheria za Kimataifa na Matamko ya Haki za Binadamu.*

1.5. USHURU NA MAPATO KATIKA MUUNGANO

Uwekaji wa viwango vinavyolingana vya ushuru na kodi usiokwenda sambamba na uwiano wa pato baina ya Tanzania Bara yenye uchumi mkubwa na Zanzibar yenye uchumi mdogo kumepelekea shughuli za biashara kudorora Zanzibar na hivyo kuifanya iathirike na ukuaji wa nakisi katika biashara, ukosefu wa uwekezaji, uondokaji zaidi wa wataalamu, na kuporomoka kwa huduma zote muhimu za kiuchumi na kijamii. Pia, mgao wa mapato kwa Zanzibar kutoka taasisi zote za muungano zilizopo Zanzibar hauridhishi.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itatafuta suluhisho muafaka katika kipindi cha muda mfupi kuondoa vikwazo vyote vya kiuchumi na kibiashara vinavyotokana na ushuru na kodi kubwa vinavyowakabili wafanyabiashara wa Zanzibar wanapopeleka bidhaa Tanzania Bara.*
- *Itahakikisha kuwa ongezeko la mgao wa mapato ya Muungano kwa Zanzibar linafakiwa kulingana na athari zinazoikabili Zanzibar kunakosababishwa na mfumo wa ushuru na kodi usiotambua hali halisi ya kiuchumi na kimaendeleo ya nchi ya kisiwa kidogo kama Zanzibar.*
- *Itaitangaza Zanzibar kama ni Bandari Huru kwa ajili ya kuvutia uwekezaji salama wa sekta mbali mbali zikiwemo za Utalii, Mabenki, Bidhaa, Viwanda, Uvuvi, na Mafuta na Gesi.*
- *Itasimamia uanzishwaji wa Soko la Hisa la Zanzibar kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara ndogo, kati na kubwa.*


KIAPO CHA MAKAMO WA RAIS
WA ZANZIBAR
ZANZIBAR

2. MARIDHIANO NA UMOJA WA KITAIFA

CUF inaamini kwamba usimamizi mzuri wa haki za wananchi na utawala wa sheria ni sharti muhimu katika kufikia maendeleo na ustawi wa jamii na taifa, katika kulinda heshima ya taifa, kuhifadhi na kuendeleza heshima ya Wazanzibari na kulinda haki zao. Maridhiano ya Kisiasa yaliyofikiwa Novemba 2009 baina ya vyama vya CUF na CCM vikiwakilishwa na viongozi wake wakuu kwa hapa Zanzibar, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama Cha Wananchi (CUF), Maalim Seif Sharif Hamad, na kupata ridhaa ya wananchi kupitia Kura ya Maoni tarehe 31 Julai 2010, yamebadilisha kabisa takriban miaka 50 ya siasa za uhasama, chuki na mgawanyiko na kuleta mwelekeo mpya wa kisiasa Zanzibar uliolenga kuleta umoja, maelewano na amani katika nchi.

Pamoja na wananchi na viongozi walio wengi kuyaunga mkono Maridhiano ya Kisiasa yaliyofikiwa, bado wapo viongozi wa kisiasa wanaojaribu kutaka kuyavuruga na hata kuwapotosha wananchi juu ya dhamira halisi za Maridhiano haya kwa maslahi yao binafsi. CUF inaamini kuwa maridhiano si tukio lakini ni mwendelezo wa hatua nyingi zinazochukuliwa kupelekea lengo lake lifikiwe.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo

- *Itaheshimu na kutekeleza kikamilifu mambo yote yaliyokubaliwa kupitia Maridhiano ya Kisiasa ya Wazanzibari.*
- *Itaendeleza muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa uliyo imara na utakaoshirikisha vyama vyote vya siasa vitakavyopata ridhaa ya Wazanzibari na kuwa na uwakilishi katika Baraza la Wawakilishi kama ilivyoelekezwa katika Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar.*
- *Itaandaa utaratibu wa kuyatekeleza mapendekezo mengine yaliyotokana na Muafaka wa 2001 yakiwemo yale yanayohusu marekebisho mbali mbali katika utendaji wa vyombo vya serikali na pia yanayohusu wananchi waliopata athari mbali mbali za moja kwa moja wakati wa kipindi cha mgogoro wa kisiasa.*
- *Tutachukua hatua za kuhakikisha kuwa dhamira na utekelezaji wa misingi ya maridhiano yanakwenda hadi ngazi ya chini ya kitaasisi na kijamii.*
- *Tutatangaza tarehe maalum ya kuadhimisha Siku ya Maridhiano na Umoja wa Kitaifa wa Wazanzibari.*
- *Itashirikisha wananchi katika kuwepo kwa haja ya kuingiza umuhimu wa mardhinao na umoja wa kitaifa kwa Wazanzibari katika mitaala ya elimu ili kuyaenzi maridhiano haya kwa vizazi vijavyo.*
- *Itafungua ukurasa mpya wa maelewano kwa kuwataka wananchi wote kusamehe na kusahau maovu yote waliyotendeana katika kipindi cha uhasama wa kisiasa.*

3. UONGOZI MWEMA NA UTAWALA WA HAKI

Tunaamini kuwa uongozi mwema ni uongozi unaowiana, unaoheshimu na unaolinda katiba na sheria za nchi. Watu wanastahiki kuishi kwa amani na haki zao kuheshimiwa. Kutokana na mgogoro wa kisiasa uliokuwepo muda mrefu kabla na hata baada ya kuja Maridhiano, kumejengeka utamaduni miongoni mwa viongozi, watumishi serikalini na hata wananchi wa kawaida kutotekeleza na kutoheshimu katiba na sheria za nchi, na hali hiyo kuathiri mwenendo mzima wa utoaji haki na huduma za serikali kwa wananchi na kupelekea kukosekana kwa utawala wa haki.

3.1. UONGOZI MWEMA

Kumekuwa na matumaini makubwa kwa wananchi baada ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na jambo lililozaa mashirikiano baina ya wananchi na pia kwa viongozi wa kitaifa ingawa hatua zainapaswa kuchukuliwa ili kuimarisha zaidi Umoja wetu wa Kitaifa na kukabili changamoto zinazoendelea kujitokeza. Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo

- *Itaheshimu ridhaa ya wananchi na itashirikiana na viongozi watakaochaguliwa kihalali katika uchaguzi huru na haki kutoka vyama vyote vya siasa vitakavyopata ridhaa ya kuingia katika Baraza la Wawakilishi katika uendeshaji wa nchi.*
- *Itajenga taifa linaloheshimu haki za wananchi na utawala wa sheria.*
- *Itahakikisha kuwa hakuna mtu yeyote atayekuwa juu ya sheria na kwamba si kiongozi yeyote yule wa ngazi yeyote ile ya kisiasa atakayeachiwa kuwakandamiza wengine kwa kutumia vibaya madaraka aliyokabidhiwa ya uongozi.*
- *Itatunga sheria mpya kuepusha utumiaji mbaya wa madaraka ya umma.*
- *Itahakikisha ina serikali ambayo inaongozwa na utawala wa sheria, na sio kujiegesha katika matakwa na maslahi binafsi ya kiongozi.*
- *Itarekebisha au kufuta sheria zote kandamizi ambazo zinakwamisha misingi ya demokrasia na haki za binadamu. Hatua hii itahakikisha kwamba hakuna atakayeonewa kuanzia siku CUF itakapokabidhiwa madaraka ya kuongoza Serikali ya Umoja wa Kitaifa.*
- *Itawashirikisha wananchi katika kufanya mapitio ya Katiba ya Zanzibar ili iweze kwenda sambamba na misingi ya haki na uwajibikaji chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi na Zanzibar mpya tunayokusudia kuijenga kwa pamoja.*

3.2. HAKI ZA BINADAMU

Ingawa kumekuwa na hali ya mafanikio kiasi katika uimarishaji wa haki za binadamu tangu Serikali ya Awamu ya Sita na ya Saba yenye muundo wa umoja wa kitaifa kuja madarakani Novemba 2010, kwa ujumla uvunjwaji wa haki za binadamu bado umebakia kuwa ni tatizo kubwa nchini. Ripoti za Hali ya Haki za Binadamu Zanzibar zimekuwa zikionyesha kuwepo na kujikita kwa tabia za kutoheshimiwa na kuvunjwa kwa haki za binadamu kunakofanywa na vyombo vya dola na hata wananchi wenyewe.

Sheria mbaya, mahakama zisizokuwa huru, na vyombo vya dola vinavyofanya kazi kwa kufuata matakwa binafsi ya baadhi ya viongozi wake, badala ya kufuata katiba na sheria, vimesababisha viwango vya haki za binadamu nchini kuendelea kuwa katika hali mbaya.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itatekeleza kwa ukamilifu Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu na miongozo yake ili kuhakikisha kila mmoja ana haki ya kuishi na kuamua juu ya mustakbali wake, haki zake za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.*

- *Tutafanikisha uundwaji wa chombo huru na chenye nguvu cha kusimamia haki za binadamu Zanzibar na kujizatiti na kuzilinda haki hizo kwa kutilia mkazo urudishaji wa heshima na ulinzi wa Haki za Binadamu nchini.*
- *Tutahakikisha kuwa Wazanzibari walionyimwa haki yao ya ukaazi kinyume na Katiba, Haki, na Sheria, wanapatiwa haki zao kwa kupewa kitambulisho cha Mzanzibari Makaazi.*
- *Tutauondoa ubaguzi wa aina yeyote ule katika haki na fursa ya ajira kwa wananchi ndani ya Taasisi za Serikali.*
- *Itahakikisha uhuru wa vyombo vya habari na kuviondoshea udhibiti wa aina yoyote ili kuviwezesha kukua na kuwa jukwaa la kuwatumikia wananchi katika kulinda haki zao na kusaidia kuifanya serikali iwajibike kwa wananchi.*
- *Italinda haki ya uhuru wa kuabudu ili kuhakikisha dini zote zinatendewa haki na wafuasi wao wanapata fursa sawa bila kuingiliwa.*
- *Itaingiza masuala ya Haki za Binadamu kama sehemu ya mitaala maskulini ili kuhakikisha watoto na vijana wanazielewa haki zao.*

3.3. VITA DHIDI YA RUSHWA

CUF inaiona rushwa kuwa ni adui wa haki, inayoua uchumi na kuwanyima wananchi haki yao ya msingi ya maisha bora na maendeleo. Rushwa imekithiri na inaonekana kuwa sehemu ya maisha ya kila siku kiasi kwamba unaonekana mtu wa ajabu kama hutoi au hupokei rushwa. Huduma nyingi za serikali zimekuwa hazipatikani bila ya mwananchi kutoa rushwa. Chanzo kikubwa cha rushwa ni ukiritimba wa madaraka, mishahara midogo ya watendaji Serikalini, maamuzi yasiyofuata taratibu zinazoeleweka na kutowajibishwa kwa wanaoshiriki katika vitendo vya rushwa.

Ingawa Zanzibar tayari imeanzisha sheria na vyombo vya kuzuia rushwa, kuwepo kwa taasisi zaidi ya moja ya kupigana na rushwa kunaleta tatizo jingine la urasimu na kuongeza gharama za uendeshaji lakini pia kuingiliana kwa taasisi hizi kimadaraka na kiufanisi hata kutishia kupotea malengo ya kupambana na rushwa yenyewe. Ufanisi wa taasisi zenyewe upo mashakani kwani pamoja na kuwepo na kero mbali mbali zinazohusu rushwa kuwasilishwa na wananchi katika ngazi tofauti za kijamii na kitaasisi, bado mafanikio ya taasisi hizi kwa Zanzibar haujaonekana.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itaanzisha mabadiliko ya muundo na utendaji katika Serikali yatakayolenga kuondosha ukiritimba wa madaraka na kuweka utaratibu wa wazi zaidi katika uendeshaji wa shughuli zake za kila siku.*
- *Itaboresha Sheria na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar pamoja kurekebisha muundo wa taasisi zenyewe ili ziweze kufanya kwa ufanisi mkubwa na bila ya kuingiliwa.*
- *Itazifanyia mapitio sheria zilizopo ili kutoa adhabu kali kwa yeyote atakayepatikana na hatia ya rushwa.*
- *Itaboresha mishahara na maslahi ya wafanyakazi kwa kiwango cha kuridhisha ili kufifisha rushwa katika ngazi zote za utumishi Serikalini.*

3.4. UHURU WA HABARI NA MAELEZO

Kwa muda mrefu toke kuasisiwa kwake, Chama Cha Wananchi – CUF kimekuwa kikipiga kelele ndani na nje ya nchi kuhusiana na hatari ya ukandamizwaji wa haki ya mwananchi ya kuwa na uhuru wa kupata habari na maelezo bila ya vitisho wala upotoshaji wa dola. Sheria

zilizopo za habari, utangazaji, na maelezo zinaendelea kuubana uhuru na haki hiyo ya utoaji na usambazaji habari na zinatoa madaraka makubwa kwa Serikali kuvidhibiti vyombo vya habari. Isitoshe, Sheria hizo zimepelekea kutokuwepo kwa vyombo vya habari binafsi vilivyo huru na vinavyofanya kazi kwa uwazi na kwa ufanisi.

Pia, vyombo vya habari vya Serikali kwa kiwango kikubwa viko katika hali duni kiutendaji, vifaa na hata maslahi ya wafanyakazi wake na hivyo kushindwa kutekeleza ule wajibu wa vyombo vya habari vya umma (public broadcasting) katika kukuza demokrasia na kuwapa wananchi jukwaa la kutoa maoni na madukuduku yao.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itaifuta Sheria iliyopo ya Habari na kutunga sheria mpya itakayohakikisha uhuru wa upatikanaji na utoaji wa habari (Right to Information Act). Sheria hiyo itasimamia haki ya mtu yoyote kutafuta taarifa, kufungua chombo cha habari kilicho huru, kukosoa Serikali, na kujadili muelekeo wa nchi kupitia haki ya raia kupokea, kupata na kutoa habari na maoni yake.*
- *Itaviondoa vikwazo vyote viliopo ambavyo vinazuia uhuru wa waandishi wa habari kujikusanya, waandishi watashajiishwa kuunda jumuiya zao kulinda uhuru wao na maslahi yao.*
- *Itaboresha na kuliendeleza Shirika la Utangazaji Zanzibar (Zanzibar Broadcasting Corporation) ambalo litapewa uhuru kikamilifu usio na mafungamano yeyote yale ya kisiasa na chama au itikadi yeyote ile, na kusimamiwa na Bodi iliyo huru yenye kutambua na kuheshimu ushiriki kamilifu wa wananchi katika mijadala mbali mbali ya kitaifa na kimataifa bila ya udhibiti, upendeleo au ushawishi wa kisiasa.*
- *Itaimarisha na kuboresha maslahi, elimu na mafunzo kwa wafanyakazi wa vyombo vya habari na utangazaji ili kuinua utendaji wao wa kazi na kuongeza ufanisi, na kuwawezesha kufanya kazi zao kitaalamu na kwa kujiamini zaidi.*
- *Itawashajiisha na kuwasaidia wahariri na wandishi wa habari kuunda Baraza la Habari la Zanzibar kwa madhumuni ya kuimarisha ufanisi na usimamiaji wa maadili ya uandishi wa habari.*

3.5. UTAWALA WA HAKI NA SHERIA

Kila Dola ulimwenguni lazima iwe na chombo kinachoitwa Mahakama; chombo hiki lazima kiwe huru na kinapaswa kufanya kazi bila kuingiliwa. Mahakama ziko kwa ajili ya kuzitafsiri sheria na kutenda haki. Ili kuwa na sekta huru ya sheria hatuna budi kuwa na Tume ya Ajira ya Sekta ya Sheria iliyo huru, ambayo ina uhuru kamili katika kuajiri Majaji, Mahakimu na wafanyakazi wengine wa Mahkama.

Mara nyingi Mahakama zimetumiwa vibaya na wale wanaoziongoza kutekeleza matakwa binafsi na hivyo kupelekea kunyima haki wananchi, kutisha na kudhalilisha watu, hali iliyopelekea kulalamikiwa na taasisi za ndani na nje ya nchi zinazofuatilia na kuchunguza masuala ya ukiukaji wa haki za binadamu na utoaji wa haki kwa ujumla.

Washitakiwa wamekuwa wanawekwa mahabusu kwa utashi wa Jaji au Hakimu pasina kuzingatia matakwa ya sheria hasa yale yanayohusu haki ya dhamana. Kumekuwa na ulimbikizwaji wa kesi nyingi katika mahakama mbali mbali bila ya hata kusikilizwa madai ya washtakiwa wake, jambo ambalo limezidi kuwatoa imani raia juu ya mahkama na Serikali kwa ujumla.

Licha ya demokrasia ya vyama vingi, bado kuna baadhi ya sheria ambazo zinapingana na kukwaza mfumo huo. Jaji Mkuu hana uajiri madhubuti unaolingana na taratibu za Mahakama duniani. Muundo wa Tume

ya Ajira ya Sekta ya Sheria kwa kiasi kikubwa unaifanya ikose uhuru wake kutokana na wajumbe wake wengi kuwa ni wateule wa Rais moja kwa moja.

Majengo na hali ya Mahkama Kuu na Mahkama za ngazi za chini yapo katika hali mbaya inayodhalilisha chombo hicho muhimu cha dola. Hakuna sehemu maalum za kuweka mahabusu watoto na hatuna vituo vya kurekebisha tabia kwa wale waliopatikana na hatia.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itaziimarisha Mahakama na kuhakikisha uhuru wake unalindwa kikamilifu, kisheria na kiutendaji.*
- *Itaziboresha Mahakama kwa kuzipa uwezo wa kutosha ili kuhakikisha hakuna ulimbikizwaji wa kesi mahakamani bila ya kusikilizwa lakini pia kutoa dhamana kwa wakati kwa wale washtakiwa wanaopaswa kupata haki hiyo.*
- *Itatoa uhuru kwa Tume ya Ajira ya Sekta ya Sheria na itaweka taratibu bora za uundwaji wake na utendaji wake wa kazi.*
- *Itapanga uajiri wa Jaji Mkuu kwa taratibu za Kimahakama zinazokubalika za ulimwenguni.*
- *Itaweka vituo vya kurekebisha tabia kwa watoto watakaopatikana na hatia za uhalifu wa sheria pamoja na kuwapa fursa ya kuendelea na elimu na mafunzo ya amali wakati wanatumikia katika vituo vya kurekebisha tabia.*
- *Itahakikisha kuwa haki za wafungwa na walio mahabusu zinatekelezwa kwa mujibu wa Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu.*

3.6. ULINZI NA USALAMA

Idara Maalum kama vile Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kikosi cha Valantia (KVZ), Chuo cha Mafunzo (Magereza), na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi vinakabiliwa na changamoto kubwa ya kujenga imani ya Wananchi wanowatumikia. Kutokana na historia yake na utendaji kazi wake huko nyuma, vikosi hivi kwa kiasi kikubwa havijajenga imani ya wananchi wote kuwa ni vikosi vya kutoa huduma maalum na visivyoegemea upande wowote wa kisiasa.

Isitoshe, vikosi hivi na askari wake wamekuwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa vifaa na mahitaji mengine muhimu, mafunzo duni na maslahi yasiyoridhisha. Kwa kiasi kikubwa, ufanisi wa vikosi hivi kama tegemeo la ulinzi, usalama, na uokozi kwa wananchi wote umeshuka na badala yake vijana wa vikosi hivi wamekuwa wakitumiwa mara nyingi katika mambo ya kisiasa. CUF inaamini kuwa wakati umefika kwa vikosi hivi kufanya kazi zao husika kwa mujibu wa taaluma na malengo yao ya kazi *(Professional Guards)*

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itavipa sura mpya vikosi hivi kwa kuvifanya kuwa vyombo vya kutoa huduma kwa jamii na kuvipatia vifaa na mafunzo muafaka ili viwatumikie wananchi ipasavyo pamoja na kuviwezesha kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.*
- *Itaangalia upya mishahara, maslahi na marupurupu ya askari na watumishi wengine wa Idara hizi Maalum za SMZ kwa lengo la kuwoangezea ari ya utendaji na ushiriki wao katika ujenzi wa Zanzibar mpya.*
- *Itabadilisha jina la KMKM na kuiita Kikosi cha Ulinzi wa Mwambao wa Zanzibar (Zanzibar Coast Guards).*
- *Itahakikisha kuwa vikosi vyote vinapewa mafunzo maalum ili kuweza kutoa huduma ya mwanzo na misaada mingine ya kibinadamu wakati wa maafa.*
- *Itasimamia haki zinazohusiana na maslahi, mazingira ya kufanyia kazi na vitendea kazi kwa kufuata utaratibu uliokuwepo*

wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza chini ya Sheikh Abeid Amani Karume ya kushugulikia nyongeza za mishahara na mafao kwa watumishi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Muungano walio Zanzibar

3.7. UTUMISHI SERIKALINI NA UWAJIBIKAJI

Utumishi Serikalini ndiyo injini ya Serikali imara na yenye ufanisi katika kuwahudumia raia wake. Katika malengo ya kuijenga Zanzibar Mpya yenye vigezo vya ushindani wa kiutendaji na serikali nyengine duniani, jukumu kubwa liliopo mbele yetu ni kuimarisha utumishi Serikalini ili uendane na mahitaji ya wakati huu na wakati ujao ili kufikia viwango vya kimataifa katika utoaji wa huduma.

Tafiti mbali mbali zimeonyesha kuwa Sekta ya Utumishi Serikalini inakabiliwa na changamoto kuu mbali mbali ikiwemo ukosefu wa sifa na ujuzi unaotakiwa, uingizwaji wa watumishi katika migogoro ya kisiasa, ukosefu wa haki za mafao kwa wanaostahiki, ubadhirifu, uwajibikaji na nidhamu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itaunda upya Tume Huru ya Utumishi Serikalini kwa kuzingatia haja ya kuongoza na kusimamia marekebisho makubwa ya Utumishi Serikalini.*
- *Itaanzisha Idara Maalum ya Msimamizi Mkuu wa Huduma za Serikali (Inspector General of Government Services), itakayochunguza na kufuatilia utendaji kazi wa vyombo vya Serikali, ufanisi wao, pamoja na kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu utumishi.*
- *Italinda ajira na maslahi ya watumishi wote wa Serikali na kuwapa fursa za mafunzo wakiwa kazini ili kuongeza elimu, maarifa na ujuzi wao wa kazi kwa lengo la kuinua ufanisi na uwajibikaji.*
- *Itahakikisha kuwa ajira atapewa Mzanzibari yeyote mwenye sifa bila aina yoyote ya ubaguzi.*
- *Itahakikisha kuwa maelezo ya dhamana za kazi yanafuatwa sawa sawa na watendaji wanawajibika ipasavyo katika kazi na dhamana zao.*
- *Itatoa mafao yote muda mfupi tu baada ya mtu kustaafu au kuacha kazi.*

4. TUTAJENGA UCHUMI IMARA UNAOTOA AJIRA NA TIJA KWA WOTE

Zanzibar bado ina uchumi wa zao moja, unaotegemea karafuu kwa wastani wa asilimia 76 ya mapato yake ya mauzo ya bidhaa zake nchi za nje. Kilimo (yaani ukulima, misitu na uvuvi) bado ndiyo sekta kuu inayoajiri kiasi cha asilimia 80 ya wananchi. Zaidi ya asilimia 25 ya mazao ya kilimo ni kwa ajili ya chakula cha mkulima mwenyewe (subsistence farming). Hali ya maisha ya Mzanzibari kwa wastani imeendelea kuwa mbaya kutokana na umasikini wa kipato. Ukuaji wa uchumi wa Zanzibar bado haujamnufaisha mwananchi wa kawaida. Kupanda kwa kasi ya kutisha kwa gharama za maisha hakuendani na ongezeko la mapato ya wananchi walio wengi. Muundo wa uchumi unaonekana kuzorotesha uzalishaji, uwekezaji, biashara na ubunifu. Kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar kunatoa fursa pekee na adhimu ya kihistoria ya kutumia vipaji na uwezo wa Wazanzibari wote walio ndani na nje ya nchi katika kuujenga upya uchumi wa Zanzibar kwa lengo la kumnufaisha Mzanzibari.

4.1. FURSA NA UWEZO WA KIUCHUMI

Zanzibar imekaa pazuri kijiografia. Uzuri wa maeneo yake na utamaduni wake unaosifika peke yake ni vivutio vikubwa kwa wawekezaji. Ina ardhi yenye rutuba nzuri inayoweza kustawisha mazao muhimu ya biashara. Bahari ya Zanzibar ina utajiri mkubwa wa viumbe vya bahari na inayo rasilimali ya mafuta na gesi asilia iliyoko katika ardhi yake na mipaka yake ya bahari ambayo pia bado haijaguswa.

Kuna maelfu ya Wazanzibari wanaoishi Tanzania Bara na nchi za nje. Wengi wao wamefanikiwa sana kiuchumi na wamekusanya rasilimali ya elimu na fedha. Hivi sasa maelfu ya Wazanzibari walio nyumbani wanatunzwa na Wazanzibari walioko nje.

Vianzio hivi vya maendeleo havijatumiwa ipasavyo kumnufaisha Mzanzibari na kuinua hali ya maisha yake. Hatujatambua umuhimu wa kuhifadhi ardhi finyu tuliyo nayo wala kupanga matumizi yake baina ya ardhi ya ukulima, makaazi ya watu, viwanda na uwekezaji, na ile ya biashara hasa biashara ya utalii.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itahakikisha mgawanyo wa rasilimali unakuwa wa uwiano baina ya visiwa vyote na mjini na mashamba.*
- *Itahakikisha tafiti mbali mbali za kiuchumi zinafanyika na kuzifanyia kazi ili kutoa maamuzi yanayofaa kwa wakati muwafaka.*
- *Itahakikisha kuwa mpango wa matumizi bora ya ardhi unajali maslahi ya wananchi wanyonge hususan katika haki zao za umiliki wa ardhi, upatikanaji wa maji safi, miundombinu na pembejeo za kilimo, mifugo, ufikiwaji wa barabara bora, nishati, huduma za elimu na afya, na mawasiliano.*
- *Itatumia sera za kibenki (monetary policy) kupunguza mfumuko wa bei ili kujenga ukuaji wa uchumi unaoenda sambamba na maisha mazuri kwa wananchi.*
- *Itatumia sera za kodi (fiscal policy) kukuza uzalishaji wa ndani na kukuza viwanda vidogo vidogo.*

4.2. UONDOSHAJI WA UMASKINI

Wastani wa kipato cha Mzanzibari ni dola za kimarekani 650 kwa mwaka. Hivyo Wazanzibari wengi wanaishi kwa chini ya dola moja kwa siku. Kiasi ya asilimia 51 ya wananchi ni maskini wa kupindukia. Maeneo ya mashamba umaskini umekuwa ndio mfumo wa maisha, ndio utamaduni wa nchi na wananchi wanalazimishwa kuukubali na kukaa bure, bila ya kazi, huku maisha yao yakiyoyoma. Wazanzibari wamekuwa hawana vishawishi wala njia za kutumia rasilimali walizo nazo kujiletea maendeleo.

Kutokana na hali hii, tofauti kubwa ya viwango vya maisha ya wananchi kati ya walionacho na wasionacho imezidi kuongezeka katika visiwa vyote viwili, mijini na mashamba. Kisiwa cha Pemba kiko nyuma kwa maendeleo pamoja na kubarikiwa uwezo mkubwa zaidi wa rasilimali ya kilimo na maliasili na kutoa robo tatu ya zao la karafuu.

Kwa muda mrefu huduma muhimu za umma kama maji na umeme zimekuwa zikitolewa kwa mgao hata katika miji mikuu ya Zanzibar. Haishangazi basi kuwa watu wengi wamehama katika maeneo yao ya asili yenye utajiri na rasilimali kwenda Tanzania Bara na kwengineko duniani kutafuta maisha bora. Ni wazi kwamba hii ni hatari kwa uchumi wa nchi yetu.

Maeneo ya mashamba ya Zanzibar yamejikuta yakishindwa kuunganishwa kiuchumi na miji ya Zanzibar na kuwafanya wananchi wake kushindwa kujiendeleza kimaisha na kiuchumi. Fursa ya mikopo ya Benki kwa mwananchi wa kawaida bado ni changamoto kubwa. Mwananchi wa kawaida anashindwa kumudu mikopo ambayo ingetumika kama mtaji wa kuanzisha miradi ya kumuinua kimaisha pamoja na familia yake.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itatengeneza mpango mpya wa maendeleo endelevu (Zanzibar Sustainable Development Strategy) utakaojali vipaumbele vya maendeleo na huduma za jamii vinavyotokana na mahitaji ya wananchi wenyewe.*
- *Itautilia mkazo mpango mpya wa maendeleo unaojali programu za uzalishaji na uendeshaji zenye ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yaani Public-Private Partnership (PPP).*
- *Itaongoza uwekezaji pamoja na ujenzi wa miundombinu mbalimbali madhubuti na endeleveu ya huduma zote muhimu za kiuchumi na kijamii, kama vile kilimo, mifugo, viwanda, uvuvi, nishati bora na endelevu, maji, mawasiliano, barabara, nakupeleka vitega uchumi sehemu zote za visiwa hivi ndani ya kipindi cha miaka mitano ya uongozi.*
- *Itahakikisha upanuzi wa huduma za jamii na masuala yanayogusa kila mtu kama vile usalama wa chakula, lishe bora, elimu bora inayojali usawa na kutoa fursa kwa wote, Tiba bora na afya ya jamii, makaazi ya kisasa na endelevu, na masoko.*
- *Itasimamia fursa mpya za maendeleo ya sekta ya bahari kuu ikiwemo mashirikiano ya kikanda ya uvuvi wa bahari kuu na uchimbaji wa mafuta na gesi katika bahari.*
- *Itatoa motisha unaohitajika kwa Wazanzibari walioko nje ili walete nyumbani akiba zao pamoja na kuwahakikishia usalama wa mali zao.*
- *Itahakikisha inatoa misaada ya kuwawezesha wavuvi wetu wadogo wadogo kujiongezea uwezo wa kuvua na kuhifadhi samaki ili kuwaongezea kipato.*
- *Itatekeleza ipasavyo sheria iliyopo inayozuia mgeni yeyote kumiliki ardhi humu nchini. Ardhi itabaki rasilimali kuu ya Wazanzibari na itaweza kutumika kama hisa ya mzalendo katika kuingia ubia wa uwekezaji na mtu yeyote. Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itawasaidia Wazanzibari kuhakikisha hawadhulumiwi wala hawaonewi.*

4.3. USIMAMIZI WA MAPATO

Kwa muda mrefu, hususan katika kipindi cha miaka ya karibuni, bajeti ya Serikali imeathirika kwa kuwepo nakisi kubwa. Hali ilibadilika na kuwa mbaya zaidi baada ya usawazishaji wa kodi wa 1999. Katika kipindi chote hicho, nakisi imekuwa ikipanda na kushuka bila ya faida yeyote kwa Pato la Taifa (GDP) la Zanzibar. Nakisi hii kubwa ya kifedha imesababishwa na mfumo dhaifu wa kodi, ubovu wa ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi, misamaha mingi ya kodi na kutojua taratibu za ushuru.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo kurekebisha kasoro hizi:

- *Katika kurejesha imani katika utaratibu wa bajeti, itaziba mianya yote ya rushwa inayopelekea kupungua kwa ukusanyaji wa mapato wa kiuchumi na huduma za kijamii.*
- *Itaoanisha muundo wa serikali na majukumu yake katika kupunguza gharama kubwa zinazoitia Serikali hasara na kuinyima mapato kwa kupunguza ukubwa wa serikali.*
- *Itajitoa katika shughuli za moja kwa moja za uzalishaji na kuunga mkono programu za Public Private Partnership (PPP).*
- *Itabinafsisha biashara ya karafuu na kuuangalia upya muundo na dhamana za Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC).*
- *Itaweka uwiano mzuri katika mahusiano ya kifedha hasa katika kushawishi mgawanyo mzuri wa gharama na maslahi ya Muungano, ikiwemo thamani ya mapato yanayokosekana Zanzibar kutokana na kusawazishwa kodi ya bidhaa ziingiazo nchini.*
- *Itarekebisha utaratibu wa misamaha ya kodi ili kuepuka utumiaji wake mbaya.*
- *Itapanua mtandao wa kodi na itaimarisha ukusanyaji wa mapato bila ya kuwaathiri wananchi wanyonge wenye kipato cha chini au wafanyabiashara wadogo.*
- *Itadai Zanzibar iongezewe kasma katika mikopo na misaada.*
- *Itazijengea uwezo mamlaka za serikali za mitaa kukusanya kodi katika maeneo yao pamoja na kukasimu madaraka ya matumizi ya maendeleo yao.*

4.4. MPANGILIO WA BAJETI

Mwanya mkubwa uliopo baina ya bajeti na mgawanyo halisi wa rasilimali umekuwa ukivuruga mipango ya Wizara na Idara mbali mbali Serikalini. Hii imeathiri sana ufanisi wa shughuli zao. Miradi mingi ya Serikali imekuwa haina matokeo mazuri *(positive impact)* wala mafanikio kwa jamii yenyewe. Hii inadumaza sana mipango ya muda mrefu ya Serikali.

Usimamizi wa nidhamu ya utekelezaji wa bajeti haupo. Hatupangi bajeti kwa kuzingatia uhalisia wa mapato yetu. Wakuu wa Wizara ya Fedha wanajipa madaraka na mamlaka ya kuamua kiasi gani kiende wapi bila ya kuzingatia bajeti iliyopitishwa. Kitendo cha watawala wa Wizara ya Fedha kujifanya wafalme katika muundo mzima wa matumizi ya fedha katika nchi ni mfano wa matumizi mabaya ya madaraka.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itahakikisha yafuatayo:

- *Itautizama upya muundo mzima wa usimamizi, madaraka, na mipango ya bajeti ya Wizara ya Fedha na kuondoa "ufalme" wa madaraka wanaojipa watawala wa Wizara ya Fedha.*
- *Itaangalia upya vipaumbele vya utekelezaji wa bajeti za Serikali kwa mujibu wa malengo ya maendeleo endelevu na vipaumbele vya Zanzibar.*
- *Itadhibiti matumizi holela ya rasilmali na kuhakikisha kuwa kila senti inayopatikana inaelekezwa kunako harakati za ujenzi wa uchumi na maendeleo ya miundombinu pamoja na huduma na usalama wa jamii.*

- *Itatafuta mufaka wa kutafuta njia bora ya mashirikiano na wafadhili (Consultative Group Meetings for Zanzibar) katika misaada ya bajeti kwa malengo makhsusi ya Zanzibar.*

4.5. MISHAHARA NA UAJIRI UTUMISHI

Orodha ya malipo ya mishahara na mafao ya wastaafu imejaa wafanyakazi na wastaafu hewa. Pamoja na ufinyu wa mafao yenyewe kumesababisha watu waliofikia umri wa kustaafu kujilazimisha kuendelea na kazi pasina kuwa na uwezo wa uzalishaji na hivyo kukosekana tija.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo kurekebisha kasoro hizi:

- *Itaondoa wafanyakazi na wastaafu hewa katika orodha ya malipo ya mishahara na mafao.*
- *Italipa mishahara inayokidhi kwa wafanyakazi wa Serikali.*
- *Itanyanyua kiwango cha chini cha mshahara*
- *Itatoa mishahara maalum ya kuvutia kwa wataalamu ili waweze kuja na kubakia kufanya kazi Zanzibar.*

4.6. AJIRA KWA VIJANA

Mojawapo ya matatizo makubwa yanayoikabili Zanzibar ni ukosefu wa ajira kwa vijana wake. Wapo vijana wengi ambao wamefaidika na fursa za elimu ya juu kutoka vyuo vikuu vilivyopo Zanzibar na kuhitimu mafunzo ya fani mbali mbali lakini wameshindwa kupata ajira. Kwa upande mwengine, bado kuna wimbi kubwa la vijana ambao hawana elimu rasmi na ambao wamebaki kuzurura mitaani kutokana na kukosa ajira. Hali hii haiashirii mustakbali mzuri huko tunakoelekea. Ukosefu wa ajira umefikia zaidi ya asilimia 30 ya nguvu kazi yote. Hali halisi huenda ikawa ni mbaya zaidi. Vile vile, Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa kuleta ajira kwa vijana wasio

na ajira wanaoongezeka sambamba na kuongezeka umaskini nchini.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itahakikisha kwamba inatoa ufumbuzi wa kudumu kwa matatizo ya ukosefu wa ajira kwa vijana na wanaomaliza skuli, kuweka mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji katika viwanda, na pia kukuza biashara na utalii wenye tija ili kuchangia vilivyo katika uchumi na upatikanaji wa ajira.*
- *Itaanzisha vyuo maalum vya kutoa elimu ya amali yenye tija na mustakbali mzuri ili kuwawezesha vijana wanaomaliza skuli na wasiokuwa na kazi kuingia katika soko la ajira la ndani na nje.*
- *Itaupitia mtaala wa sekondari, vyuo na vyuo vya amali ili kuenda sambamba na mahitaji ya ajira na kujiajiri.*
- *Itarahisisha mawasiliano kwa kuwawezesha vijana kupata habari za ajira zilizopo na ili vijana waweze kuzifikia.*
- *Itashajiisha na kuvisaidia viwanda vidogo vidogo vidogo kukuza ajira.*
- *Itawalinda vijana kupiga vita unyanyasaji wowote unaotokana na ajira.*
- *Itawatayarisha vijana kitaaluma na mafunzo kuweza kushindana kwenye soka la ajira la kimataifa.*

4.7. UWEKEZAJI

Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2010 *(Doing Business in Zanzibar 2010)*, uwekezaji Zanzibar bado unafanyika katika hali ya mashaka makubwa na vikwazo vingi mno. Kwa mfano, kampuni yeyote inayotaka kuwekeza Zanzibar inabidi ilipe malipo yapatao 48 na jumla ya wastani wa asilimia 40.8% ya faida yake kama kodi. Pamoja na hayo, mwekezaji humbidi atumie masaa 158 kwa mwaka katika taratibu za ulipwaji kodi. Isitoshe, mwekezaji anakumbana na vikwazo vingi vya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mambo ya kodi ya mapato ya mashirika na makampuni, na iliyobaki basi huja kama kodi kutoka sehemu mbali mbali za tozo mfano Bodi ya Mapato Zanzibar, Manispaa, Halmashauri, n.k. Hali hii inatisha

Mfumo wa Sheria unaosimamia vitega uchumi ni wa kukanganya, kugongana kimajukumu na unaopoteza wakati. Kumekuwa na mitafaruku ya kitaasisi katika kufanya kazi moja mfano ZIPA, Wizara za Fedha, Utalii, Uvuvi, Biashara, n.k. Lakini pia katika urasimu wa kutoa huduma kwa mwekezaji katika masuala ya vibali vya ardhi, mazingira, Tawala za Mikoa, Halmashauri, n.k. Wawekezaji wanapata usumbufu mkubwa kwa kupewa ahadi za uongo na kutembea taasisi nyingi pamoja na kutumia gharama kubwa sana katika kupitisha vitega uchumi vyao serikalini.

Hakuna utaratibu wa kupata wawekezaji wenye uzoefu mkubwa watakaoleta tija katika nchi. Pia huduma za kiuchumi na kijami hazijielekezi katika uwekezaji wakati mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo imeweza kukusanya mitaji mikubwa na ya kutosha imeshindwa kufanya uwekezaji wa maana na wa miradi mikubwa itakayoleta tija, kuongeza pato la taifa na kutoa ajira kwa wananchi.

Vivutio vya uwekezaji haviridhishi kutokana na kukosekana kwa huduma muhimu kama za ujenzi wa barabara, upatikanaji wa maji, usimamizi wa mazingira, maji machafu na taka ngumu, pamoja na kasoro mbali mbali zilizopaswa kufanyiwa kazi ili kuvutia uwekezaji mkubwa zaidi. Migogoro isiyokwisha ya ardhi, ugomvi baina ya sekta za utalii baharaini na wavuvi, na mabadiliko ya kidemokrasia ni ya kujilazimisha na hayajengi imani ya wawekezaji. Halikadhalika, upungufu mkubwa wa akiba ya fedha nchini unaathiri uwekezaji wa wazalendo kwa kuwapatia nyenzo na taaluma muhimu ili kushiriki kikamilifu

katika kuleta maendeleo. Mojawapo ya matatizo makubwa yanayoikabili Zanzibar ni ukosefu wa ajira kwa vijana wake. Wapo vijana wengi ambao wamefaidika na fursa za elimu ya juu kutoka vyuo vikuu vilivyopo Zanzibar na kuhitimu mafunzo ya fani mbali mbali lakini wameshindwa kupata ajira.

Ili Zanzibar iweze kuendelea, hakuna budi kuwepo mazingira muafaka kwa kuvutia uwekezaji. Katika kutimiza lengo hilo, Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itarekebisha sheria ya uwekezaji iwe bora zaidi na kuimarisha utekelezaji wa kweli uwavutie na kuwaridhisha wawekezaji.*
- *Itaweka mamlaka moja tu ya uwekezaji itakayokuwa na dhamana pekee ya kukuza na kusimamia uwekezaji pamoja na kutoa huduma zote kwa wawekezaji (one stop centre) kwa uwazi na ufanisi mkubwa na isiwe kumhangaisha mwekezaji kama ilivyoelezwa katika tafiti za Benki ya Dunia kuhusu Uwekezaji Zanzibar.*
- *Itaimarisha huduma zote za kiuchumi na kijamii na itawafuata na kuwavutia wawekezaji wazoefu na wenye uwezo mkubwa.*
- *Itaweka vivutio vilivyo bora zaidi (competitive) kwa uwekezaji na vinavyokwenda na wakati.*
- *Itaanzisha utaratibu endelevu wa kutathmini mafanikio na kasoro za sera nzima ya uwekezaji na vitega uchumi na kufanya marekebisho kila inapojitokeza haja ya kufanya hivyo.*
- *Itaangalia uwezekano wa kuwa na sera maalum ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar kuwekeza katika miradi mikubwa na endelevu kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali, ajira na tija kwa wanaohifadhi fedha katika mifuko hiyo.*
- *Itasimamia uanzishaji wa Benki ya Uwekezaji (Zanzibar Investment Bank) ambayo itakuwa ikitoa mikopo kwa lengo la kuwainua wawekezaji wa ndani kusudi waweze kuwekeza na kutoa mchango katika pato la taifa na pia kuongeza nafasi za ajira kupitia miradi itakayoanzishwa*

4.8. NGUVU KAZI

Ufanisi na tija ya nguvu kazi ilikuwa ni vigumu kuonekana kutokana na mgogoro wa kisiasa uliodumu kwa muda mrefu, maslahi yasiyoridhisha na ukosefu wa fursa za kujiendeleza. Hakuna maslahi mazuri ambayo yangeivunja nguvu rushwa. Hakuna mpango kazi wa maendeleo unaotekelezwa.

Mchango wa wastaafu katika maendeleo ya nchi hauheshimiwi ipasavyo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo:

- *Itarekebisha na kutekeleza sheria na taratibu zitazopelekea utumiaji mzuri wa nguvu kazi.*
- *Itarekebisha na kuweka mfumo mzuri wa maslahi kwa wafanyakazi.*
- *Itaunda na kutekeleza mpango unaofaa kwa mafunzo ya kazini na katika taasisi za elimu.*
- *Itasimamia sekta binafsi kulinda maslahi ya wafanyakazi na kuhakikisha sheria zinazowekwa zinafuatwa.*
- *Itaruhusu vyama vya wafanyakazi kuwa huru na haitaviingilia katika utendaji wake wa kazi.*
- *Itaweka utaratibu wa upimaji wa utendaji kazi na kuhakikisha utaratibu wa upandiswaji vyeo makazini utafuatwa.*

5. TUTAKUZA BIASHARA KWA KUONDOSHA URASIMU NA KUPUNGUZA VIWANGO VYA USHURU NA KODI

Zanzibar ni nchi ya Visiwa vidogo na hivyo ina changamoto nyingi za kiuchumi na kimaendeleo. Udogo wa ardhi yake, kuzungukwa kwake na bahari, matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi na kuongezeka kwa kina cha bahari, pamoja na changamoto na athari za kimazingira kwa uchumi na jamii yake kunaleta haja kubwa na ya haraka ya mapinduzi ya kiuchumi na kimaendeleo kwa jamii yake nzima katika kupambana na unyonge na umaskini unaowakabili na kuelekea katika taifa lenye hadhi ya uchumi wa kati. CUF inaamini kuwa njia pekee ya kuitoa Zanzibar katika janga la unyonge na umaskini na kubadilisha hali ya maisha ya watu ni kuitumia neema tuliyopewa ya kijiografia, maliasili na kihistoria kuigeuza Zanzibar kuwa kituo kikuu cha kibiashara cha Afrika ya Mashariki na Magharibi ya Bahari ya Hindi. Neema hii ipo katika sekta ya uagizishaji, uwekezaji katika maliasili za pwani na baharini kama utalii na uvuvi, miundombinu ya sekta mpya ya mafuta na gesi, bandari huru, na mabenki. Yote haya yatafanikiwa pale tutakapoweza kwa kauli moja kuitoa Zanzibar ndani ya sera zilizofeli za "kusawazisha uchumi" kwa jina la Muungano na kuifanya ipumue na sera zake wenyewe ndani ya Muungano wa Haki, Heshima na Usawa. Dira ya mabadiliko ya CUF ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inarejesha haki yake ya maamuzi katika ushuru, kodi na mapato.

5.1. UAGIZAJI WA BIDHAA

Usawazishaji wa kodi uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka 1999, pamoja na kuipunguzia sana mapato SMZ umeathiri vibaya sana ajira na mapato ya watu wengi wanaotegemea bandari na biashara kwa mapato yao. Hatuonekani kuwajali maelfu ya watu hao wanaojiajiri na kuipatia mapato makubwa serikali. Hata baada ya Usawazishaji huo wa kodi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inabagua bidhaa zinazopitia Zanzibar kwenda Tanzania Bara kwa kuziwekea vikwazo kwa kuzitoza kodi na ushuru mara mbili na kuacha huru zile zinazotoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Pia kunaonekana wazi kuwa kuna nia ya kuiua bandari ya Zanzibar na kuangusha uchumi wake ili Zanzibar ishindwe kujitegemea.

Halikadhalika, utitiri wa kodi unazifanya bidhaa zipitazo Zanzibar kuwa na bei kubwa na zisiuzike katika soko la nje.

Kwa kufuata mfumo wa uchumi wa soko huria, Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itairudisha Zanzibar katika hadhi yake ya kuwa kituo kikuu cha biashara na huduma katika eneo lote la Afrika Mashariki kwa kutekeleza sera zitakazoweka mazingira mazuri na yanayovutia ya kufanyia biashara na kuleta uwekezaji mkubwa.*
- *Itaimarisha zaidi miundombinu na huduma za bandari zetu na viwanja vya ndege ili viwe na uwezo wa ushindani na ufanisi zaidi katika eneo la Afrika Mashariki na Magharibi ya Bahari ya Hindi.*
- *Itafungua milango ya biashara kwa kuitangaza Zanzibar kuwa Bandari Huru (Free Port) ili kuwavutia wafanyabiashara wenye kulenga soko la Afrika ya Mashariki na Kati. Lengo la sera hizi ni kufikia ile ndoto ya muda mrefu ya kuifanya Zanzibar kuwa Singapore ya Afrika Mashariki.*
- *Itahakikisha shughuli za uingizaji bidhaa nchini zinafanyika kwa uwazi, bila ya usumbufu kwa wateja, na kwa uharaka na ufanisi mkubwa lakini pia katika viwango vidogo kabisa vya ushuru na kodi kulingana na uchumi wa nchi yenyewe ya Kisiwa.*
- *Itatoa kipaumbele katika kutengeneza mikakati na mipango kazi ya uingizaji wa vifaa vya miundombinu ya sekta ya mafuta na gesi katika kuharakisha na kurahisisha maendeleo ya sekta hii ya mafuta na gesi.*
- *Itashirikiana na washiriki wa kibiashara wa kikanda katika utekelezaji wa misingi ya "Transit Trade" kwa ajili ya nchi zisizo na bahari (Landlocked States) za Afrika.*

5.2.UAGIZISHAJI WA BIDHAA YA MAFUTA

Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa kuwa wazi katika ukiritimba na uhodhi wa biashara wa baadhi ya wafanyabiashara wachache wanaonekana kuwa na ushawishi wa kisiasa. Kuna upotevu mkubwa wa fedha za umma katika biashara hii. Bei ya mafuta imekuwa ikipandishwa mara kwa mara kufidia upotevu wa mapato. Kupanda huko kwa bei ya mafuta kunapelekea kuongezeka kwa bei ya huduma zote na bidhaa nyingi na matokeo yake ni kumtwika mzigo mkubwa sana mwananchi wa kawaida.

Vile vile tunaona ongezeko la matumizi ya gesi ya kupikia (LPG), ambalo ni jambo la faraja kwa vile litasaidia sana kupunguza matumizi ya makaa na hatimae kupunguza ukataji wa miti. Hata hivo bidhaa hii inaonesha kutokudhibitiwa na kuonekana kuuzwa kiholela, jambo ambalo linaweza kuleta madhara makubwa pindipo pakitokea hitilafu katika mitungi hiyo ya gesi.

Baada ya kilio cha muda mrefu, Zanzibar imeanzisha Taasisi mpya ya Udhibiti ya Huduma ya Zanzibar (ZURA). Hata hivyo Taasisi hii inahitaji kuwezeshwa vyema ili kuweza kufanya majukumu yake kwa ufanisi kwa kuipatia nyenzo kama vile ofisi, rasilimali watu na vitendea kazi ili kuweza kuidhibiti biashara ya huduma za mafuta, umeme, maji na gesi za matumizi ya nyumbani ili kuleta ufanisi, usalama na kuondoa usumbufu wa upatikanaji na upandaji holela wa bei za bidhaa hizi.

Serikali imeshindwa kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa mafuta na kusababisha upungufu wa mara kwa mara unaozorotesha utendaji katika sekta zote. Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itahakikisha kuwa kila Mzanzibari mwenye uwezo wa kufanya biashara ya uagizaji mafuta kutoka nje basi anapata fursa hiyo kwa mujibu wa sheria na viwango.*
- *Bila ya kuathiri mpango wa bajeti wa taifa, Serikali itashirikiana na waagizaji na wawekezaji wa mafuta katika kudhibiti mfumuko wa bei ya mafuta kwa wananchi na kwa kuzingatia soko la bidhaa za mafuta la dunia.*
- *Itaongoza kwa njia ya uwazi fursa sawa kwa wakala wote wa biashara ya mafuta kuendesha biashara hiyo kwa kufuata kanuni na taratibu halisi zilizowekwa.*
- *Itamlinda mwananchi dhidi ya ukitirimba wowote wa biashara ya mafuta unaofanywa kinyume na sheria.*
- *Itaunda sera na sheria mpya inayohusu usimamizi wa uagizaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaji wa gesi ya kupikia (Cooking Gas) ili kudhibiti biashara holela ya bidhaa hii kwa usalama na viwango vya bidhaa yenyewe.*
- *Itaweka kipaumbele kwa mamlaka ya ZURA ili kuhakikisha inasimama wenyewe kwa muda mfupi na kuondoa kero kwa wananchi wetu.*

5.3. USAFIRISHAJI WA MAZAO YA KILIMO NA BAHARI

Ubinafsishaji wa zao la karafuu umekuwa ni mada nyeti sana katika maisha yetu. Serikali siku zote imekuwa ni msimamizi mkuu wa zao hili katika uzalishaji, usafirishaji, utafiti, na uendelezaji wake. Malalamiko mara nyingi yamekuwapo katika kumpatia faida ya kweli mkulima wa zao hili na hapo ndipo pamekuwa pakitokea suitafahamu baina ya Serikali na wakulima na kupelekea kudorora kwa zao hili.

Hata hivyo, marekebisho makubwa yaliweza kufanyika mara tu baada ya maridhiano na hali ya mkulima kwa kiasi imekuwa ikiendelea kunyanyuka japokuwa na changamoto mbali mbali. Lakini mafanikio haya yanatakiwa kusimamiwa zaidi yaendelee kulinyanyua tena zao hili.

Lakini hakuna njia thabiti kama zile za ufufuaji wa zao la karafuu ambazo zimechukuliwa kuwasaidia wananchi kuendeleza uzalishaji na uuzaji wa mwani. Yote haya yanafanyika katika hali ambayo mazao ya matunda na viungo pamoja na mazao mengine ya bahari Zanzibar yamekosa kabisa sera bunifu za uwekezaji na usafirishaji.

Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kuendeleza Maeneo Huru ya Fumba na Micheweni kutengeneza na kusafirisha bidhaa kama hizi nchi za nje (EPZ). Pia, Serikali inayoongozwa na CCM inaonekana imeridhika na kusafirisha bidhaa ghafi na kupelekea bidhaa hizo nje zikiwa na thamani ndogo katika soko la kimataifa bila ya kujali maslahi ya wakulima wa mazao haya.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo katika kurekebisha hali hii:

- *Itaendelea kubuni mbinu mbali mbali mbadala za kumwezesha mkulima wa biashara ya karafuu kuweza kupata maslahi zaidi ya jitihada zake chini ya usimamizi wa Serikali.*
- *Itaipa msukumo sekta binafsi kuimarisha kilimo, uchambuaji na uuzaji nje wa viungo na kushindana katika soko la nje.*
- *Itaunda sera bunifu za uwekezaji, uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya bahari kama vile mwani, kaa, chaza, majongoo ya pwani, samaki wa kufuga, n.k. pamoja na kuongeza mpango kazi wa kuwasaidia wananchi wanaojishughulisha na sekta hii.*
- *Itaviondoa vipingamizi vyote vinavyozuia maendeleo ya Maeneo Huru na Bandari Huru kwa kuimarisha huduma muhimu za kiuchumi na kijamii, kuimarisha mfumo wa sheria, kutangaza Zanzibar mpya iliyotokana na Maridhiano, pamoja na kuwashajiisha Wazanzibari wa ndani na nje washiriki katika maeneo haya ya kiuchumi.*
- *Itajitahidi kuingiza teknolojia mpya ya kuziongezea thamani bidhaa zinazokusudiwa kusafirishwa kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo humu humu nchini.*

5.4. VIWANDA NA UZALISHAJI

Sekta ya uzalishaji viwandani inachangia chini ya asilimia 3 ya Pato la Taifa. Hali hii mbaya inatokana na dhamira ya makusudi ya kuhakikisha Zanzibar haiendelei kiviwanda. Inasikitisha sana kuona kuwa karibuni viwanda vyote vilivyokuwepo kabla na baada ya Mapinduzi vimekufa.

Viwanda binafsi vilivyoanzishwa katika miaka ya karibuni vimeshindwa kuhimili ushindani na Tanzania Bara na soko zima la Afrika Mashariki kwa sababu ya kodi na tozo kubwa za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Viwanda vichache sana ndivyo vilivyopo na hivi peke yake haviwezi kuleta tija yeyote ya kitaifa kwa ujumla.

Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa kuweka huduma muhimu za kiuchumi na kijamii zinazolenga katika utekelezaji na uendelezaji wa shughuli za viwanda hapa Zanzibar. Bado hakuna sera wala mipango kazi madhubuti nchini ya kukaribisha fursa mbali mbali za uwekezaji katika viwanda. Sera ya viwanda hakuna. Miundombinu ya kuwa na sekta bora ya viwanda bado haipo. Vivutio (incentives) vya kuwezesha uimarishaji wa sekta ya viwanda hakuna. Na pia hakuna maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kujenga viwanda vya kudumu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo katika kurekebisha hali hii:

- *Itaunda Baraza la Taifa la Viwanda ili kuimarisha ushirikiano wa dola na jamii kwa masuala yanayohusu uendelezaji wa sekta binafsi.*
- *Itahakikisha kwamba mambo yatakayopewa kipaumbele katika kukuza sekta ya viwanda ni yale yanayohusika*

kwa karibu na maliasili zetu zilizopo nchini.

- *Itahakikisha kwamba inaelekeza sehemu ya kutosha ya matumizi ya umma katika kukuza mfumo muafaka na unaovutia wa kifedha, kisheria, kijamii na kiteknolojia ambamo wenye viwanda wanaweza kuendeleza shughuli zao kwa ufanisi.*
- *Itaunda sera ya viwanda inayokwenda sambamba na mabadiliko ulimwenguni.*
- *Itahakikisha kuna mahusiano mazuri viwandani na uongozi bora wa mashirika ya serikali.*
- *Itatenga maeneo maalum ya kujenga viwanda vya kudumu.*
- *Itashajiisha wawekezaji wa kibenki kufungua mabenki ya viwanda.*
- *Itahakikisha kuwa Mamlaka ya Viwango Zanzibar (Zanzibar Bureau of Standards) inafikia hadhi ya ushindani wa kimataifa kupitia mashirikiano zaidi na Taasisi ya Viwango Ulimwenguni (International Standardization Organization).*

5.5. SEKTA ISIYO RASMI (JUA KALI)

Wafanyabishara ndogo ndogo wanaojishughulisha na sekta hii (Jua Kali) wamekuwa wakipewa usumbufu, vitisho visivyokwisha na unyang'anyi wa kimacho macho wa mali zao. Hakuna mazingira muafaka ya kiutendaji kwa sekta isiyo rasmi. Hakuna usalama wa mali ya wafanyabiashara katika sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi inaumizwa na mzigo mzito wa kodi isiyolipika. Serikali haijaonyesha kutambua na kuthamini kabisa sekta hii hadi kuonekana kama inaipiga vita.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo:

- *Itaheshimu na kuthamini sekta isiyo rasmi na kuwapa nguvu wale walioamua kujiendeleza kwa kujiajiri na kuzalisha mapato.*
- *Itawawekea wajasirimali wa Jua Kali mazingira mazuri na endelevu sekta hiyo isiyo rasmi iweze kustawi.*
- *Itaweka na itasimamia taratibu za kisheria zinazosaidia kuongoza shughuli hizo na mali zao.*
- *Itaondoa urasimu na kupunguza mzigo wa kodi kwa sekta isiyo rasmi.*
- *Itasaidia katika utoaji wa elimu ya uwezeshaji wa kitaaluma (Capacity building) pamoja na kutafuta miundombinu endelevu na ya kibinadamu kwa wafanyabiashara wake.*

5.6. UKUZAJI WA UTALII

Sekta ya Utalii imekuwa katika kasi ya kuridhisha na hata kufikia mahala Serikali imetangaza kwamba imelipiku zao la karafuu kama chanzo kikuu cha mapato ya fedha za kigeni kwa Zanzibar. Serikali imetangaza kwamba idadi ya watalii wanaoingia Zanzibar imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Hili ni jambo la kutia moyo hata kukitiliwa maana kuwa Zanzibar ni nchi ya uwekezaji.

La ajabu ni kuwa ukusanyaji wa mapato umekuwa ukishuka kila mwaka. CUF inaamini kuwa Serikali inayoongozwa na CCM haina Sera ya Utalii iliyo muafaka na iliyopangika kulingana na umuhimu ambao sekta hii imekuwa nayo katika uchumi wa Zanzibar. Kwa nini basi pamoja na mafanikio yote hayo tunayoelezwa, Zanzibar ibaki kuwa nchi yenye umaskini mkubwa takriban miaka 30 sasa tangu uwekezaji katika utalii ulipoanza?

Suala la vivutio limekuwa ni mtihani mwengine kwa sekta hii. Pamoja na kuwepo vivutio vya maliasili za ufukweni na baharini, bado sekta ya utalii Zanzibar haijaweza kuunganishwa na sekta nyingine za kibiashara na uwekezaji katika utoaji wa huduma kwa watalii.

Bado Wazanzibari hawajapata fursa inayostahiki ya kupata ajira katika sehemu za utawala (Managerial Position) za uendeshaji wa hoteli. Hakuna fursa

za kuwawezesha Wazanzibari kuhitimu katika sekta ya utalii kwa viwango vya kimataifa.

Halikadhalika, Serikali inayongozwa na CCM imeshindwa kuwavutia wawekezaji wa mahoteli ya kitalii ya daraja la kwanza. Imeshindwa kuitangaza Zanzibar kwa watalii wa hadhi ya juu. Imeshindwa kuweka utaratibu mzuri kiutawala na kiuchumi na kukusanya mapato ya utalii hasa mahotelini na katika makazi yasiyo rasmi. Lakini pia, ukuzaji wa utalii kwa wakati huu ni wa kushtukia na kubahatisha tu wakati huduma kwa ajili ya utalii wa ndani ni finyu.

Hakuna kinga dhidi ya tabia za kuchafua mazingira katika maeneo muhimu yanayowavutia watalii. Na mfumo huu uliopo unaolelewa na Serikali ya CCM umeshindwa kuiepusha jamii na taathira mbaya zinazotokana na utalii, hasa kiutamaduni na kijamii au kutoa taaluma ya kutosha kwa wafanyakazi wa sekta hii na kusababisha wawekezaji kuagiza wafanyakazi kutoka nje, hivyo kupelekea Wazanzibari kukosa ajira.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itaanzisha sera muafaka ya utalii endelevu (Sustainable Tourism) inayojali usawa wa kijamii (social equity) katika maslahi yao mbali mbali kama vile maji safi, nishati, barabara, matumizi ya haki ya umiliki wa ardhi, malisho ya mifugo, kilimo, madiko yao ya uvuvi pamoja na maeneo yao ya kuvulia ya mwambao.*
- *Itatekeleza mkakati maalum wa kuwavutia wawekezaji wa mahoteli ya kitalii ya daraja la kwanza kwa kuwekeza zaidi katika miundombinu ya mahoteli, barabara, mawasiliano, maji, nishati na ardhi.*
- *Itatekeleza mpango madhubuti wa kuitangaza Zanzibar kwa watalii wa hadhi ya juu.*
- *Itaimarisha maeneo yote ya vivutio vya watalii kwa kuhakikisha vinatunzwa na kuenziwa na kuwekwa katika mazingira ya usafi yanayoendana na viwango vya kimataifa ili kuikuza Zanzibar kama kituo cha watalii wa daraja la juu*
- *Itahakikisha uhifadhi wa visiwa vidogo vidogo vilivyo kando ya Unguja na Pemba pamoja na maeneo ya asili ya viumbe vya baharini.*
- *Itaimarisha na kukuza uwezo uliopo wa kukusanya mapato ya serikali katika sekta ya utalii ili kukuza na kupanua ukusanyaji.*
- *Itachukua hatua muafaka za kuzuia utalii usiathiri na kubadili hazina ya utamaduni mzuri wa Zanzibar pamoja na kuhifadhi mazingira yake.*
- *Itaongeza zaidi ubunifu wa vivutio kwa watalii ili waongeze siku za kukaa nchini na hivyo kukuza pato la Taifa linalotokana na utalii.*
- *Itasomesha vijana wa kutosha wa masomo ya utalii kwa ngazi zote ili waweze kuajiriwa katika soko la utalii hasa katika maeneo ya ngazi za juu*
- *Utalii wa kibiashara, utalii wa tiba na vivutio vinginevyo vitawekewa vipaumbele maalum vya mipango ya taifa.*
- *Itahakikisha Sheria ya kamisheni ya utalii inaweka kipaumbele kwa Wazanzibari.*



6. TUTAENDELEZA KILIMO, MIFUGO NA KUIMARISHA SEKTA YA UVUVI

Ni dhahiri kuwa Kilimo, Mifugo, na Uvuvi ni kiini cha maisha yetu ya kila siku. Takriban kila Mzanzibari kwa njia moja au nyingine anajishughulisha na mojawapo ya sekta hizi ama kwa kujipatia riziki au kwa biashara. Wakati nchi nyingi duniani zimepita katika Mapinduzi ya kasi ya kilimo, mifugo na uvuvi (Green and Blue Revolution) na kubadilisha hali za maisha za wananchi wake, bado katika visiwa vyetu hivi kuna pengo kubwa la kufikia malengo hayo na hatimaye kubadilisha maisha ya mwananchi. CUF inaamini kuwa ukosefu wa sera thabiti shirikishi, mipango bora ya kitaifa yenye vipaumbele vinavyolenga matakwa ya mwananchi katika kufikia malengo ya usalama wa chakula na lishe bora, ikiwemo uwezeshaji wao katika uzalishaji na ufikiwaji wa masoko ya ndani na nje, umechangia kwa kiasi kikubwa kwa wananchi wetu kuendelea kukwama katika wimbi la umaskini, kukata tamaa, na maisha duni. Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa kuliona hili na bado inaendelea kutekeleza sera na mipango ile ile iliyokosa dira na malengo kwa kulazimisha utekelezaji wa sera zilizokosa ushirikishwaji wa matakwa ya mwananchi. Mapinduzi ya sekta hii yatafanikiwa pale ambapo matakwa na vipaumbele vya wananchi vitakaposikilizwa na kutekelezwa ipasavyo. Serikali ya Wananchi itakayoongozwa na CUF itakuwa tayari kuubadili muundo mzima wa uendeshaji wa sekta hizi na kuleta Mapinduzi ya kweli ya Kilimo (Green Revolution) na Uvuvi (Blue Revolution).

6.1. UZALISHAJI WA MAZAO

a) Mpunga

Mabonde ya mpunga yasiyopungua hekta 8,000 bado hayajaweza kuendelezwa kwa ukamilifu. Yale yaliyoweza kuendelezwa kwa kiasi miaka ya nyuma yanazidi kupotea kutokana na kukosekana kwa maji, pembejeo, sera na mipango madhubuti ya uzalishaji na masoko. Lakini pia upanuzi wa matumizi ya ardhi ikiwemo ujenzi holela wa makaazi na shughuli nyingine zisizo za kilimo ndani ya ardhi yenye rutuba pia imesababisha kukatwa miti mingi, hasa mikarafuu na minazi na kupotea kwa misitu na ardhi yenye rutba.

b) Miwa na Sukari

Uzalishaji wa miwa Mahonda umeingia katika migogoro isiyoisha baina ya mwekezaji na wananchi na hali imekuwa mbaya zaidi kwa Serikali iliyopo kushindwa kusimamia haki na uadilifu baina ya wananchi na wawekezaji binafsi wa sekta hii ya sukari. Lakini wakulima wa miwa wanaendelea kubezwa na maslahi yao kupuuzwa.

c) Matunda

Zanzibar ina aina nyingi za matunda, lakini hakuna hata kiwanda kimoja cha kusindika matunda ili kuongeza pato la Taifa na kutoa ajira kwa vijana. Matunda mengi yanaozeana mitini. Hakuna takwimu sahihi za kitaifa zinazoonekana kupima hali halisi ya matunda Zanzibar. Mara nyingi umuhimu wa mazao kama Shokishoki, Mananasi, Matofaa, Embe, na Madoriani umekuwa ukibezwa na hata kukosa nafasi katika sera na mipango ya taifa.

d) Mafuta ya Nazi na Usumba

Viwanda vya mafuta ya nazi na usumba vilivyokuwepo navyo vimekufa mbali na kushindwa kuanzisha viwanda vyengine ambavyo vingeweza kuipa nguvu sekta ya kilimo.

Katika kuzishughulikia changamoto hizi na kufikia azma ya Mapinduzi ya kweli ya kilimo na uzalishaji, Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza yafuatayo:

- *Itaiendeleza sekta nzima ya kilimo na kukirejeshea hadhi yake kama moja ya njia kuu za uchumi inayotegemewa na wananchi wetu walio wengi hasa wa vijijini.*
- *Itaondoa vizingiti vyote vinavyowabana wakulima na kuwaruhusu kuingia moja kwa moja katika soko la ndani na nje la mazao yao.*
- *Itashirikiana kwa ukaribu zaidi na washiriki wa sekta zisizo za kiserikali pamoja na vyama vya wakulima wa mazao mbali mbali katika kushajiisha uzalishaji na usafirishaji zaidi wa mazao yao nje.*
- *Itayapitia upya mapendekezo ya marekebisho ya muundo mzima wa usimamizi wa uzalishaji, ununuzi na usafirishaji wa mazao na hususan nafasi ya Shirika la Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC).*
- *Itapitia upya athari za makubaliano ya uwekezaji katika sekta za zao la mpira na miwa (Sukari) kwa ajili ya maslahi na haki za wakulima na wananchi kwa ujumla.*
- *Itaongoza mchakato ulio wazi wa kitakwimu, uendeshaji, uzalishaji, na mapato yatokanayo na karafuu, mpira, na miwa.*
- *Itaangalia upya muundo na mipango ya mradi unaopendekezwa wa kilimo cha umwagiliaji katika mabonde yanayolimwa Unguja na Pemba ili kuhakikisha maslahi ya wakulima na haki zao za umiliki na matumizi ya ardhi katika sehemu hizo hayapotei na kuwa mradi hauna athari mbaya kwa mazingira na maji ardhi.*
- *Itayafanyia kazi manung'uniko ya wakulima na wananchi wa mashamba ya miwa na sekta ya sukari Mahonda katika kuhakikisha uwazi na uadilifu wa mradi wenyewe na haki za wenyeji.*
- *Itatilia mkazo kilimo cha viungo ((pilipili, mdalasini na hiliki n.k.), matunda na mboga mboga ili tuendelee kutumia vyema soko linaloweza kupatikana kutokana na jina maarufu la Zanzibar kama visiwa vya viungo.*
- *Itaanzisha program kabambe za kukuza kilimo cha mpunga kupitia umwagiliaji maji pamoja na matumizi bora ya teknolojia ili kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa zaidi ya mara tatu ya hali ilivyo sasa.*
- *Itawasaidia wakulima wadogo wadogo kwa kuwafundisha mbinu za kisasa, kuwapa zana, soko na bei nzuri ya mazao yao.*
- *Itafanya mazungumzo na washirika wa maendeleo wa kimataifa yenye lengo la kuipatia Zanzibar mkopo nafuu wa kuchechemua uchumi wa vijijini kwa kuunga mkono hatua za ukuzaji wa kilimo kupitia ununuzi na ukopeshaji wa matrekta na pembejeo kwa vikundi mbali mbali vya wakulima rasmi vinayojishughulisha na kilimo visiwani Unguja na Pemba.*
- *Itaanzisha mfuko rasmi wa kulea na kukuza uzalishaji kwa wakulima (Agricultural Incubator Fund) kwa ajili ya kilimo cha kibiashara. Mfuko huu ambao utakuwa ni wa kudumu utalenga katika kuwasaidia wakulima nchini kote kuanzisha kilimo cha kibiashara kwa kuwapa uwezo wa kununulia matrekta, vifaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa maghala, pembejeo na kadhalika.*
- *Itatoa leseni za biashara kwa wafanyabiashara binafsi kuuza nje aina zote za mazao yao na kuwapa motisha ya kukuza uzalishaji.*
- *Itapunguza ukulima wa kutumia jembe la mkono na kutegemea mvua na badala yake kuendeleza ukulima wa kutumia matrekta (ikiwa ni pamoja na matrekta madogo madogo ya mkono) na kutoa msukumo mpya wa kilimo cha umwagiliaji.*
- *Itashajiisha uanzishwaji wa jumuiya za wakulima ili kuwawezesha kulinda maslahi yao.*
- *Itashajiisha kilimo cha mazao mengine ya chakula na biashara ili kuhakikisha Zanzibar inajitegemea kwa chakula.*
- *Itaimarisha Chuo cha Kilimo Kizimbani na vituo vya utafiti wa kilimo na majaribio*

ya mimea na utafiti wa kilimo pamoja na kuwezesha upatikanaji wa kuingiza zana na mbinu za kisasa ili kukuza sekta ya kilimo na kuongeza mchango wake kwenye pato la Taifa.

- *Itasaidia katika kutafuta na kuvutia wawekezaji watakaojenga viwanda vya kusindika matunda, mboga mboga na viungo ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na bidhaa zake kwa lengo la kuinua soko lake la nje na pia kuongeza pato la nchi kupitia bidhaa zinazouzwa nje.*
- *Itaandaa mazingira bora ya kutumia fursa za soko la bidhaa mbali mbali zinazopatikana kwenye sekta ya utalii ili kuwafaidisha wakulima na kuwainua kiuchumi.*
- *Itatilia mkazo matumizi ya teknolojia mbali mbali za kilimo ikiwa ni pamoja na kushajiisha utengenezaji na utumuaji wa mbolea za kioganiki kwa kutumia fursa ya upatikanaji wa taka taka za majumbani ili kuongeza uzalishaji wa mazao bora unaotilia mkazo hifadhi ya mazingira.*

6.2. UHUISHAJI WA SEKTA YA MIFUGO

Ufugaji kwa Zanzibar bado unafanywa kwa njia za kienyeji na haujatoa mchango mkubwa katika uchumi wa taifa. Wananchi wa Unguja na Pemba wanaoishi katika ardhi yenye rutuba nzuri na wamekuwa na utamaduni mzuri wa ufugaji na iwapo ufugaji utapewa msukumo unaweza kuchangia vizuri katika kunyanyua hali za maisha ya wafugaji wetu na hata kuchangia katika pato la taifa. Wawekezaji binafsi wa Kizanzibari wameonyesha njia kwamba tukiamua tunaweza hata kuwa na viwanda vya bidhaa zitokanazo na mifugo ikiwemo, maziwa, samli, siagi na jibini.

Ni dhahiri kabisa kuwa umaskini umeshamiri miongoni mwa wafugaji kutokana na kukosa maelekezo ya kitaalamu endelevu na kutokuwepo kwa msukumo kutoka Serikalini wa jinsi gani wanaweza kuinyanyua sekta hiyo. Katika maeneo mengi ya mashamba uzalishaji wa mifugo umeshuka kutokana na ukame, ukosefu wa mbegu bora na chakula bora, ukosefu wa matibabu ya kutosha, huduma za kitaalamu na uwezo wa kuhimili gharama za ufugaji. Uwekezaji katika sekta hii umedharauliwa na hivyo kuufanya ufugaji kubaki ukifanywa kwa njia za kienyeji mno.

Ili kuinyanyua sekta ya ufugaji na kuifanya itoe mchango wake stahiki katika ujenzi wa uchumi, Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUFitachukua hatua zifuatazo:

- *Itazihuisha na kupanua huduma za hospitali za mifugo na majosho angalau katika kila wilaya.*
- *Itahakikisha kuwa wafugaji wanapata fursa sawa ya kupata mikopo ya uhakika ya uzalishaji na uendeshaji.*
- *Itashajiisha kuundwa jumuiya za wafugaji kulinda maslahi yao na kuongeza uzalishaji wa mifugo.*
- *Itashajiisha wakulima kupanda majani ya kulisha wanyama kwa kutumia umwagiliaji wakati wa kiangazi.*
- *Itaongeza nafasi za masomo kwa madaktari wa mifugo pamoja na kuwapa vivutio vizuri ili wabaki makazini.*
- *Itawavutia wawekezaji madhubuti na kuwapa motisha wale ambao tayari wamewekeza kwenye sekta hii.*
- *Itakuza sekta ya mifugo na uzalishaji wake na kutumia soko linalopatikana katika sekta ya utalii.*

6.3. UVUVI NA UCHUMI BULUU

Bahari yetu bado ina hazina kubwa ya samaki ambayo haijaguswa. Zanzibar kama visiwa vilivyozungukwa na bahari vina utajiri wa samaki wakubwa na wa aina mbali mbali. Uvuvi ni sekta kuu muhimu ya uzalishaji mali inayotoa ajira ya moja kwa moja kwa wavuvi wasiopungua 35,000 na wanaovua kunako mwambao wa visiwa vya Unguja na Pemba. Lakini pia sekta hii huajiri wananchi wengine zaidi wasiopungua 4,000 katika njia moja au nyingine.

a) Uvuvi kwa Ujumla

Rasimu ya karibuni ya sekta ya uvuvi iliofanywa na Kamisheni ya Bahari ya Hindi kupitia Mradi wa *SmartFish* unaonyesha kuwa uvuvi wa samaki ulifikia tani 29,000 kwa mwaka 2012 na kuingizia wastani wa thamani ya Shilingi Bilioni 103.1/- au Dola za Kimarekani US$ Milioni 64. Uzalishaji katika sekta hii ya uvuvi katika kipindi cha miaka kumi na mbili ulionyesha wastani wa ongezeko la asilimia 4.3% kwa mwaka. Takwimu pia zinaonyesha kuwa madiko 30 rasmi ya wavuvi ndiyo yanayotambuliwa, ukilinganisha na madiko na bandari bubu nyingine nyingi ambazo bado, kwa sababu moja au nyingine, hazitambuliwi rasmi.

Ni ukweli usiopingika kuwa kitoweo cha samaki ni chanzo kikubwa kabisa cha "protein" kwa wananchi wa Zanzibar na kuwa kwa wastani kila Mzanzibari hutumia kilogramu 20 za samaki kwa mwaka, kiwango kikubwa katika bara la afrika. Lakini sekta hii imeachwa bila ya kuendelezwa na hakuna juhudi na hatua makhsusi za kuihudumia na kuiendeleza sekta hii ipasavyo. Kwa kiasi kikubwa uvuvi unaendelea kuwa wa kienyeji kuliko wa kisasa na kitaalamu, umejikita zaidi karibu na mwambao, na wavuvi hawana vyombo vya kuaminika wala zana za kisasa.

b) Migogoro baina ya Wavuvi na Watalii

Hakujafanyika jitihada za kuwasaidia wavuvi kusafirisha samaki nchi za nje. Zaidi ya asilimia 90 ya samaki huliwa au kuharibika nchini. Uvuvi haramu umeongezeka na kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa baharini. Uharibifu wa matumbawe na maeneo ya mengine ya mwambao wa bahari unaendelea bila jitihada zozote za kutafuta suluhisho la kudumu. Ugomvi na migorogo baina ya wavuvi wa mwambao na watalii wa matumbawe umekithiri na kufikia hadi kuhatarisha maisha ya watalii. Jumuiya za kitalii zimefikia kulalamikia sana utungwaji kiholela wa kanuni za uhifadhi wa bahari zinazolenga kuwakamua kimapato kuliko kuijikita katika uhifadhi wa kweli wa mwambao na matumbawe yake.

c) Kukosekana kwa Sheria Mama ya Uhifadhi wa Bahari

Hakuna sheria yeyote iliyoundwa kupitia Baraza la Wawakilishi *(Marine Protected Areas Act)* ya utangazaji wa mipaka ya maeneo ya uhifadhi wa bahari *(Marine Protected Areas)* na kutoa ugawaji wa maeneo *(Zonation)* katika hali ya uwazi na ushirikishwaji ili kuepusha mizozo na migogoro baina ya shughuli za uvuvi na utalii. Badala yake, watawala wa taasisi husika wanatunga kanuni wanavyojitakia; kanuni zinazokandamiza haki na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya mwambao wa bahari na kulazimisha kutoza kwa kiasi kikubwa na bila ya mpangilio au utaratibu wowote wa sekta ya kifedha na mapato ya nchi.

d) Kukosekana kwa Uwazi na Uadilifu katika Usimamizi wa Uvuvi

Ndio maana kukosekana kwa uwazi wa kitaasisi katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za uvuvi na uhifadhi wa maeneo ya bahari kumeleta suitafahamu kubwa kati ya wavuvi wengi na Serikali iliyopo madarakani inayoongozwa na CCM. Migogoro ya matumizi ya maeneo ya hifadhi za mwambao kama vile visiwa vidogo vya Kwale, Nyamembe, Mnemba, Tumbatu na Fundo imeshadidiwa na watawala na kuamuliwa katika misingi ya ufuasi wa kisiasa. Haki na uwazi kwa wananchi wanyonge inaendelea kunyimwa na badala yake utashi wa kisiasa na kulazimishana kwa maslahi ya wachache umetawala. Suala hili haliwezi kufumbiwa macho milele. Wahusika wa migogoro hii ni lazima wawajibike kwa mujibu wa sheria.

e) Suala la Kisiwa cha Fungu Mbaraka

Suala la uvuvi kando kando ya Kisiwa cha Fungu Mbaraka (*Latham Island*) limezua mjadala mkubwa katika Baraza la Wawakilishi. Haki ya umiliki wa eneo hili ipo wazi. Pamoja na yote, inashangaza kuona suala hili limefumbiwa macho na Serikali inayoongozwa na CCM na matokeo yake ni kuona Zanzibar ikikosa haki zake katika sekta ya uvuvi, lakini pia na katika suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi kunako mwambao wa Kisiwa hicho. Matokeo yake ni kuwa Kisiwa cha Latham Island kimebaki kuwanufaisha zaidi wavuvi wa kitalii wa nje

wanaofika hapo kutokea nje ya Zanzibar na hivyo kusababisha Serikali kupoteza mapato makubwa na kuwaacha wavuvi wa Zanzibar katika hali ngumu.

Fungu Mbaraka imebaki kuwa chanzo cha mapato ya wachache wanaopeleka watalii wao wa kivuvi kimya kimya kwa kutumia vyombo vya dola na mawakala wageni wasiokuwa na sifa kwa mujibu wa Sheria ya Utalii ya Zanzibar wanaotuhumiwa. CUF inaamini kwa nguvu zote kuwa huu ni ufisadi unaoikosesha mapato Serikali na unaopaswa kukomeshwa mara moja na kwamba ni lazima wahusika wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria.

f) Uvuvi wa Bahari Kuu, UNCLOS na EEZ

Zanzibar ilitegemewa iwe imeendelea sana katika uvuvi wa bahari kuu lakini suala hili halijapewa kipaumbele katika mipango na sera za kudumu za nchi hususan katika sekta ya maendeleo ya uvuvi. Ingawa kumeanzishwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania (Tanzania Deep Sea Fishing Authority) bado kuna migongano ya kitaasisi na hasa ikitiliwa maanani kuwa kuna mamlaka mbili tofauti zinazosimamia uvuvi wa mwambao katika Jamhuri ya Muungano. Hili linaizorotesha mamlaka iliyopo ya Uvuvi wa Bahari Kuu hasa pale panapotakiwa kufanywa maamuzi ya kisera na mipango pamoja na kujengwa miundombinu mbali mbali ya kupakua, kusindika na kusafirisha mazao ya samaki wa bahari kuu nje ya nchi.

Suala la Eneo Maalum la Uchumi wa Bahari Kuu (Exclusive Economic Zone) pamoja na kuwa ni suala linalosimamiwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari (United Nations Convention on the Law of the Sea au UNCLOS) ni suala la kihistoria kwa Zanzibar na kuwa hata katika muundo wa Umoja Mataifa unayoitambua Jamhuri ya Muungano, bado Zanzibar ina haki zake ndani ya Jamhuri ya Muungano ya kufaidika na maliasili za bahari kuu ikiwemo uvuvi na mafuta na gesi.

CUF tunasema kuwa Zanzibar, kama nchi ya Kisiwa iliyozungukwa na bahari, haiwezi kuzipoteza haki hizi. Na katika muungano wa haki, heshima na usawa, ni wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhakikisha kuwa inaitambua haki hiyo ya ushirikishwaji kikamillifu wa Zanzibar katika utekelezaji wa sera, mipango, na maamuzi yanayohusiana na Mkataba wa UNCLOS na usawa katika matumizi na faida za kuwa na eneo la EEZ.

g) Uvuvi wa Kikanda (Regional Fisheries Management)

Usimamizi wa uvuvi wa kikanda (Regional Fisheries Management) kwa upande wa Bahari ya Hindi upo chini ya taasisi iitwayo Indian Ocean Tuna Commission (IOTC). Kamisheni hii ya kiserikali ya nchi za ukanda wa Bahari ya Hindi inajishughulisha katika kuhakikisha mashirikiano na mawasiliano katika utekelezaji wa uvuvi endelevu na uhifadhi wa samaki wa aina ya jodari na wale wengine wanaofanana ndani ya maeneo ya EEZ ya nchi washirika. CUF tunasema hatuoni sababu za msingi zinazoizuia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokuwa na ushirikishwaji au uwakilishi wa kudumu katika mashirikiano haya. Je, kuna ubaya gani wa mamlaka yeyote ya Muungano ulio wa haki na usawa inayojishugulisha na masuala ya msingi kwa maisha ya Wazanzibari kama uvuvi na bahari, kutambua umuhimu wa ushirikishwaji na uwakilishi wa Zanzibar katika mikataba na itifaki za kikanda au kimataifa ndani ya Muungano huu? CUF tunasema kuwa wakati umefika kwa maslahi ya nchi kuwekwa mbele kwanza.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo katika kuinua sekta ya uvuvi Zanzibar:

- *Itauangalia upya muundo mzima wa sheria na usimamizi wa sekta ya maendeleo ya uvuvi Zanzibar katika kuhakikisha ufanisi wake pamoja na kulinda maslahi na haki za wavuvi dhidi ya uonevu na ufisadi.*
- *Itatunga sheria, sera na mipango madhubuti ya uzalishaji, uhifadhi, matumizi ya sekta ya uvuvi wa mwambao na wa bahari kuu.*
- *Itahakikisha kuwa inatumia sheria, hoja, midahalo, na ushirikishwaji wa jamii katika upatikanaji wa suluhisho la migogoro ya kimipaka na matumizi baina ya wavuvi kwa wavuvi na baina ya wavuvi na watalii wa baharini.*

- *Itatunga kupitia Baraza la Wawakilishi Sheria Mama itakayounda Mamlaka Maalum ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari (Zanzibar Marine Protected Area Authority) itakayotangaza na kusimamia kwa uhuru na bila ya kuingiliwa na taasisi yeyote maeneo maalum ya hifadhi ya bahari (Marine Protected Areas) na kuweka mipaka yake maalumu (zonation) mbali na maeneo yanayotumika kwa shughuli za kila siku za uvuvi na utalii.*
- *Italitangaza eneo la mwambao wa Kisiwa cha Latham Island kama ni eneo la hifadhi na kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kusimamia utaratibu wa udhibiti wa vyombo vinavyoingia ndani ya eneo hilo la mwambao.*
- *Itaangalia upya leseni zote zinazotolewa katika utalii wa bahari (Sportfishing) na hususan ule wa Kisiwa cha Latham Island pamoja na za mawakala wa utalii wasiokidhi sifa za uwakala (Tour Operators) kwa mujibu wa Sheria ya Utalii, na kuanza mchakato wa kisheria wa kuwawajibisha wote wale watakaonekana kujinufaisha wenyewe binafsi na maliasili za Kisiwa hicho.*
- *Itapitia upya mikataba ya makubaliano ya kuruhusu wageni wa nje kuingia moja kwa moja katika maeneo nyeti kama ya Mnemba, Latham island na Misali na kuangalia ikiwa kuna ukiukwaji wowote wa kisheria uliofanyika katika mikataba hii.*
- *Itawaongezea nguvu wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapatia fursa za mikopo, maboti ya kisasa na usalama, zana na mbinu za kisasa za kuvulia zisizo na athari za kimazingira na kuendeleza maeneo maalum kwa wavuvi wa kienyeji.*
- *Itaanzisha sensa mpya ya madiko na masoko ya wavuvi kwa ajili ya mipango ya usajili, utambuzi, uwezeshaji na ufikiwaji wa washiriki wa uvuvi.*
- *Itaanzisha sera bora za kuvutia wawekezaji katika miundombinu ya sekta ya uvuvi wa bahari kuu. Hii inajumuisha upunguzaji wa kodi (Tax Relief), Mafuta rahisi (Affordable Fuel Prices), Ufanisi bora wa bandari (Efficiency of the Port) na mahitaji yote yanayotakiwa katika usimamizi, ukarabati, uangalizi, na uendeshaji wa vyombo vinvyokwenda bahari kuu.*
- *Itaanzisha mashirikiano na washirika wa kimataifa katika kujenga bandari zaidi za kisasa za uvuvi, ambazo zitawapa wavuvi fursa ya kuhifadhi, kusindika na kuuza mazao yao ya bahari kuu na kuongeza ajira.*
- *Itakaribisha kampuni binafsi za uvuvi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu ili kutoa ajira zaidi kwa Wazanzibari na kusafirisha samaki nje ya nchi.*
- *Tutatumia uzoefu wa Seychelles kama mfano mmojawapo wa nchi za visiwa katika Bahari ya Hindi ambayo imeitumia vyema nafasi yake na kukuza uvuvi wa bahari kuu ambao unachangia kikamilifu pato la taifa la nchi hiyo.*
- *Itashirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kutafuta ufumbuzi wa ushirikishwaji wa kudumu wa Zanzibar katika masuala ya usimamizi eneo la EEZ lililo sambamba na Pwani za visiwa vya Unguja na Pemba.*
- *Itahakikisha kuwepo kwa utaratibu wa kudumu wa uwakilishi wa Zanzibar katika masuala ya Kamisheni ya Usimamizi na Uvuvi wa Samaki wa Aina ya Jodari katika Bahari ya Hindi (Indian Ocean Tuna Commission au IOTC) yenye makao yake makuu nchini Seychelles.*
- *Tutashirikiana na washiriki wote wa ndani na nje ya nchi pamoja na marafiki zetu wote wa Zanzibar kutusaidia katika kuongeza hali ya usalama ya wavuvi wetu kutokana na majanga ya kimaumbile na yale yanayosababishwa na binadamu.*
- *Kwa mashirikiano na washiriki wa maendeleo wa kikanda na kimataifa, tutaihuisha sera na mipango ya usimamizi shirikishi wa maliasili za Pwani na baharini (Integrated Coastal Zone Management).*

- *Itahakikisha kuwa inapambana na uvuvi haramu unofanywa kwa maslahi ya kisiasa.*

6.4. MAZAO YA BAHARI NA UFUGAJI SAMAKI

Zao la Mwani hapa Zanzibar limekuwa njia kuu mbadala ya kimaisha kwa asilimia 14% ya wakaazi wote wa mwambao wa Pwani ya visiwa hivi na hasa akina mama katika kujipatia riziki zao za kila siku. Kufikia mwaka 2010 kulikuwa na wakulima wa mwani wapatao 21,970. Mwaka 2012, Zanzibar ilisafirisha tani 14,400 za mwani zilizokuwa na thamani ya Shilingi Bilioni 5.7 (Dola za Makekani US$ Milioni 3.6). Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa kuwahakikishia zana, bei, na maslahi bora wakulima wa mwani. Serikali imeshindwa kufanya utafiti wa kulikuza zao la mwani na kulijengea viwanda vinavyotumia zao hilo ili kuleta tija zaidi kwa nchi na wananchi. Mazao mengine ya bahari kama ufugaji wa samaki wadogo, kaa, majongoo ya bahari na uvunaji wa wa chaza hayajawekewa mipango kazi thabiti ya kitaifa ya kuigeuza kuwa hazina ya kiuchumi kwa wanajamii.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itatayarisha mpango kazi wa utekelezaji wa uzalishaji wa mwani na mazao mengine ya bahari.*
- *Itashirikiana na washiriki mbali mbali wa kimaendeleo wa kikanda na kimataifa na nchi marafiki katika kuhuisha ufungaji wa samaki, kaa, chaza, n.k.*
- *Itawapatia wanawake wanaolima mwani misaada mbalimbali inayohitajika kwa kuendeleza ukulima wa mwani na kukuza vipato vyao.*
- *Itaisimamia Wizara inayohusika na Utalii kushajiisha hoteli za kitalii kutumia mwani wa Zanzibar kama njia ya kuwa na soko la ndani ili kuwaongezea tija wanawake wanaojishughulisha na ukulima wa mwani.*
- *Itaanzisha maabara ya mazao ya bahari na kufanya utafiti wa zao la mwani utakaopelekea kujenga viwanda vinavyosindika na kutumia zao hilo ili kuzidisha thamani ya zao hilo na kuleta tija zaidi kwa wakulima wa mwani.*
- *Itaandaa utaratibu unaofaa wa kuongeza thamani ya zao la mwani.*
- *Itashajiisha kilimo endelevu na kinachozingatia mazingira katika maeneo ya Maweni (Coral Rag Agriculture).*
- *Itaandaa utaratibu unaofaa wa kuongeza thamani ya zao la mwani na mazao mengine ya baharini.*
- *Itaanzisha na kushajiisha jamii kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki na kutumia fursa ya kisoko iliyopo kwenye sekta ya utalii ili kuongeza kipato cha wananchi.*

7. TUTAWEKEZA KATIKA KUIMARISHA HUDUMA ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

Mipango yoyote ya maendeleo endelevu ni lazima iwe na nguzo kuu nne: uchumi tengamano, jamii inayochangia na kufaidika na huduma mbali mbali za maisha, uhifadhi wa mazingira na usimamizi endelevu wa maliasili pamoja na nishati rahisi na mbadala. Ukuaji wa uchumi tu si kigezo pekee cha kuangalia maendeleo ya jamii. Maendeleo ya kweli yanakuja pale Serikali ya kweli ya wananchi inapotambua wajibu wake wa msingi katika kuhakikisha usawa wa jamii na haki (Social Justice and Equity) katika kupambana na janga la umaskini. Usawa wa jamii haupo kunako ujenzi wa miundombinu peke yake; lakini pia katika utungaji wa mipango na sera zinazojali hali za maisha ya watu, umaskini wao, kilio chao, mahitaji na vipaumbele wanavyovipigania katika kujiletea haki, usalama, na matumaini ya maisha yao. CUF inaamini kuwa mwananchi ana haki ya kuihoji Serikali yake na kuikosoa pale inapokwenda kinyume na matakwa, mahitaji, vipaumbele, haki na usawa katika maisha yake ya kila siku. Mwananchi ana haki ya kushirikishwa kikamilifu na kutoa maamuzi katika masuala mbali mbali kama vile haki ya umiliki ardhi, haki ya makaazi bora na ya kibinadamu, upatikanaji wa maji safi na nishati, elimu bora na ya uhakika, afya bora, na haki ya kupata fursa mbali mbali za kijamii ikiwemo haki ya kupatiwa ajira na mustakbali wa vizazi vyake.

7.1. MATUMIZI YA ARDHI

Zanzibar ni nchi yenye ardhi finyu inayohitaji kulindwa, kuendelezwa na kutumiwa kwa uangalifu mkubwa sana. Kuna mengi yanahitaji kufanywa juu ya kutumia ardhi, lakini kwa muda mrefu nchi imeshindwa kutekeleza sera na mikakati yoyote ile ya matumizi ya ardhi iliyoasisiwa kwa ajili ya matumizi bora na endelevu ya ardhi. Matokeo yake ni matumizi mabaya ya ardhi na migogoro isiyokwisha baina ya taasisi na wananchi, ndani ya jamii yenyewe na baina ya wananchi na wawekezaji. Mpaka sasa hakuna hata eneo maalum la kuwepo kwa ofisi za Serikali.

a) Mipango ya Ardhi na Amri za Wakubwa

Pamoja na kuwepo kwa mikakati kadhaa ya ujenzi na usimamizi wa mipango miji, bado utekelezaji wa mipango na mikakati hiyo haujaonekana kuzaa matunda yoyote. Miji yetu hususan ule waki historia wa Mji Mkongwe uliomo ndani ya Hifadhi ya UNESCO unaendelea kupoteza haiba yake ya kihistoria na kimazingira kutokana na ujenzi holela wa kushitukizia na usiofuata viwango vyoyote vinavyokubalika. Serikali inayoongozwa na CCM kwa muda mrefu imeshindwa kufuata na kusimamia ramani ya mipango yake wenyewe (Master Plan) ya Mji wa Zanzibar na miji mingine midogo midogo. Hakuonekani kuwepo mamlaka inayosimamia ipasavayo ugawaji na matumizi ya ardhi. Badala yake, ardhi imekuwa kama haina msimamizi anayefahamika. Mipaka ya kitaasisi inapuuzwa kwa makusudi na kila kiongozi wa Serikali anayejisikia kufanya maamuzi katika ugawaji na matumizi ya ardhi, iwe Wizara, Idara, Baraza la Manispaa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Halmashauri, Diwani au Sheha, huwa anafanya hivyo.

b) Haki ya Mwananchi na Ardhi

Haki ya umiliki wa ardhi imekuwa ni changamoto kubwa katika azma ya taifa hili kujikwamua kutoka katika umaskini. Migogoro inayosababishwa na maamuzi yaliyo juu ya kanuni na sheria za Ardhi hususan katika uwekezaji wa hoteli za kitalii umeleta suitafahamu kubwa ya kijamii na kisiasa miongoni mwa wananchi waathirika na kupelekea kuzorota kwa hali ya amani na usalama ndani ya maeneo hayo.

c) Ukiritimba wa kuwanyima wananchi haki yao ya malipo

Haki za asili za wakaazi zinapuuzwa. Wanavijiji huondolewa kunako maeneo yao ya kujipatia riziki kama mashamba, malisho ya mifugo au hata makaazi yao. Watawala bado hawataki kutambua haki ya kimataifa ya kibinadamu ya mwathirika kulipwa kwa mujibu wa thamani ya kweli ya ardhi, vipando na makaazi yake; na ushauri wa kuunda sheria maalum ya malipo (*Resettlement Action Plan*) imekuwa ukipingwa na kudharauliwa.

Kisingizio cha kuwa ardhi yote ni mali ya Serikali iliyo chini ya mikono ya Rais wa Nchi ndicho kinachowapa kiburi baadhi ya watawala wachache wakiwemo viongozi wa Serikali kukiuka taratibu, haki za binadamu na utawala wa sheria katika kuamua kiholela kuzigawa ardhi kwa kuzikandamiza haki za wakaazi na wenyeji katika matumizi ya ardhi.

CUF inaamini kuwa suluhisho pekee katika kuhakikisha uwiano wa jamii katika matumizi endelevu ya ardhi ni kulimaliza suala hili kwa utekelezaji kwa ukamilifu wa Sheria za Ardhi pamoja na kanuni zake mbali mbali zilizotungwa ambazo bado hazitekelezwi vilivyo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo:

- *Itauangalia upya muundo mzima wa usimamizi na matumizi ya ardhi pamoja na maingiliano ya mipaka ya madaraka ya taasisi husika.*
- *Itahakikisha kuundwa kwa sheria ya malipo ya wakaazi wanaoathirika kwa sababu ya miradi ya maendeleo (Resettlement Action Plan Act).*
- *Itapitisha bila ya ucheleweshaji mpango wa kugawa mipaka mipya ya manispaa mbali mbali za miji na maeneo ya Unguja na Pemba kama ilivyopendekezwa katika ramani mpya za mipango miji.*
- *Itazipitia upya sheria zote za taasisi nyingine zinazohusiana na usimamizi, uhifadhi na matumizi ya ardhi zinazoonekana kuingiliana na sheria mama ya ardhi.*
- *Itatunga sera bora ya mipango na matumizi ya ardhi ikibainisha ardhi ya makaazi, ofisi na taasisi za huduma za jamii, bandari, viwanja vya ndege, barabara, viwanda, hoteli za utalii, makaburi, kilimo, misitu na maeneo ya hifadhi, vyanzo vya maji, majaa, maeneo ya kale, viwanja vya michezo na wazi, n.k. na serikali itasimamia utekelezaji wake ipasavyo.*
- *Itaandaa mpango wa mazingira na hifadhi ya ardhi kuzuia mmong'onyoko wa ardhi na fukwe.*
- *Itabuni na kutekeleza mikakati madhubuti ya kudhibiti na kuhifadhi visiwa vidogo vidogo vya mwambao wa Unguja na Pemba visivyokaliwa na watu.*

7.2. NYUMBA NA MAKAAZI BORA

Kila mtu ana haki ya makaazi mema na moja ya malengo ya Mapinduzi yalikuwa ni kuwapatia Wazanzibari makaazi mema. Jitihada kadhaa zimefanyika kufikia malengo haya lakini bado kunahitajika juhudi kubwa zaidi ili kufikia kikamilifu azma ya kuwapatia Wazanzibari makaazi bora yanayoendana na mahitaji ya kisasa.

Mpaka sasa, hakujakuwa na mipango madhubuti na ya uhakika ya kuwasaidia watu kupata nyumba nzuri kwa gharama nafuu. Hakuna sera ya nyumba inayoeleweka. Serikali imeshindwa kugawa viwanja kwa maelfu ya wananchi walioomba. Badala yake kumekuwa na ukiritimba unaongozwa na baadhi ya viongozi wachache kukiuka taratibu za sheria na kanuni za makaazi kwa kuhodhi viwanja vingi kwa maslahi yao. Hili linawalazimisha wananchi kujitafutia kwa njia zao wenyewe maeneo ya kujistiri na matokeo yake ujenzi holela na usiozingatia viwango wala sheria umeenea nchi nzima na kusababisha maafa makubwa kama vile mafuriko wakati zinaponyesha mvua kubwa, maradhi ya mripuko unaotokana na kuzagaa kwa taka ngumu na maji machafu n.k. Utekelezaji wa Sheria ya *Condominium Act (2010)* kwa kutunga kanuni zake bado haujafanyika.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo:

- *Itahakikisha kuwa wananchi wanapata fursa ya kupatiwa viwanja vya majenzi vilivyopimwa na vinavyostahili bila ya vikwazo au ukiritimba wa wachache, rushwa na upendeleo katika utoaji wa viwanja hivyo.*
- *Itawafidia au kuwapatia nyumba wale wananchi waliobaki ambao nyumba zao zilibomolewa na Serikali kwa kutoa nafasi ya miradi ya serikali.*
- *Itaandaa mpango maalum wa kuhakikisha wananchi wanamiliki nyumba kwa kujenga nyumba za kisasa za bei nafuu kwa ajili ya kuwasaidia wale wenye kipato kidogo kwa njia ya kuwakopesha.*
- *Itahakikisha kuwa bei ya vifaa vya ujenzi ni nafuu ambazo wenye vipato vya chini wanazimudu kwa kuteremsha ushuru wa bidhaa na kodi kwa bidhaa hizo.*
- *Itahakikisha kuwa vifaa vya ujenzi vinavyoingizwa nchini vina ubora wa viwango vinavyokubalika.*
- *Itashajiisha wananchi, wafanyabiashara na makampuni kujenga nyumba za ghorofa kama mkakati wa kupunguza tatizo la nyumba za mawe katika maeneo ya mijini na mashamba na pia kuinusuru ardhi kwa ajili ya matumizi mengine na kwa manufaa ya vizazi vijavyo.*
- *Itafuatilia ujenzi unaofanywa na wakandarasi ili kulinda viwango.*
- *Itayatengeneza majumba yaliyo mikononi mwa serikali na kuwashajiisha watu binafsi kutengeneza majumba yao.*
- *Itaandaa mpango maalum wa kuzifanyia matengenezo nyumba zilizoko Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni eneo lililotangazwa na kutambuliwa na UNESCO kama Hifadhi ya Kimataifa na ni kivutio kikubwa cha watalii wanaotembelea Zanzibar.*
- *Italiangalia upya suala la fursa za mikopo nafuu ya ujenzi wa nyumba (mortgages).*
- *Itatekeleza uundwaji wa kanuni za Sheria ya Condominium Act ya Zanzibar katika kufikia azma ya mipango bora na makaazi endelevu katika Zanzibar Mpya.*

7.3. HUDUMA YA NISHATI KWA JAMII

Chanzo madhubuti na cha uhakika cha nishati ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Zanzibar imekuwa na tatizo kubwa la upungufu wa nishati (hasa mafuta na umeme) kila mara kwa muda mrefu. Kisiwa cha Unguja kwa mara ya kwanza kiliunganishwa na umeme wa nguvu za maji wa Kidatu mwaka 1979. Kwa miaka mingi Pemba ilibaki na mitambo chakavu ya umeme wa mafuta ya Wesha hadi mwaka 2010 wakati ambapo kwa mara ya kwanza kisiwa hiki hatimaye pia kikaunganishwa na umeme kutoka Tanzania Bara. Ni dhahiri kwamba kama si misaada ya washirika wa maendeleo na nchi wahisani kama Marekani, Norway na Japan, tungeshindwa kufikia azma yetu ya kupata umeme wa uhakika kwa Unguja na Pemba.

Lakini kwa miaka yote hii, pamoja na misaada ya wafadhili ya kukarabati mkonga wa umeme wa baharini wa Ras Kiromoni hadi Fumba, na ule wa Tanga hadi Pemba, hakukuwa na nia kutoka kwa Serikali hii inayoongozwa na CCM wala sera madhubuti ambayo ingeiwezesha Zanzibar kuwa na mitambo yake wenyewe mbadala ya uzalishaji ya umeme.

Majanga ya kukatika umeme ya mwaka 2008 na 2009/2010 yalianzisha kwa kiasi mdahalo wa kutafuta vyanzo mbadala vya nishati kwa Zanzibar. Lakini bado inaonekana kuwa Serikali inayoongozwa na CCM haijaonyesha shauku ya kutimiza ahadi zake kuhakikisha kuwepo kwa umeme wa usalama na uhakika endapo patatokea hitilafu kama ya miaka ya 2008 na 2009 tena. Pamoja na gharama za kununua majenereta ya kuzalisha umeme wa dharura kwa angalau asilimia 60 (megawati 25) ya mahitaji yote ya sasa ya kisiwa cha Unguja, kunaonekana kuwepo kwa juhudi za makusudi za kuyazima matumaini yoyote yale yanayopelekea kuiwezesha Zanzibar kuwa na mikakati mbadala ya huduma ya nishati ikiwemo uwezo wake wa kuzalisha umeme wa dharura.

a) Uhuru wa Nishati (Energy Independence)

CUF inaamini kuwa nishati ni uhai na usalama wa taifa na kwa hivyo kisingizio cha gharama kubwa za umeme kinachotolewa na Serikali inayoongozwa na CCM ni njama za makusudi za kuikwamisha Zanzibar kimaendeleo na kushindwa kupatikana kwa uhuru wa nishati (*Energy Independence*). Kuna haja ya kuipitia upya Sera ya Nishati ya Zanzibar na kujenga mipango ya muda mrefu ya kuirejeshea Zanzibar uwezo wake wa kuwa na mitambo ya umeme ya dharura kama katika visiwa vingine vya Bahari ya Hindi. Inastaajabisha kusona kuwa pamoja na jiografia ye visiwa vyetu na ukaribu wetu kwa Bara la Afrika, tungeweza kuwa na mpango kabambe wa kuwekeza katika utoshelezeshaji wa vyanzo vya nishati wakati tukijiandaa kwa muda mrefu kuiunda upya mitambo yetu ya dharura ya kuzalisha umeme.

b) Changamoto za madeni na miundombinu ya umeme.

Pamoja na umuhimu wa kipekee wa huduma ya umeme Zanzibar inayopata kutoka Tanzania Bara, hatuwezi kuendelea kuwa tegemezi kwa umeme kutoka Tanzania Bara kwa asilimia mia. Isitoshe, kukuwa kwa uchumi na mahitaji ya nishati kunatulazimisha kutafuta njia mbadala mapema zaidi. Utafiti uliofanywa na DFID unaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2050, Zanzibar itahitaji kiasi cha Megawati 250 za umeme kutoka kiwango cha Megawati 100 kwa sasa kupitia mikonga yake ya baharini. Gharama za kulipia umeme wa TANESCO ni kubwa mno. Pamoja na madeni ambayo shirika la ZECO Zanzibar linalodaiwa bado ZECO inalazimika kutumia gharama kubwa kila mwezi kulipia huduma ya umeme TANESCO au kutishiwa kukatiwa.

Baada ya kilio cha mda mrefu Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeanzisha Taasisi mpya ya Udhibiti ya Huduma ya Zanzibar (ZURA). Hata hivyo Taasisi hii inahitaji kuwezeshwa vyema ili kuweza kufanya majukumu yake kwa ufanisi kwa kuipatia nyenzo kama vile ofisi, rasilimali watu na vitendea kazi ili kuweza kuidhibiti biashara ya huduma za mafuta, umeme, maji na gesi za matumizi ya nyumbani ili kuleta ufanisi, usalama na kuondoa usumbufu wa upatikanaji na upandaji holela wa bei za bidhaa hizi. CUF itaweka kipaumbele kwa ZURA ili kuhakikisha inasimama wenyewe kwa mda mfupi na kuondoa kero kwa wananchi wetu.

c) Nishati ya Makaa na Kuni

Unyonge na umaskini wa wananchi wa Zanzibar bado umetukwamisha katika kutegemea kwa asilimia kubwa nishati ya kuni na makaa kama chanzo kikuu cha nishati. Utafiti wa karibuni umeonyesha kuwa matumizi ya kuni na makaa yamechukua zaidi ya asilimia 80% ya matumizi ya nishati mbali mbali nchini. Matokeo yake ni kusababisha kutoweka misitu ya mwambao kwa haraka. Utafiti wa UK-DFID wa mwaka 2012 unaonyesha kuwa kama hali haitorekebishwa basi visiwa vya Zanzibar havitoweza tena kujinasibu kama vina maeneo ya misitu inayotoa kuni za kutosheleza ifikapo mwaka 2030. Hali hii ni hatari kwa mazingira yetu na vizazi vyetu.

d) Nishati ya Gesi ya Kupikia

Matumizi ya Gesi ya aina ya LPG yamekuwa yakiongezeka kwa haraka tangu kuja kwa Mradi wa Hifadhi ya Misitu wa HIMA uliofadhiliwa na Serikali ya Norway. Lakini bado gharama za matumizi ya gesi hii zipo katika kiwango cha juu kabisa kufikiwa na mwananchi wa kawaida. Mtungi mmoja wa kawaida wa matumizi ya nyumbani unagharimu wastani wa Shilingi 55,000/-. Bila ya uwekezaji wa muda mrefu au ruzuku ya Serikali, nishati hii itaendelea kuwa ndoto kwa zaidi ya asilimia 75% ya wananchi wa Zanzibar.

e) Miundombinu ya bidhaa ya mafuta

Kwa upande wa nishati ya mafuta ya matumizi ya ndani kama vile vyombo vya moto na kadhalika, tumeona kuwa Zanzibar katika vipindi tofauti imekua ikikumbwa na tatizo kubwa aidha la uadimikaji wa bidhaa hizi au upandaji holela wa bei bila ya sababu yeyote ile ya msingi. Vile vile tunaona ongezeko la matumizi ya gesi ya kupikia (LPG), ambalo ni jambo la faraja kwa vile litasaidia sana kupunguza matumizi ya makaa na hatimae kupunguza ukataji wa miti. Hata hivo bidhaa hii inaonesha kutokudhibitiwa na kuonekana kuuzwa kiholela, jambo ambalo linaweza kuleta madhara makubwa pindipo pakitokea hitilafu katika mitungi hiyo ya gesi.

Pamoja na kuwepo kwa azma ya kutafuta maeneo zaidi (Oil Depots) ya uingizaji na uhifadhi wa mafuta ya petrol, diesel, mafuta ya taa, mafuta ya ndege, n.k, bado Zanzibar haina Sera madhubuti iliyo wazi wala mikakati inayotoa dira ya usimamizi na uendeshaji wa sekta hii. Kuja kwa chombo cha usimamizi wa biashara hii (ZURA) au ile ya viwango (ZBS) bado hakujajiibu suala la msingi la nani anayehusika katika kujenga miundombinu ya kitaifa ya kuingizia na kuhifadhi bidhaa ya mafuta haya.

Mitambo ya Mtoni inaonyesha kuchoka na kubanana sana. Pamoja na Serikali kutoa fursa ya wawekezaji kuelekea maeneo ya Mangapwani na Bumbwini, uamuzi huu haukutilia maanani hali halisi ya maeneo hayo kimaumbile, kijamii na kimazingira. Ukosefu wa miundombinu ya msingi ya kuvutia wawekezaji kunaturejesha katika hatari ya kuigeuza Mangapwani na Bumbwini kuwa Fumba ya pili. CUF inaamini kuwa suala la miundombinu ya bidhaa ya mafuta Zanzibar ni suala la msingi na ni suala la usalama wa nishati ya taifa (*Energy Security*) linalopaswa kupewa kipaumbele cha pekee.

f) Nishati Mbadala

Kwa muda mrefu Serikali inayoongozwa na CCM imekuwa ikilikalia bila ya kujali suala la utafutaji na uwekezaji katika nishati mbadala. Harakati nyingi za utafutaji na uwekezaji katika nishati hii umeishia katika rasimu za tathmini na hotuba katika Baraza la Wawakilishi. Pamoja na kuwa Zanzibar ilikuwa ya mwanzo katika kutilia mkazo masuala ya upatikanaji wa nishati mbadala, inasikitisha kuona kuwa sasa tumeshapitwa na Seychelles (Nishati ya Upepo) na Mauritius (Nishati ya Jua).

Pamoja na misaada mbali mbali ya washirika wa kimataifa kama Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Jamhuri ya Watu wa China, India, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, na wawekezaji mbali mbali wa ndani na nje kusaidia katika miundombinu ya barabara za manispaa, mawasiliano, na hata katika vijiji, bado inatia shaka kuona kuwa Serikali iliyopo ya CCM imejiridhisha – sio kwa jitihada zake – bali kwa juhudi zinazochukuliwa na mashirika na taasisi hizo na washiriki wengine wanaohangaika usiku na mchana kuwaletea wananchi kunako manispaa na shehia mbali mbali za visiwa hivi nishati ya jua.

CUF inaamini kuwa nishati mbadala ni dira inayoipa Zanzibar fursa ya kukabiliana na changamoto za nishati za leo na kesho.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itaipitia upya Sera ya Huduma ya Nishati ya Zanzibar pamoja na muundo wa usimamizi wa sekta zake pamoja na kupeleka muswada wa Sheria mpya ya nishati itakayoongoza uwekezaji, usimamizi, uzalishaji, utafiti, na uendeshaji wa sekta hii ya huduma ya nishati kwa jamii.*
- *Itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo na washiriki wa huduma ya nishati katika kuisaidia Zanzibar Kuzidi kujikwamua na kufikia uhuru wa nishati (Energy Independence) kwa kujenga na kuipanua miundombinu ya uzalishaji na usambazaji wa umeme.*
- *Itahakikisha kuwepo kwa muundo mpya wa sekta ya huduma ya nishati kwa jamii pamoja na kuangalia kwa kina njia mbali mbali za kukuza ufanisi wa uwajibikaji katika huduma hii kwa jamii kupitia mamlaka ya ZURA (Zanzibar Energy Utility and Regulatory Authority).*
- *Itaanzisha taasisi makhsusi cha uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme.*
- *Itaasisi chombo cha uwekezaji, utafiti na uzalishaji wa nishati mbadala. Chombo hichi pia kitafanya utafiti juu ya chanzo cha umeme mbadala ambacho kitakuwa endelevu na cha kutosha ikiwa ni pamoja na nguvu ya upepo, jua, mawimbi na vyanzo vyengine.*
- *Itaendelea kutafuta mbinu bora na mbadala za usambazaji wa umeme kwa gharama nafuu kwa mwananchi pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa cha uharibifu wa mazingira unaofanywa kwa kukata miti kwa ajili ya makaa na kuni za kupikia.*

- *Itatengeneza utaratibu wa kuondoa ushuru kwa miundombinu na vifaa vya uzalishaji wa umeme mbadala.*
- *Itaigeuza Zanzibar kuwa ni kituo cha kibiashara cha mafuta (Oil Investment Hub).*

7.4. UPATIKANAJI WA MAJI SAFI

Tatizo la upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama limeendelea kuathiri maeneo mengi ya visiwa vyetu. Wananchi wanalazimika kulipa Serikalini kupitia Mamlaka ya Maji ada za michango ya utoaji wa huduma ya maji lakini bado hawajaona tija ya michango hiyo wala huduma kuimarika.

a) Uvunaji mdogo wa maji ya mvua

Chanzo pekee cha upatikanaji wa maji safi Zanzibar ni maji ya ardhi (Groundwater). Tofauti na visiwa vingine vya ukanda huu, Zanzibar haina mito wala maziwa ya kuhifadhi maji ya juu. Tafiti mbali mbali zinaonyesha kuwa visiwa vya Zanzibar vinapoteza takriban asilimia 83% ya maji yote ya mvua ambayo huachiwa bila jitihada za kuyavuna, kutiririkia baharini.Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa sasa ina uwezo wa kuvuta kiasi cha wastani wa mita milioni 33 za ujazo kwa mwaka au sawa na asilimia 9% ya maji yote yanayoweza kufikiwa chini ya ardhi.

b) Uvutaji wa Maji Ardhi

Ni ukweli usiofichika kutokana na hali hii kuwa bado hatujaweza kuyavuna maji ya mvua kwa wingi ipasavyo, na kwamba bado hatujawa na miundombinu bora au teknolojia ya uhakika ya kuvuna na kuvuta maji ardhi ya kutosha tuliyo nayo kwa matumizi ya binadamu, kilimo, umwagiliaji, na maendeleo mengine.

c) Misaada, Sera Mbovu, na Ukosefu wa Haki ya Maji Safi na Salama

Pamoja na juhudi mbali mbali za washirika wa maendeleo wa kimataifa kama Finland, Umoja wa Ulaya, Japan, n.k. katika kuisadia Zanzibar kujikwamua kutokana na shida ya maji safi, bado suala la upatikanaji wa maji safi na ya uhakika kwa wananchi wengi wa visiwa hivi limekuwa ni jambo sugu lililokosa mpango kazi wa kweli wa kitaifa kulimaliza.

Serikali ya CCM imeshindwa kutumia fursa zilizopo za ndani na nje ya nchi kumaliza kabisa tatizo la upatikanaji wa maji safi na ya uhakika kutokana na sera zake mbovu na zilizopitwa na wakati za usimamizi endelevu wa sekta hii. Vipaumbele vya uwekezaji katika miundombinu vimewekwa kibiashara zaidi bila ya kujali uwiano wa jamii (Social Equity). Unyonge huu wa mwananchi wa Zanzibar hauwezi kuachwa kuendelea kama ulivyo na ni wajibu wa kila Mzanzibari kuhakikisha kuwa maji safi ni haki ya kila mtu.

d) Wawekezaji na Maji Safi kwa Wanavijiji

Wananchi wengi vijijini hususan katika kanda za Pwani za mashariki wamelazimika kuviacha visima vyao vinavyokabiliwa na tatizo la ukame na kuingia kwa maji ya chumvi na kutegemea maji yanayotolewa na wenye mahoteli. Shida kubwa hutokezea pale ambapo maji yanapofungwa au panapotokea suitafahamu kati ya wananchi na wenye mahoteli. Hakuna maji ya kutosha na vyanzo vya maji safi vilivyobaki kama visima na mapango ya maji hufungwa ili kuzuiwa watu kwenda kuchukua maji huko. Hali hii imezidi kuwatia unyonge wananchi wa vijijini na kujihisi kuwa hawana haki ya maji safi ndani ya nchi yao wenyewe.

e) Kamati za Maji na Uongozi Mbovu

Kamati za maji pia zinalalamikiwa kuwa hazitendi haki na hazifanyi kazi zake kwa njia za kidemokrasia. Siasa za kupendelea CCM zinaonekana kuongeza zaidi kamati hizi. Hakuna uwakilishi wa kweli kutoka kwa wananchi katika kutafuta ufumbuzi wa maji safi. Mamlaka ya ZAWA inalalamikiwa kutosikiliza vilio vya wananchi. Sheria au kanuni au sheria ndogo za huduma ya maji safi zipo katika kulinda maslahi ya wawekezaji zaidi kuliko kutafuta njia za kumaliza kabisa tatizo la ukosefu wa maji safi kwa jamii visiwani. Sekta ya maji safi Zanzibar inaonekana kuongozwa katika misingi ya faida na kusahau kabisa malengo ya Mapinduzi ya kuhakikisha kuwa maji safi ni haki ya kila Mzanzibari popote pale alipo, mjini na vijijini.

f) Ukosefu wa Maji Safi na Salama Mijini na Hatari ya Afya

Halikadhalika, mfumo wa usambazaji maji kutoka kwenye vyanzo vya maji umechakaa na kupelekea kiasi cha theluthi nzima ya maji yanayotoka kwenye vyanzo hivyo kupotea bure kutokana na tatizo la uvujaji ovyo wa mabomba. Ujenzi holela na uvujaji ovyo wa mabomba yanayosambaza maji safi mijini umepelekea kuathirika kwa sekta nzima ya maji katika maeneo hayo. Hatari ya maji safi kuchanganyika na maji machafu imekuwa ni jambo la kawaida kwa wakaazi wa maeneo mbali mbali ya mjini wakiwemo wale wanaoishi katika nyumba za maendeleo. Maradhi ya mripuko kama kipindupindu huja kwa sababu kuu moja nayo ni ukosefu wa maji safi na ya kutosha kwa matumizi ya binadamu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itatekeleza hatua zifuatazo:

- *Tutahakikisha tatizo la upatikanaji na usambazaji wa huduma ya maji safi na salama, Mjini na vijijini, Unguja na Pemba, linamalizwa katika kipindi cha miaka mitano na linakuwa historia.*
- *Itaupitia upya muundo wa usimamizi, usambazaji, ugawaji na utoaji wa huduma za maji safi ikiwemo mfumo mzima wa kitaasisi inayohusika na huduma za maji safi.*
- *Itapitia upya upya muundo, malengo na operesheni za kamati za maji na kuhakikisha kuwa kamati hizi zipo kwa kuwahudumia wananchi na si kwa kuwabughudhi au kuwachonganisha kisiasa.*
- *Itaanzisha mfumo wa usimamizi shirikishi wa maliasili ya maji (Integrated Water Resources Management) katika uongozaji wa sekta nzima ya maji safi ikiwemo uhifadhi wa vyanzo vya maji safi.*
- *Itahakikisha kuwa haki ya huduma ya maji safi kwa wananchi kama ilivyoahidiwa na wawekezaji wa mahoteli (Corporate Social Responsibility) haichezewi na kwamba wananchi wanapata maji yao safi kama kawaida na bila ya madhila na kufungiwa kiholela.*

- *Itashughulikia mara moja na kwa vitendo mpango kazi wa kitaifa wa ujenzi wa miundombinu ya uvutaji, uhifadhi, na usambazaji maji safi na salama kwa wananchi wote, mijini na vijijini.*
- *Itashajiisha uwekezaji katika miundombinu ya huduma za maji safi, ikiwemo kupitia mifumo ya kodi, ushuru, na gharama nyingine zinazokwamisha mipango ya taifa ya kufanikisha upatikanaji wa maji mijini na vijijini.*
- *Itaendelea kushirikiana na washirika wa kimaendeleo wa kimataifa katika kusaidia Zanzibar kufikia lengo lake la uhakika wa maji safi.*
- *Italinda vianzio vya maji na kuzuia ujenzi unaoathiri vianzio vya maji.*
- *Itaweka mfumo wa usambazaji maji katika maeneo mapya yanayokusudiwa kwa makaazi kabla ya viwanja kugawiwa.*
- *Itajenga matangi ya maji katika maeneo mengi yenye matatizo ya maji ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa maji ni wa uhakika.*
- *Itaunda mpango kazi wa kitaifa wa kushajiisha wananchi kutumia mbinu za kisasa na bora za kuvuna maji ya mvua (Rain Water Harvesting).*
- *Itajenga maabara ya kisasa kwa ajili ya uchunguzi wa maji Unguja na Pemba ili kuhakikisha usambazaji wa maji kwa wananchi ni safi na salama.*

7.5. USAFIRI WA NCHI KAVU

Zanzibar haina Sera yeyote makhsusi ya Usafiri wa Nchi Kavu. Pamoja na kwamba kipaumbele kikubwa katika sekta hii kipo katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, lakini mazingira ya kazi, ufanisi, na usimamizi kutoka taasisi husika zinazoshughulika na utoaji wa leseni, upasishaji, takwimu, na viwango hayaridhishi kabisa. Hii inatoa mwanya kwa vitendo vya ufisadi, rushwa, na upotevu wa umakini katika kusimamia uendeshaji wa Sekta hii muhimu kushamiri. Wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia kuzorota kwa huduma mbali mbali zinazohusiana na usajili na usimamizi wa vyombo vyao na kwa baadhi ya wakati kulazimishwa kutoa rushwa katika kupata baadhi ya huduma zao hizo kwa uharaka.

a) Usalama barabarani na uvunjifu wa haki za wasafiri

Suala zima la usalama barabarani bado limedharauliwa. Usafiri wa wananchi hasa wa mjini umeendelea kuwa wa gari za abiria zisizo na viwango wala njia za uhakika za kuhakikisha usalama wa abiria. Mahusiano baina ya waendesha vyombo vya usafiri wa nchi kavu na maaskari wa usalama wa barabarani pia hayaridhishi. Kuja kwa askari jamii na kuanza kujishughulisha na kazi zisizowahusu za usalama barabarani kama kuwasimamisha na kuwaadhibu wananchi kunachangia kwa kuzorota kwa haki za kibinadamu za wasafiri na waendesha vyombo vya nchi kavu.

b) Usimamizi mbovu, mizozo, na maamuzi yasiyo tija

Hali ya vituo vya daladala na magari mengine ya usafiri hairidhishi. Hakuna maeneo ya kutosha ya kuegesha vyombo na mizozo baina ya wenye vyombo na wafanyakazi wa mansipaa imezidi kukua. Wananchi wamekuwa wakiteseka kwa kuburuzwa na sheria na kanuni za manispaa zisizo mwelekeo wala suluhisho katika kutafuta muafaka wa usafiri barabarani. Kuhamishwa kiholela kwa vituo vya daladala bila ya mpango wowote kunahatarisha usalama na afya ya jamii.

c) Mfumuko wa vyombo barabarani, afya na mazingira

Pia mfumuko wa idadi ya vyombo vya usafiri barabarani kumeleta msongamano wa magari na vyombo vingine katika barabara. Hali hii imepelekea kuwepo kwa uvunjaji wa sheria barabarani, ajali, na hata kupelekea kutishia usalama wa waendesha baiskeli na wapita njia. Hali ya mazingira pia imezorota (Air Pollution). Moshi wa vyombo hivi na vumbi la barabarani limechangia sana katika kupanda kwa kesi mbali mbali za maradhi yanayosababishwa na uvutaji wa hewa chafu (Respiratory diseases).

d) Ujenzi na utanuzi wa barabara

Mtandao mzuri wa barabara ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii na kwa kujenga uchumi wa kisasa. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Amani Karume imefanya kazi kubwa ya ujenzi wa barabara kwenda katika maeneo mengi ya visiwa vya Unguja na Pemba. Changamoto ya Serikali ijayo ni kuziendeleza na kuzitunza barabara hizo na kuziwekea huduma muhimu na za kisasa. Bado kuna baadhi ya barabara ambazo ujenzi wake haujazingatia viwango vinavyohitajika. Hakujakuwa na mipango ya ujenzi wa madaraja katika barabara kuu na tumebaki kutegemea madaraja yaliyojengwa karibu karne nzima iliyopita.

e) Ujenzi wa Barabara na Athari za Kijamii na Kimazingira

Wananchi wengi wanaoathiriwa na miradi ya barabara wamekuwa wakilalamika kuwa hawapatiwi haki zao wanazostahiki za fidia kwa mashamba, nyumba au vipando vyao. Hii imeleta suitafahamu kubwa baina ya Serikali na wananchi. Yote haya yamekuwa yakisababishwa na ukosefu wa uangalizi madhubuti katika kuhakikisha kuwa masuala yote ya kijamii na kimazingira yanatiliwa mkazo. Uchimbaji kiholela wa mashimo ya vifusi na mchanga pia yameleta migogoro ya kitaasisi na kijamii na kuleta hasara kubwa kwa uchumi na mazingira.

f) Ajali Barabarani

Idadi ya ajali kubwa na za kutisha Zanzibar zimeongezeka. Hakuna jitihada zozote endelevu na zenye mafanikio zinazowekezwa katika kuzuia wimbi la ajali barabarani. Sababu ni nyingi ikiwemo kukosekana kwa mikakati bora ya elimu ya usalama barabarani pamoja na usimamizi wa hali ya nidhamu na usalama barabarani. Hali ya uagizaji wa vyombo ya usafiri barabarani visivyo na sifa kabisa imezidi kuwa mbaya. Hakuna viwango vya udhibiti wa ubora wa vyombo hivyo. Hakuna sera na mipango kabambe ya usimamizi na uendeshaji wa sekta ya usafiri wa barabara. Hakuna maeneo yaliyowekwa kwa wanaokwenda kwa miguu au baiskeli. Vitendo vya matumizi ya ulevi kwa waendesha vyombo vimeongezeka. Janga hili linapaswa kudhibitiwa au tutaendelea kupoteza wananchi wetu katika ajali hizi.

g) Usafiri wa Umma (Public Transport System)

Nchi yeyote yenye kujali utoaji bora wa huduma za usafiri wa nchi kavu basi ni lazima iwe na sera na mikakati bora ya kurahisisha usafiri wa raia wake ambao ndiyo nguvu kazi ya maendeleo ya nchi hiyo. Kukosekana kwa huduma ya usafiri wa umma kunaleta maswali mengi. Hivyo ubinafsishaji una tija gani ikiwa Serikali inayakimbia majukumu yake ya msingi kuhusu utoaji wa huduma ya jamii? Kama hiki si kipaumbele muhimu katika kurahisisha hali ya usafiri wa wananchi ikiwemo kuunganisha mitaa ya miji, viunga, na mashamba ya visiwa hivi basi ni nani mwenye dhamana ya usimamizi wa mfumo mzima wa utoaji huduma ya usafiri Zanzibar?

CUF inaendelea kuthamini jitihada za sekta binafsi na hususan waendesha daladala katika kuziba pengo hili la utoaji wa huduma za usafiri mijini na mashamba. Hata hivyo wakati umefika kwa Serikali kuongeza huduma hizi kwa kuanzisha usafiri wa umma hasa katika miji ya Zanzibar utakaoshindana moja kwa moja kibiashara na katika utoaji wa huduma rahisi, salama na haraka ya usafiri kwa wananchi hasa wale wanaosafiri baina ya mijini na mashamba.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo katika suala la usafiri wa nchi kavu:

- *Itaanzisha sera mpya ya usafiri wa nchi kavu na mpango kazi wa taifa wa usimamizi na uendeshaji wa sekta hii kwa Zanzibar.*
- *Itadhibiti uvunjaji wa haki za binadamu barabarani na kuwawajibisha kisheria wote watakaopatikana na makosa kama hayo.*
- *Itaupitia upya muundo mzima wa usimamizi, utoaji leseni, na uongozaji barabarani na kukabiliana na mazingira yoyote ya rushwa au ufisadi wa aina yoyote utakaoonekana.*

- *Itashirikiana na washiriki wa kimaendeleo wa ndani na nje katika kutafuta uwekezaji katika barabara kuu na za mitaa, maegesho, vituo vya daladala, njia za kupitia waenda kwa miguu, n.k.*
- *Italipa umuhimu mkubwa suala la kukamilisha ujenzi wa barabara kuu na za ndani mjini na mashamba ambazo bado ujenzi wake haujakamilika na kuzipanua kulingana na ukuaji wa watu na wingi wa magari.*
- *Itaweka mkakati maalum wa kupunguza msongamanao na kuzitunza barabara zilizojengwa na kuziwekea vifaa na huduma zote za kisasa zikiwemo alama na taa za barabarani.*
- *Itatoa upendeleo maalum katika ujenzi wa barabara kwa kampuni za ndani zenye uwezo wa kufanya kazi na zenye vifaa vya kisasa na wafanyakazi wenye sifa.*
- *Itasimamia usafirishaji wa barabarani kuhakikisha usalama wa maisha ya watumiaji, heshima na usalama wa abiria na mizigo yao.*
- *Itaimarisha usalama barabarani, kwa kuweka alama kila panapostahiki na kuzitilia nguvu sheria za barabarani, hasa zile zinazohusika na uzito wa mizigo na mwendo.*
- *Itasisitiza usafi wa mji na barabara zake na kutengeneza maeneo wazi (buffer zones) ili kuondoa kero kwa wananchi na wenye vyombo.*
- *Itahakikisha kuwa mfumo wa tathmini na malipo kwa waathirika wa miradi ya ujenzi wa barabara unatekelezwa (Resettlement Action Plan).*
- *Itadhibiti uendeshaji ovyo barabarani unaosababisha ajali na majeraha mengi kwa wananchi.*

7.6. USAFIRI WA BAHARINI

Kuongezeka kwa kasi ya huduma na viwango vya usafiri wa baharini hususan baina ya Zanzibar na mwambao wa Afrika ya Mashariki kunatoa ishara njema ya ukuaji wa kiuchumi na maendeleo ya jamii na katika kukidhi mahitaji ya kila siku ya wananchi. Lakini wakati kasi hii inaonekana sana katika usafiri wa vyombo baina ya Unguja na Dar es Salaam, bado usafiri wa ndani baina ya Unguja, Pemba, Tumbatu, Kojani, Fundo, Kokota, Uvinje, Kisiwa Panza, na hata baina ya bandari ndogo za mwambao wa Unguja na Pemba hautoshelezi. Na hapajakuwa na jitihada zozote kutoka upande wa Serikali inayoongozwa na CCM ya kuhakikisha uungwanishaji wa usafiri wa uhakika na salama wa visiwa vyetu vidogo. Hii inatokana na Sera mbovu zinazoridhia kuendelea kuwatenganisha wakaazi, badala ya kuwaunganisha katika kutafuta rizki, maisha na mustakbali wao.

a) Ukiritimba wa kisiasa unaofanywa na watawala

Utashi wa kisiasa unaofanywa na watawala katika kulazimisha kufanya maamuzi mabovu yanayokidhi maslahi yao binafsi na hususan katika masuala ya usafiri wa baharini kwa wananchi wa visiwa vidogo vidogo kama Tumbatu na katika mwambao wa visiwa vyetu hauwezi kuzima kiu ya kweli ya haki ya maendeleo ya mwananchi. Haki ya ushirikishwaji wa wananchi katika kufanya maamuzi ya kweli ya kuleta maendeleo ya miundombinu ya usafiri wa baharini ni haki ya binadamu. Haki hii inastahiki kutiiwa na kuheshimiwa. CUF itahakikisha kuwa maamuzi yoyote yale yasiyoendana na haki ya mwananchi ya ushirikishwaji katika kufanya maamuzi ya kuleta maendeleo ya kweli na badala yake maamuzi hayo kutumika kuleta kiburi, ufisadi, uonevu, na mgawanyiko wa kisiasa ndani ya jamii, hayapewi nafasi yoyote katika Serikali ya kweli ya wananchi wote.

b) Usalama wa wananchi na abiria

Usalama wa wananchi na abiria katika usafiri wa baharini umekuwa ukizorota siku hadi siku. Majanga mawili ya kitaifa yaliyotusibu ndani ya kipindi cha mwaka mmoja (*MV Spice Islander*:2011 na *MV Skagit:2012*) yanadhihirisha wazi jinsi mamlaka husika za usafiri wa baharini zilivyoshindwa kusimamia usalama wa maisha ya abiria na kuhakikisha usimamizi wa kweli wa viwango vya huduma pamoja na viwango vya vyombo vyenyewe.

Maafa yaliyowakuta wananchi wasio na hatia – wake kwa waume, watoto na wazee, yanahitaji majibu ya kweli na ya haki. Familia zilizopoteza ndugu na wazee wao, marafiki na jamaa, bado wanasubiri haki kwao na hukumu za kisheria kwa wahusika wa ajali hizo. Ukurasa mpya utaweza kufunguliwa pale ukweli na haki utakaposimama.

c) Uchumi, Maendeleo na mahitaji ya kuwa na bandari zaidi

Kama katika nchi nyingine yeyote ile ya kisiwa, Bandari ni kitovu cha maisha na maendeleo ya Mzanzibari. Ni mlango unaounganisha Zanzibar na ulimwengu wote na ni urithi wa utambulisho, utaifa na umoja wetu pamoja na kuwa chanzo cha uchumi na maendeleo yetu kwa ujumla. Hichi ni kipaumbele kisichoepukika cha kuujenga upya uchumi wetu na kuleta maendeleo ya haraka kwa jamii yetu. Bila ya kuwepo kwa bandari za kisasa na zenye miundombinu na huduma za uhakika katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, basi usimamizi na ufanisi wa sekta nzima ya usafiri wa baharini, pamoja na uagizaji, uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa, utaathirika.

Ni dhahiri kwamba uwezo wa hivi sasa wa Bandari zetu haukidhi mahitaji yaliyopo hivi sasa ya huduma za usafirishaji, kupakia, kupakua, kuhifadhi mizigo na shehena nyingine mbali mbali za kiuchumi na hususan katika kuitayarisha Zanzibar na uchumi ujao wa mafuta na gesi. Hatua za makusudi na za haraka za dharura zinahitajika kuujenga upya mfumo mzima wa huduma za usafirishaji wa baharini na miundombinu ya bandari zote Unguja na Pemba na kufikia kiwango cha ufanisi wa kimataifa, na unaozingatia ubora, ukuwaji, uwekezaji, na usalama wa sekta nzima.

d) Gharama kwa mwananchi wa kawaida

Gharama za kupakia na kusafirisha mizigo ni kubwa mno kiasi kwamba baadhi ya wenye meli wanafikiria kusita kutumia bandari hiyo na hao wanaotumia hupandisha bei za huduma zao kutokana na ufanisi mdogo wa bandari zetu. Pamoja na hatua iliyochukuliwa ya kutenga eneo la matumizi ya boti za abiria, bado kuna meli zinazotumia eneo moja kwa ajili ya abiria na mizigo na kusababisha msongamano unaoweza kuepukika. Hii inaweza kusababisha ajali na kuleta hasara kubwa.

e) Zanzibar na Shirika la Kimataifa la Baharini (IMO)

Mengi yanaendelea kuzungumzwa kuhusiana na mahusiano ya Zanzibar na Shirika la Kimataifa Bahari (International Maritime Organization au IMO). Lengo kuu la Shirika la IMO ni kuendeleza na kuusimamia kwa makini mfumo kisheria wa kimataifa unaoendesha sekta zote husika za usafiri baharini katika nyanja mbali mbali ikiwemo usajili wa meli wa kimataifa (*International Registry*), huduma za bendera (*Flag State*), usalama kazini, uhifadhi wa mazingira, sheria za usafiri, biashara na uchumi zinazotumika baharini, mashirikiano ya kiufundi, usalama dhidi ya uharamia wa baharini (piracy) na ufanisi wa sekta nzima ya usafiri baharini. Shirika la IMO linaongozwa na mikataba na itifaki mbali mbali za kiusalama, kiufundi, kimazingira, kiuendeshaji, n.k.

Nafasi ya Zanzibar katika IMO ni muhimu sana kwani bahari ni urithi na uti wa mgongo wa utambulizi wetu kama nchi ya Kisiwa. Hata hivyo ushirikishwaji wetu, uwazi katika maamuzi ya ndani na nje kuhusiana na mikataba ya IMO na Zanzibar pamoja na faida ambayo Zanzibar imekuwa ikiipata kutokana na huduma zinazofungamana na IMO bado imekuwa ni kitendawili kikubwa cha kisiasa katika kufikia azma ya mafanikio yetu ya maendeleo ya bahari.

f) Utambulisho wa Zanzibar katika IMO

Umuhimu mkubwa wa shirika hili kwa Zanzibar ndiyo moja ya misingi ya ilani yetu inayohusiana na haki za nchi katika Muungano. Inachoshangaza ni kuwa pamoja na Zanzibar kushiriki katika sekta nyingi za utendaji wa Shirika la IMO, hatutambuliwi hata katika kiwango cha "*Associate Member*". Wakati Hong Kong, Macau na Taiwan zinatambulika rasmi kama Associate Members wa IMO. Bado Zanzibar - pamoja na kuwa na sifa kemkem zinazotambulika ikiwemo katika ushiriki wake kikamilifu wa kazi mbali mbali za shirika la IMO kusajili meli za kimataifa (Flag State) – haijapata utambulisho wake inayostahiki.

g) Shirika la Usafiri Baharini Zanzibar na Uwazi wa dhamana zake.

Kukosekana kwa utaratibu unaoeleweka wa kimataifa kama huo kumesababisha migogoro kuhusiana na dhamana na uendeshaji wa shughuli za Shirika la Usafiri wa Baharini Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*) ndani na nje ya nchi. Kwa mfano hakuna uwazi wa uendeshaji wa shughuli za ZMA. Masuala ya usimamizi wa mapato ya Zanzibar katika masuala ya "*International Registry*" kama ni *Flag State* hayana utaratibu wowote ule ulio wazi na unaoweza kuhojiwa ndani ya nchi.

h) Upendeleo katika Ajira na Ukiukwaji wa Sheria za Kimataifa

Tuhuma za ufisadi na upendeleo katika ajira na fursa kwa kazi za ubaharia zimeshamiri na baya zaidi ni pale Zanzibar inapotuhumiwa kwa ushahidi na kuhusishwa katika uvunjaji wa sheria za kimataifa kunakofanywa na meli zilizosajiliwa chini ya himaya ya bendera yake kama kuvunjwa sheria za vikwazo, usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya na binadamu, na katika magendo ya mimea na wanyama pori. Masuala kama haya ndiyo yanayoitia doa sifa ya Zanzibar katika ulimwengu wa kimataifa. CUF inadhamiria kuumaliza ukiritimba huu wa uendeshaji chini kwa chini kwa dhamana za "*Flag State*" na kutafuta suluhisho la kudumu litakaloipa Zanzibar nafasi na wajibu wake katika IMO, na kurejesha hadhi yake ya ufanisi na uendeshaji wa dhamana zake kwa kutii utawala wa kisheria wa kimataifa.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itauboresha muundo mzima wa usimamizi na uendeshaji wa sekta ya usafiri wa baharini.*
- *Itatathmini hali halisi ya mashirika mengine husika yaliyopo, ufanisi wao, maingiliano ya kitaasisi, na gharama za uendeshaji.*
- *Itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo wa kimataifa katika kuisaidia Zanzibar kukarabati bandari zake zilizopo hivi sasa pamoja na kuharakisha ujenzi wa bandari mpya kuu zikiwemo za Mpiga Duri, Ras Mkumbuu, Mangapwani, Wete na Mkoani.*
- *Itatengeneza sera na mipango kazi ya kitaifa ya kutafuta uwekezaji katika miundombinu ya bandari za ndani za visiwa vya Zanzibar pamoja na bandari maalum zitakazotumika kwa ajili ya kutoa huduma za miundombinu ya sekta ya mafuta na gesi baharini.*
- *Itaendelea kushirikiana na washiriki mbali wa ndani na nje ya nchi katika kuongeza miundombinu, ufanisi wa huduma kwa abiria na usafiri wa baharini wa ndani na ule wa baina ya visiwa vya Zanzibar na nchi za jirani.*
- *Itazipitia programu zote za miradi ya maendeleo zilizopo hivi sasa zinazohusiana na usafiri wa baharini na kuhakikisha kuwa programu hizi hazivunji haki za binadamu, au kusababisha migawanyiko ya kijamii, au kutowashirikisha wananchi katika maamuzi ya mustakbali wao.*
- *Itaupitia upya muundo wa usajili, usimamizi, na upekuzi wa vyombo vinavyobeba abiria na kuhakikisha usalama wa maisha na viwango katika utoaji wa huduma ya usafiri wa baharini.*
- *Itaitangaza Zanzibar kuwa bandari huru ili kuchechemua maendeleo ya kiuchumi na kuirejeshea Zanzibar nafasi yake kama kituo kikuu cha kibiashara katika eneo la Afrika Mashariki na Kati.*
- *Itaweka vifaa vya kisasa vya kuongoza meli katika bandari zote na kuzipa huduma muhimu, kama vyoo, maji, umeme na sehemu za kupumzikia abiria.*
- *Itaendelea kushirikiana na washiriki wa sekta ya mafuta na gesi baharini katika kufanya uchunguzi wa ujenzi wa bandari mpya za kisasa zitakazohudumia sekta hiyo.*
- *Itainua sekta ya ukaguzi rasmi wa meli za abiria Zanzibar kabla ya kupewa vibali vya uendeshaji.*
- *Itahakikisha kuwa Zanzibar inaanzisha kikosi maalum cha kitaifa (Search and Rescue Unit) kitakachokuwa na uwezo wa kuingia katika harakati za uokozi baharini katika kipindi cha muda mfupi na zana za uhakika za uokozi.*

- *Itaanzisha Chuo cha Ubaharia ili kukidhi haja ya taaluma ya vijana wetu wa Zanzibar.*
- *Itazisimamia na kuhakikisha kuwa fursa za ajira kwa Wazanzibari wawili wawili kwa kila meli iliosajiliwa na bendera ya Zanzibar (Tanzania) zinatumika vilivyo kwa uwazi na pasina na vitendo vya upendeleo, rushwa au uhodhi wa nafasi hizo kwa maslahi binafsi.*
- *Itashikirikana na IMO kuhakikisha utekelezaji wa sheria za kimataifa kuhusiana na meli zilizosajiliwa kwa jina la Zanzibar.*
- *Itaalika makampuni zaidi ya meli za kimataifa kuja Zanzibar kusajili meli zao na kuongeza ajira kwa vijana.*
- *Itaipitia sheria ya ZMA na kuendeleza kanuni mbali mbali zinazokidhi utekelezaji wa mikataba na itifaki za Shirika la IMO.*
- *Itaangalia uwezekano wa kushirikiana na sekta binafsi katika usimamizi wa shughuli za huduma za bandari.*
- *Itapitia upya mikataba yote iliyofungwa kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kampuni za nje zilizopewa uwakala wa kusajili meli kimataifa na zile zitakazobainika kwenda kinyume na mikataba zitafutiwa mikataba hiyo.*

7.7. USAFIRI WA ANGA

Kwa kuzingatia nafasi ya Zanzibar kama mlango wa kuingilia na kutokea baina ya Bahari ya Hindi na eneo la Afrika Mashariki na Kati na kama kiungo kati ya eneo hilo na maeneo muhimu ya kiuchumi ulimwenguni kama vile Mashariki ya Kati, Bara Hindi na Mashariki ya Mbali, kunahitajika Uwanja wa Ndege wa kisasa na wenye huduma zote muhimu. Matengenezo makubwa ya barabara ya kurukia na kutulia ndege (runway) yametoa nafasi kwa mashirika ya kimataifa kufikiria tena kurejesha usafiri wa moja kwa moja kati ya Zanzibar na miji mikuu ya nchi husika.

a) Hali za Viwanja

Lakini bado jengo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar ambao sasa umepewa jina la "*Abeid Karume International Airport*" ni la kiwango duni sana na huduma zake haziko katika viwango vya kimataifa. Jengo jipya linalojengwa tayari limeshaingia katika ngazi mbali mbali za changamoto zinazoendelea kuitia hasara kubwa Serikali hata kupitia mkataba wa kupata mkopo nafuu kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Uwanja wa Ndege wa Karume ulioko Chake Chake, Pemba haujatumika kikamilifu katika kukiunganisha kisiwa cha Pemba na miji mingine ya Tanzania na Afrika Mashariki na huduma zake ni za kiwango cha chini.

b) Kupotea kwa Fursa adimu za uwekezaji

Pamoja na kuwepo kwa fursa za uwekezaji wa viwanja vya ndani vya kurushia ndege ndogo ndogo, bado Serikali kupitia wahusika wao wa kitaasisi wamekuwa wakishindwa kuzitumia fursa hizi kwa sababu mbali mbali za maslahi yao binafsi. Miradi kadhaa kama hiyo imekwama kwa sababu zisizoeleweka licha ya kuwepo kwa sifa za msingi zinazokidhi miradi hiyo.

c) Maingiliano, Maamuzi na Athari Zake

Maingiliano ya kitaasisi katika usafiri wa anga ndani ya Zanzibar na baina ya Zanzibar na Tanzania Bara pia umekwamisha juhudi mbali mbali za kupanua wigo wa ufanisi wa huduma za usafiri wa anga katika visiwa vya Zanzibar. Mashirika mengi ya kimataifa ya ndege yanashindwa kuharakisha kuleta huduma zao za usafiri wa moja kwa moja kutoka makao makuu yao hadi Zanzibar kwa sababu ya kushindwa kwa wenye mamlaka kuyatetea maslahi ya kiuchumi na na maendeleo ya nchi hii. Hii inapelekea usumbufu mkubwa kwa wasafiri wanaotaka kuja Zanzibar na wale wa Zanzibar wanaotaka kwenda nje kwa shughuli mbali mbali zikiwemo za kiuchumi.

d) Usalama na Viwango

Tunaona jinsi huduma za usalama katika viwanja vya ndege bado zilivyo duni. Ubovu wa mitambo ya upekuzi, ufanisi na utoaji huduma wa kiwango kisichoridhisha, ufahamu

mdogo wa wahusika na watendaji wa viwanja vya ndege, kuingiliwa kisiasa, upendeleo katika ajira, bughudha za mara kwa mara wanazozipata abiria kutokana na miundombinu duni, tatizo la uingiaji wa madawa ya kulevya, vituo duni vya upekuzi wa afya na mazao, n.k yanatosha kulazimisha utawala uliopo kukubali kuwa sekta ya usafiri wa anga Zanzibar haipo katika viwango vya kimataifa na hivyo kunahitajka "*Post-Moterm*" ya haraka kuunusuru uchumi wa Zanzibar siku za mbele.

e) Usafiri wa Anga na Muungano

Kuna taasisi nyingi za kidola zinaingiliana katika masuala ya usimamizi na udhibiti wa usafiri wa anga Zanzibar. Suala hili linaulizwa kila siku pale panapoteka migongano ya maamuzi na amri za kitaasisi. Wawekekzaji mara nyingi wamekuwa wakilalamika kuwa wanabanwa sana katika suala la ujenzi wa viwanja vidogo na huduma za wagonjwa wanaohitaji usafiri wa haraka wa anga. Haya ni mojawapo ya masuala ambayo yanahitaji suluhisho la haraka na pia katika mambo yanayoitwa kama "kero" za Muungano.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo katika suala la usafiri wa anga:

- *Itaanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar (Zanzibar Airways) kwa njia ya ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.*
- *Itafanya mazungumzo na mashirika ya kimataifa ya usafiri wa anga kuanzisha usafiri wa moja kwa moja kati ya miji mikuu yao na Zanzibar ili kuchechemua maendeleo ya kiuchumi na kibishara na kukuza maingiliano ya watu katika ukanda huu wa Afrika na ulimwengu wa kimataifa.*
- *Itahakikisha kwa muda mfupi inakamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege (Abeid Karume International Airport) uliopo Unguja na kuufanyia marekebisho makubwa uwanja wa ndege uliopo Chake Chake Pemba ili viwanja vyote viwili viwe na kiwango cha kimataifa.*
- *Itaviimarisha viwanja vya ndege na kuviendesha kibiashara kwa misingi ya mashirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi (Public – Private Partnership).*
- *Itaongeza urefu na upana wa njia ya kurukia ndege kwa Uwanja wa Ndege wa Karume ulioko Pemba na kupanua majengo ya uwanja kufikia viwango vya kimataifa.*
- *Itaimarisha huduma za wasafiri pamoja na usalama wa viwanja vya ndege.*
- *Itahakikisha miundombinu bora na wahudumu waliofikia viwango katika nyanja za uhudumu wa vyombo na abiria, usalama wa afya, mazao na bioanuwai katika viwanja vya ndege.*
- *Itahakikisha mahitaji yote ya usalama wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege yanawekwa na kuendelezwa.*
- *Itaondoa ufisadi na upendeleo wa ajira kwa wahudumu na watendaji wa viwanja vya ndege.*
- *Itaharakisha mashirikiano zaidi na mashirika makubwa ya kimataifa ya ndege kuja moja kwa moja Zanzibar.*
- *Itashirikiana na washiriki wa nchi za visiwa vya ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi kama Comoros, Seychelles, Madagascar, Mauritius na Reunion katika kuanzisha mahusiano ya karibu ya usafiri wa anga baina ya visiwa hivi.*
- *Itahakikisha mafanikio ya fursa za uwekezaji wa viwanja vya ndege vidogo Unguja na Pemba ili kupanua wigo wa sekta ya ndani ya usafiri wa anga hususan katika kukuza utalii wa anga katika mwambao wa Zanzibar (Microlight Aviation Tourism).*
- *Itafanya uchunguzi wa mara kwa mara wa ndege zinazobeba abiria na mizigo kuepusha ajali, na kuzuia Zanzibar kuwa eneo la kusajili ndege zilizochoka.*
- *Itaunda kwa mashirikiano na mashirika ya ndege ya kimataifa idara maalum za matengenezo mbali mbali (line maintenance) na vituo vya kutia mafuta kwa ndege za masafa ya mbali zinazopitia ukanda huu yaani "Transit Refuelling Hub'.*

8. TUTAISIMAMIA NA KUIENDESHA KWA UWAZI SEKTA YA MAFUTA NA GESI

Historia ya mafuta na gesi ya nchi yetu inatoka mbali. Kwa zaidi ya miaka sitini visiwa vya Zanzibar vimekuwa vikiyatafuta mafuta katika himaya yake ya ardhini na baharini bila ya mafanikio. Lakini katika miaka ya karibuni na kufuatia kukua kwa fani mbali mbali za teknolojia za utafutaji mafuta na gesi, matumaini ya kupatikana kwa mafuta na gesi ndani na katika mwambao wa Zanzibar yameongeza kasi ya hamasa na mwamko kwa wananchi ya kuelekea katika mapinduzi mapya ya kimaendeleo yatakayowatoa kutoka katika dimbwi la umaskini na kuinyanyua Zanzibar kiuchumi na kimaendeleo. Ni dhahiri kwamba siku zote CUF imekuwa ikipigania uhuru wa usimamizi na uendeshaji wa sekta ya mafuta na gesi kwa Zanzibar. Serikali ya Awamu ya Sita ilisimama kidete katika kutafuta muundo mpya wa usimamizi, uendeshaji na mapato ndani ya Muungano na Tamko la Baraza la Wawakilishi la mwaka 2009 lilikuwa ndio mwanzo wa safari ya kuelekea kunako uhuru huo wa usimamizi wa mafuta na gesi yetu wenyewe. Pamoja na kwamba kumekuwa na jitihada mbali mbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Saba katika kuasisi muundo na usimamizi wa sekta ya mafuta na gesi hapa Zanzibar, jitihada hizo zimekuwa zikizimwa au kukwamishwa kwa utashi wa kisiasa na woga wa viongozi wa CCM walio madarakani wa kufanya maamuzi ya Zanzibar Kwanza. Inaonekana wazi kuwa Serikali inayoongozwa na CCM haina nia safi ya kuipa Zanzibar haki yake ya usimamizi na uendeshaji wa Sekta hii na iko tayari hata kulidharau Azimio la Baraza la Wawakilishi kwa maslahi yao wanayoyajua. Sheria zilizotungwa na kupitishwa kinyemela katika Bunge la Jamhuri ya Muungano karibuni zimekusudiwa kuimaliza Zanzibar na azma yake ya kusimamia na kuendesha Sekta yake ya Mafuta na Gesi.

8.1. AZIMIO LA BARAZA LA WAWAKILISHI (2009)

CUF inalichukulia Azimio la Baraza la Wawakilishi la Mwaka 2009 kama ni mwanzo wa dira ya kuelekea kunako uhuru na usimamizi wa sekta ya mafuta na gesi kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Hii ni dira iliyobeba matumaini ya Wazanzibari na katika kukidhi kiu yao ya kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yao. Ni chachu ya umoja na mashirikiano ya jamii waliowakilishwa na waliowachagua katika ngome ya wananchi wa Zanzibar ambayo ni Baraza la Wawakilishi. Ni dira ya kishujaa na iliyojaa matumaini mapya kwa Wazanzibari. Lakini leo tunashuhudia viongozi wa Serikali ya CCM wakiendelea na usaliti wao kwa wananchi wa Zanzibar kwa kulidharau na kulitupilia mbali Azimio hili la ngome ya wananchi wa Zanzibar na kuendeleza na njama zao za kuwahadaa wananchi wa Zanzibar wanaodai haki zao za dhati katika usimamizi na uendeshaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi na kuzidi kuzizamisha fursa na matumaini ya wananchi wa Zanzibar kwa kuyapeleka mafuta na gesi kunako himaya ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

CUF haiwezi kamwe kuukubali usaliti huu unaofanywa na viongozi wa Serikali ya CCM na italisimamia kidete Azimio la Baraza la Wawakilishi la kudai haki ya wananchi Zanzibar katika usimamizi na uendeshaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi yaliyopo Zanzibar. CUF haitazitambua Sheria zilizopitishwa kinyemela na kimabavu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na itapinga uonevu huo na kuhakikisha kuwa mafuta na gesi ya Zanzibar na mapato yake yanabaki kuwa haki na mali ya Wazanzibari.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itahakikisha kuwa Rasimu ya Sera ya Utafutaji, Uchimbaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi inapelekwa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Azimio la 2009.*
- *Itatunga Sheria mpya kwa ajili ya Zanzibar ya Utafutaji, Uchimbaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi na kupelekwa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Azimio la 2009.*
- *Itahakikisha mikataba yoyote itakayotiwa saini kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar basi ipelekwe Baraza la Wawakilishi kwa mujibu taratibu zilizopo ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji.*

8.2. MAFUTA NA GESI KWA MAENDELEO YA KWELI

Hadi sasa Serikali inayoongozwa na CCM haijawa na maamuzi ya msingi kuiwezesha Zanzibar kuanza shughuli zake za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Hili ni jambo la kusikitisha sana kuwa makampuni makubwa duniani kama vile Shell International, RAK Gas, Statoil na nyenginezo, zimekua zikija Zanzibar na kutumia muda wake mwingi kuwashawishi watawala kuanza shughuli za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

Hata hivyo, wakati ikiona ndugu zetu wa Tanzania Bara wanaendelea kwa kasi kubwa na zoezi la ugunduzi na utumiaji wa Gesi kwa shuhuli za kijamii kama vile kuzalisha umeme, watawala wa CCM bado wanaogopa kuwapatia wananchi wanyonge wa Zanzibar manufaa yatokanayo na Mafuta na Gesi Asilia kwa kisingizio cha kuwa Mafuta na Gesi Asilia bado ni jambo la Muungano. Je tujiulize Muungano huu ni wa upande mmoja tu?

CUF inatambua kuwa usimamizi na uendeshaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi pamoja na mapato yake yanahitaji muundo na mfumo ulio wazi, wa kidemokrasia, wenye usawa katika fursa na maslahi, na wenye baraka na imani za wananchi wenye matarajio kemkem.

CUF inaamini kuwa mfumo bora wa usimamizi ni ule wenye mkakati shirikishi na tengamano ulionyooka kiutawala na kisheria pamoja na taasisi zinazokidhi sifa za usimamizi na uendeshaji wenyewe; wenye watu walio na uwezo na ushujaa wa kufanya maamuzi sahihi na ambao ni waadilifu na wanaoaminika; wenye umma ulio na ufahamu na uelewa; wenye uwazi katika utoaji leseni na uzalishaji wa mafuta na gesi pamoja na mfumo unaoaminika wa ukusanyaji wa kodi na mapato.

Ushirikishwaji kwa ukamilifu wa wananchi katika kufanya maamuzi yanayohusu maeneo na mazingira yao; haki zao za umiliki na usawa katika fursa ni nguzo muhimu ya Sekta ya Mafuta na Gesi inayohudumia wananchi. Halikadhalika, ushirikishwaji na uendelezwaji wa taasisi mbali mbali husika za kisekta katika kushughulikia masuala ya mafuta na gesi ni nguzo nyingine muhimu sana katika kufikia usawa wa kimaendeleo katika sekta zote.

Uwekezaji wa muda mrefu wa mapato na faida za sekta ya mafuta na gesi itakuwa ni moja kati ya vipaumbele muhimu vya mikakati ya Serikali inayongozwa na CUF. Na hili litahusisha udhibiti holela wa matumizi ya fedha zitokanazo na mafuta na gesi.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itahakikisha kuwa Sekta ya Utafutaji, Uchimbaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi inaendeshwa katika misingi ya maendeleo endelevu yenye kujali uwiano wa kijamii katika fursa za kiuchumi, uwekezaji, maendeleo pamoja na uhifadhi wa mazingira.*
- *Itasimamia mabadiliko ya kimipango, kitaasisi, kisheria, na kiutekelezaji ili kupisha uchumi bora na shirikishi uliotengamana na mafuta na gesi.*
- *Itahakikisha mageuzi katika mahusiano ya kijamii, elimu, uelewa, uwezeshwaji na uwazi katika ngazi zote za uwekezaji wa mafuta na gesi.*

8.3. VIPAUMBELE VYA SEKTA WAZI NA IMARA

Katika kuhakikisha haki, fursa, usawa na maendelelo, CUF inaamini kuwa vipaumbele vifuatavyo ni muhimu sana katika kufanikisha muundo wa mfumo ulio wazi na endelevu wa sekta ya mafuta na gesi Zanzibar: Uundwaji wa mamlaka ya mafuta na gesi husika ya Zanzibar; utayarishwaji wa muundo ulio wazi wa kitaasisi, usimamizi, na uendeshaji wa maendeleo ya mafuta na gesi; na uwezo wa Zanzibar katika kuingia katika mazungumzo na makampuni ya mafuta na gesi ya kimataifa ikiwemo utaratibu madhubuti wa utoaji wa leseni na mikataba ya uchimbaji.

Pia suala la ugawaji na usimamizi wa mipaka ya bahari kwa vitalu vya Zanzibar; uwezo wa Zanzibar kuingia katika safu za kimataifa kutafuta uwekezaji katika mafuta na gesi nchini; masuala ya afya, usalama na mazingira; usimamizi wa masuala ya tathmini za athari za kijamii na kimazingira ikiwemo ushirkikishwaji wa jamii katika masuala ya sekta ya mafuta na gesi; uunganishwaji wa sekta ya mafuta na gesi na sekta nyingine za kiuchumi; na uongozi thabiti katika kusimamia kodi na mapato. Lakini pia uwezo wa kuwapatia fursa na ajira Wazanzibari katika masuala ya mafuta na gesi.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaanzisha Mamlaka huru ya usimamizi wa mafuta na gesi Zanzibar itakayowakilishwa na wataalamu wa fani mbali mbali waliobobea katika fani kama za ugawaji wa vitalu, utoaji leseni na mikataba, Uhandisi na usimamizi wa utafuta na uchimbaji, mazingira na usalama, uwekezaji, kodi na mapato, n.k.*
- *Itahakikisha katika ngazi ya maamuzi ya utekelezaji wa mipango ya sekta ya mafuta na gesi Zanzibar basi wananchi wanashirikishwa kikamilifu.*
- *Itasimamia azma ya kuwepo kwa mipaka ya baharini katika usimamizi na udhibiti wa kazi za vitalu vya mafuta na gesi.*
- *Itauanzisha muundo mpya wa ukusanyaji wa kodi na usimamizi wa mapato ya mafuta na gesi.*

8.4. UTOAJI WA LESENI NA MIKATABA

CUF inaamini umuhimu wa kuihakikishia Zanzibar mapato na faida katika kila eneo la uzalishaji wa mafuta na gesi. Kuna njia mbili kuu ambazo CUF inaziona ni muafaka katika kufikia uhakika wa mapato na faida za uzalishaji. Kuna mfumo wa *Production Sharing Agreement (PSA)* na ule wa *Concession*. Kila mfumo una faida zake na changamoto zake. CUF itafanya maamuzi sahihi na busara kulingana na mahitaji ya wananchi wake na inaona kwa sasa kuwa mfumo wa *Production Sharing Agreement* (PSA) una faida kubwa ya kuwashirikisha kwa upana wananchi na jamii kupata fursa katika sekta hii.

Pamoja na yote, CUF inaamini kuwa maamuzi ya kuamua mikataba ipi itakayofungwa yanahitaji kupita Baraza la Wawakilishi na itaheshimu matakwa ya wananchi kwa mujibu wa Azimio la Baraza la Mwaka 2009. Uwazi wa mikataba na leseni zake utakuwa ni nguzo ya Serikali inayoongozwa na CUF katika kuhakikisha kuwa hakuna ufisadi wa aina yoyote utakaoruhusiwa kunako Sekta hii.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itatengeneza mfumo maalum na unaofaa kwa Zanzibar katika kuhakikisha mikataba bora na yenye kutoa haki na uwiano baina ya mwekezaji na wananchi wa Zanzibar.*
- *Itapendekeza mfumo wa Production Sharing Agreements (PSA) katika muundo wa utekelezaji wa mikataba na leseni.*
- *Italishirikisha Baraza la Wawakilishi katika ngazi zote za utengenezwaji wa mikataba baina ya mwekezaji na wananchi wa Zanzibar.*

8.5.UTAYARISHAJI WA MIUNDOMBINU MUHIMU

Kwa kuwa Sekta ya Mafuta na Gesi ni sekta mpya Zanzibar, nchi yetu inahitaji mpango kazi wa uhakika utakaosaidia kupatikana kwa haraka miundombinu mbali mbali ya sekta ya mafuta na gesi. Miundombinu hio ni pamoja na ujenzi wa bandari maalum, mabomba ya mafuta, marigi ya uchimbaji mafuta na gesi, upatikanaji wa ardhi inayotosha kwa uwekezaji wa sekta hii; barabara, umeme, maji, TEKNOHAMA, usafiri baharini, mawasiliano, mabenki, viwanda na huduma za jamii.

CUF inaamini kuwa yote haya yanataka mpango maalum wa taifa wa uwekezaji na bila ya kuwepo kwa mpango mpya wa maendeleo wa nchi, basi jitihada hizi zitakwama. CUF ipo tayari kupitia mpango mzima wa taifa wa maendeleo kwa ajili ya kujiandaa na mapinduzi ya maendeleo haya ya sekta ya mafuta na gesi.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itatengeneza mpango makhsusi wa maendeleo utakaohusisha sekta zote nyingine za kiuchumi na huduma za jamii lakini pia utakaokaribisha vivutio (incentives) vya kuwaalika wawekezaji katika kujenga miundombinu mbali mbali ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na ile ya utoaji huduma mbali mbali kama barabara, umeme, maji, TEKNOHAMA, usafiri baharini, mawasiliano, mabenki, viwanda na huduma za jamii*

8.6. KODI NA USIMAMIZI WA MAPATO

Vile vile tutambue wazi kuwa ili nchi iweze kupata manufaa yatokanayo na rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia ni lazima iweze kupanga, kukusanya na kuwa na uwezo kamili wa kufanya matumizi yatokano na mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi Asilia ikiwemo kodi (*Corporate Income Tax*).

Sote ni mashahidi kua katika katiba ya sasa ya Muungano na ile katiba pendekezwa ya Bunge la Katiba chini ya shindikizo la Chama cha Mapinduzi na Serikali zake mbili, zimeliweka jambo la kodi ya Income Tax kuwa ni jambo la Muungano kinyume na matakwa ya katiba iliyopendezwa na wananchi. Hii ni kusema kuwa kama Zanzibar itachimba rasilimali hizi za Mafuta na Gesi Asilia basi haitakua na uwezo wa kudhibiti kodi ya aina hii, jambo ambalo itafuta ile dhana na madhumuni ya Zanzibar ya kuwa na mamlaka kamili katika mambo ya mafuta na gesi asilia.

CUF itahakikisha kwa nguvu zote kuwa mapato ya Serikali yanayotokana na Sekta ya Mafuta na Gesi hayafikiwi na ufisadi wa aina yeyote. Na hili litafanikiwa pale ambapo mapato yote yatakapowekwa katika mfuko maalum uitwao *Sovereign Wealth Fund*. Mfuko huu utahakikisha kuwa fedha za mafuta na gesi zinazopatikana kama "*Royalties*" au "*Income tax*" au vyanzo vinginevyo haziingizwi kunako mifuko ya kawaida ya Serikali na kutumiwa kiholela au kwa ufisadi.

Serikali ianyoongozwa na CCM imeshindwa kabisa kulifanyia kazi suala la kuondoa kodi ya mapato (*Income Tax*) ya mafuta na gesi kutoka kunako mambo ya Muungano. Kushindwa huku kunaihatarisha azma ya Zanzibar ya kufikia uhuru wake wa usimamizi, uendeshaji na mapato katika sekta ya mafuta na gesi. CUF itahakikisha kuwa kodi ya mapato inarudi kwa Wazanzibari.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaanzisha Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mapato na Kodi za Mafuta na Gesi kwa Zanzibar.*
- *Itaanzisha Sheria ya Mfuko wa Sovereign Wealth Fund kwa ajili ya kuhakikisha uhifadhi na usalama wa mapato ya mafuta na gesi.*
- *Itatafuta muafaka na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kuhakikisha haki kamili za kodi na mapato kwa mafuta na gesi kwa Zanzibar.*

8.7. FURSA KWA WANANCHI (*LOCAL CONTENT*)

CUF inaamini kuwa kodi ya mapato peke yake haitoshi kuwa ndio chachu ya maendeleo kwa wananchi. Kuwepo kwa fursa mbali mbali za ajira ndani ya Sekta hii kutaleta mapinduzi makubwa ya kimaendeleo kwa jamii na

kubadili hali za maisha za watu. Serikali inayoongozwa na CCM haioni umuhimu wowote wa kuwatengenezea Wazanzibari fursa za ajira, huduma na ubunifu ndani ya Sekta hii. CUF itatengeneza Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi (*Local Content Development Policy*) itakayotoa fursa kwa wananchi kujiunga moja kwa moja kwenye ajira ya sekta kuu yenyewe ya mafuta na gesi, katika biashara ndogo ndogo, utoaji wa huduma, ununuzi wa bidhaa za ndani, teknolojia, elimu, mafunzo na uelewa katika fani mbali mbali za sekta ya mafuta na gesi, ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaanzisha Sera na Sheria ya Uwezeshaji wa Wananchi (Local Content Development Policy) kuhusiana na mafuta na gesi.*
- *Itahakikisha kuwa wananchi wanapata fursa za kushiriki kwa ukamilifu katika ngazi zote za sekta ya mafuta na gesi.*

8.8. MASHIRIKIANO YA KIMATAIFA

Zanzibar inapaswa kuwa na mfumo madhubuti utakayoiwezesha kuyajenga mahusiano yake ya kibishara na kitafiti na washiriki wa kimataifa katika sekta ya mafuta na gesi. Mpaka sasa, Serikali iliyoko madarakani ya CCM imeshidwa kulitambua suala hilo na kulilazimisha liwe la kisiasa na hivyo kupelekea kuinyima Zanzibar fursa zaidi za kutafuta wawekezaji wake. CUF inaliona hili kama mfano wa jitihada mbali mbali za kuidhoofisha Zanzibar kufikia malengo yake haya ya uhuru wa usimamizi na uendeshaji wa sekta yake ya mafuta na gesi.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itajenga mahusiano ya kibiashara na kitafiti na washiriki mbali mbali wa kimataifa katika sekta ya mafuta na gesi na kuvutia wawekezaji wa sekta hii kuja Zanzibar hususan wale walioonesha hamu na shauku ya muda mrefu.*

8.9. MIPAKA YA BAHARINI

Mambo ya msingi ambayo yanahitajika ili kuweza kuanza shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika nchi ni pamoja na kujua mipaka ya nchi yako, kuwa na Sera na Sheria ya kutafuta na kuchimba mafuta. Watawala wa CCM wanoongoza Zanzibar mpaka sasa hawana hata jambo moja waliloweza kulikamilisha katika haya, hivyo ni kusema wazi maneno ya mdomoni na vitabuni ya kuambiwa tuko tayari kuweza kutafuta na kuchimba Mafuta na Gesi Asilia hayana mantiki yeyote.

Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa kuja na sera, mkakati au mpango wowote wa kuviondoa vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi katika mwambao wa Zanzibar na Bahari Kuu. Hakuna jitihada yoyote iliyofanywa ya kuanzisha mazungumzo yoyote yale ya maana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kuiachia Zanzibar vitalu vyake vya Bahari Kuu na vile katika mwambao wa magharibi wa visiwa vya Unguja na Pemba, ikiwemo Kisiwa cha Latham Island. Kila siku idadi ya vitalu ambavyo Zanzibar ilikuwa ivisimamie imekuwa ikipungua kwa kuchukuliwa au kupewa wawekezaji waliopitia Shirika la Uendelezaji Mafuta Tanzania (Tanzanian Petroleum Development Corporation).

Unyonge huu unaopandikizwa na Serikali ya CCM umeleta suitafahamu kubwa baina ya washiriki wa Sekta ya Mafuta na Gesi wanaotarajia kuanza kazi zao Zanzibar na Serikali inayoongozwa na CCM. Kunaonekana kushindwa kabisa kwa watawala katika kutekeleza ahadi zao walizotoa kwa wananchi. CUF inasema kuwa suala la mipaka ya baharini ni kitovu cha uhai wa sekta nzima ya mafuta na gesi Zanzibar na kwamba haki hiyo ni haki ya wananchi wa Zanzibar.

Serikali inayoongozwa na CUF itafanya yafuatao:

- *Itatafuta muafaka wa haki wa kuipatia Zanzibar vitalu vyake vya mafuta na gesi nchini.*
- *Itasimamia mamlaka kamili ya uendeshaji wa vitalu vyote vilivyo upande wa Zanzibar bila ya kunyimwa haki hiyo.*

9. TUTALINDA NA KUHIFADHI MAZINGIRA KWA UCHUMI ENDELEVU

Uchumi na Maendeleo Endelevu wa nchi hayawezekani bila ya dira iliyo bora yenye kuendana na uhifadhi wa mazingira na bioanuwai yake. Utajiri wa nchi ya Kisiwa kama yetu siku zote hufungamana na maliasili tulizo nazo katika ardhi na bahari. Bila ya uvunaji na matumizi endelevu ya maliasili hizo, tutajikuta katika majanga makubwa ya uharibifu wa mazingira na upotevu kiholela wa maliasili zetu. Zanzibar, kama nchi ya kisiwa, ina kila sababu ya kuyaweka mazingira katika msingi wa dira yake ya maendeleo. Katika miaka ya karibuni tumeshuhudia mipango ya maendeleo ya taifa ikitekelezwa bila ya umakini unaostahiki wa utunzaji wa mazingira na bioanuwai. Kama kuna jitihada inayofanywa ya kuyahifadhi na kuyalinda mazingira, basi hufanywa kwa shingo upande na bila ya nguvu ya kisheria au nidhamu yoyote. Matokeo yake ni uchafuzi wa mazingira yetu tunayoishi kwa kumwaga taka ovyo kila pahali, kumwagwa maji machafu katika mitaa, fukwe na misitu yetu, kuharibiwa kwa ardhi, vyanzo vya maji, misitu na fukwe zetu, kukatwa miti ovyo, kutumia vibaya maji ardhi, kuharibu haiba ya makaazi yetu wenyewe, na kuruhusu uchimbaji kiholela wa michanga, mawe na vifusi, popote pale panapotolewa vibali. Huku ni kujiangamiza kimazingira, kijamii na kimaendeleo. Wakati umefika kwa Serikali makini kuchukua hatua za dharura kuviokoa visiwa vyetu kutokana na janga hili la harakati za mwanadamu, hasa pale tunapokabiliwa na janga kuu jipya la mabadiliko ya tabia nchi linalosababisha mabadiliko ya miongo, uhaba wa mvua, kuzidi kwa joto, ukame, mmomonyoko wa fukwe na kupanda kwa kina cha bahari katika mwambao wetu. Serikali inayoongozwa na CUF itayaweka mazingira kama kitovu cha dira ya maendeleo yetu.

9.1. UCHAFUZI WA MAZINGIRA

Ni jambo lisilopingika kuwa mazingira na afya jamii ni chanda na pete. Lakini unapotenganisha ukweli huu na kuziweka taasisi hizi mbili katika hali ya mtengano, unakaribisha majanga tuliyo nayo hivi sasa katika miji na mitaa yetu, misitu na fukwe zetu. Utupaji ovyo wa taka umeshamiri, maji machafu yanamwagwa popote pale panapofaa bila ya kujali afya za watu na mazingira yenyewe. Majaa yaliyo kando na mitaa na makaazi yetu yaliyoruhusiwa bila ya utaratibu wowote ule yanachomwa moto bila ya hadhari yeyote. Bidhaa chakavu za kila aina imekuwa ndio mtindo leo ndani ya jamii yetu. Msongamano wa magari barabarani, vumbi na hali nzima ya afya ya jamii ikidorora.

Serikali inayoongozwa na CCM hailioni janga hili na badala yake huwekeza fedha na rasilmali kwa kutumia utashi wa kisiasa na kukandamiza haki za wananchi inaowaona kuwa si wenzao. Sheria mama zilizotungwa za tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazina dira yoyote ya mipango ya uhifadhi mbali na kuzidi kuwatoza kodi wananchi na wawekezaji. Hili haliwezi kukubalika kuendelea na CUF inaamini kuwa muundo mzima wa usimamizi wa mazingira, ardhi, na tawala za mikoa unahitaji kupitiwa upya ili kuyaokoa mazingira yetu kwa maslahi ya vizazi vyetu vinavyokuja.

Serikali inayoongozwa na CUF itafanya yafuatao:

- *Itawekeza katika huduma za usafi wa mazingira kutoka katika ngazi ya Shehia, Halmashauri hadi Manispaa.*
- *Itasimamisha mara moja utolewaji kiholela wa vibali vya kufanya majaa bila ya utafiti au tathmini maalum ya maeneo hayo.*
- *Itasimamia utowaji zaidi na wa kiufanisi wa elimu ya uhifadhi wa mazingira na afya ya jamii kwa wananchi kwa kutumia njia mbali mbali za mawasiliano.*

9.2. UHARIBIFU WA ARDHI NA MAPORI

Taasisi inayoshughulika na usimamizi wa ardhi ina Idara zisizopungua tatu lakini cha kushangaza ni kuwa uharibifu wa ardhi unaendelea kila kukicha bila ya kudhibitiwa. Pamoja na kuwa tumepiga hatua kubwa katika kutengeneza ramani bora za mipango miji, bado mipango hiyo inabaki kuwa ndani ya nyaraka tu na utekelezaji wake haupo kabisa. Ujenzi holela ndani ya mapori, vyanzo vya maji na mabonde ya kilimo unaendelea bila ya udhibiti wowote. Sheria zilizopo za mazingira na matumizi ya ardhi zinavunjwa au kupuuzwa na kwa niaba ya baadhi wa watu wachache katika ngazi ya utendaji na uongozi. Misitu inavamiwa bila ya mpangilio kwa kukidhi maslahi ya wachache.

a) Uchimbaji Holela wa Vifusi

Uchimbaji holela wa mchanga, vifusi na mawe umeshamiri mno. Tathmini inaonyesha kuwa zaidi ya hekta mia nne (400) za ardhi katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba zimechimbwa kwa shughuli za kuvuna mchanga, vifusi au mawe. Inatisha kuona kuwa hata wenye mashamba ya eka tatu yaliotolewa wakati wa Mapinduzi sasa wanayageuza kuwa mashimo ya vifusi na kupata leseni kutoka kwa taasisi inayohusika na uhifadhi wa misitu. Matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa mazingira ambao ungeweza kuzuilika kama Serikali ingedhibiti vitendo hivi kwa kuwa na maeneo maalum ya uchimbaji wa mchanga, vifusi na mawe na kukataza kwa nguvu zote za kisheria ardhi za eka tatu kugeuzwa mashimo ya uchimbaji. inaamini kuwa njia pekee ya kumaliza migogoro hii ya kimazingira ni kuufumua upya muundo mzima unaousimamia misitu na uchimbaji vifusi kwa ajili ya kuyaokoa mazingira yetu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itahakikisha kuwa malengo ya ramani ya mipango miji yanatekelezwa ipasavyo ili kuokoa mazingira.*
- *Itaupitia muundo uliopo sasa wa usimamizi wa kisheria wa uchimbaji wa vifusi, mchanga na mawe na kuunda taasisi mpya husika itakayoshighulikia masuala hayo.*
- *Itatangaza mikakati mpya ilio sambamba na ramani ya mipango miji na vijiji na kudhibiti uchimbaji holela wa mchanga, vifusi na mawe na badala yake kuweko maeneo maalum kwa mujibu wa sheria mpya ya uchimbaji.*

9.3. HIFADHI ZA MISITU

Zanzibar imebarikiwa na hifadhi kuu za misitu mbili za Jozani na Ngezi. Lakini pia kuna hifadhi nyingine ndogo ndogo za misitu zilizotengwa kwa ajili ya urithi wa bioanuwai na mazingira yetu. Lakini leo hifadhi hizi nyingi zimeshavamiwa kwa makaazi, miradi ya maendeleo, uchimbaji wa vifusi na mawe, lakini na hata pia kuwekwa majaa ya kutupia taka. Ukatwaji wa Mikoko umeshamiri na hii inaongeza tishio la kumezwa zaidi kwa fukwe za mwambao wetu.

Maamuzi ya kutangaza au kuondoa hifadhi za kimazingira yanafanywa kiholela bila ya mpangilio wa tahthmini zozote za kimazingira na kijamii. Maamuzi ya mustakbali wa mazingira ya nchi yetu unakuwapo mikononi mwa wachache wanaoamua hatma ya ardhi, misitu, hifadhi na uchimbaji bila ya ushirikishwaji wa kutosha na wa kweli wa jamii kwa ukamilifu. Matokeo yake ni kupotea kwa hifadhi zetu na bioanuwai zake na kuzidisha athari za kimazingira.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itahakikisha mipaka yote ya hifadhi za msitu za aina yote inalindwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria na ramani za mipango miji na vijiji pamoja na kudhibiti vibali vyovyote vile vinavyotolewa kiholela vya kukata miti ovyo mijini na mashambani.*
- *Itaendelea kutoa huduma mbali mbali za kusaidia uhifadhi na uendeshaji wa shughuli zinazohusiana na misitu ya jamii katika kuendeleza malengo ya kupambana na upoteaji wa msitu.*
- *Itasaidia katika uwekezaji zaidi wa shughuli zinazohusiana na mavuno ya maliasili ndogo ndogo za misitu (Minor*

Forest Products au Mazao yasiyohusiana na mbao) kama ufungaji nyuki, uvunaji wa mimea na mizizi ya tiba asilia, mazao yanayotoa viungo (spices, dyes, additives), na mimea inayotoa mazao ya chakula.

- *Itaiboresha zaidi taasisi ya hifadhi na usimamizi wa misitu katika fani mbali mbali za uongozi, utendaji, vitendea kazi, taaluma, na maslahi bora kwa wote.*
- *Itatengeneza mkakati mpya wa kitaifa wa kuhifadhi misitu ya Mikoko na maeneo ya mapori ya maweni.*
- *Itaunda mikakati maalum ya kusimamia uhifadhi wa wanyamapori wa ardhini, ndege na wanyamapori wanaohama hama (Migratory Species)*

9.4. HIFADHI ZA BAHARINI

Usimamizi wa hifadhi za baharini (*Marine Conservation Areas*) bado haujawa wenye kuleta mafanikio ya kweli kwa wananchi na watalii wanaolipa kodi kuja kuzitembelea hifadhi hizi. Pia, baadhi ya wakati, kumekuwa na uvunjwaji wa taratibu za kimamlaka baina ya wasimamizi wa hifadhi za baharini na watendaji wakuu wa Serikali.

a) Hitilafu za Usimamizi

Mfumo ulio hivi sasa wa kuyaacha madaraka ya sekta nzima ya uhifadhi wa bahari mikononi mwa wachache katika ngazi ya Idara ni janga linalofukuta la kuzidisha migogoro baina ya washiriki mbali mbali wanaotumia maliasili za baharini. Malalamiko yamekuwa mengi, haki za wananchi na wavuvi kudharauliwa. Wakala wa utalii kulalamikia kanuni zinazowalenga kwa madhumuni ya kutoza kodi tu na kuwakamua watalii wenyewe! Isitoshe. Kwa taasisi inayohusika na usimamizi wa hifadhi ya bahari inapovunja sheria yake yenyewe iliyoiandika na kuruhusu uvuvi haramu wa kutumia mkuki (*Spearfishing*) ni jambo ambalo linapaswa kukemewa kwa hali zote.

b) Uvuvi haramu na uharibifu wa Matumbawe

Vile vile, matumbawe yetu ya mwambao yamekuwa yakipotea kwa kasi kubwa. Uvuvi haramu, usimamizi usioridhisha wa maeneo ya uvuaji baharini, uchafuzi wa mazingira ya bahari na ukataji ovyo wa mapori ya visiwa vidogo vidogo vilivyomo ndani ya hifadhi za baharini, yote haya yanaidumaza sekta ya utalii endelevu wa baharini pamoja na kuhatarisha maisha ya wakaazi wanaotegemea chakula kutoka sekta ya uvuvi.

c) Maslahi ya Wasimamizi wa Hifadhi

Wasimamizi wa hifadhi za baharini hawana uhuru wa kutosha wa kujenga maamuzi endelevu ya kusaidia kuzisimamia hifadhi hizi. Hakuna zana za kutosha kama maboti, mafuta, vitendea vingine vya kazi wala maslahi bora ya kuongeza ari katika usimamizi. Mara nyingi watendaji hushirikishwa katika harakati au shughuli ambazo hazijali sana uhifadhi wa mazingira na ambazo zina mafungamano ya kisiasa.

d) Mipaka ya Hifadhi

Mipaka ya maeneo ya hifadhi za baharini ni jambo nyeti na linalogusa kila eneo la maisha ya mwanadamu Zanzibar. Utaratibu uliofuatwa wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kuunda mipaka ya hifadhi za baharini kwa kutumia kanuni ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010, badala ya kupelekwa Sheria mama kamili inayohusiana na usimamizi wa hifadhi za kimazingira baharini, umeleta mgogoro mkubwa baina ya Serikali, washiriki wa utalii na wavuvi wenyewe. Kuna haja ya kuiangalia upya kanuni hii na kutoa haki na fursa kwa wote bila ya kuathiri malengo ya uhifadhi wa mazingira ya nchi yetu.

e) Ujenzi ndani ya visiwa vidogo vilivyomo ndani ya Hifadhi

Pamoja na kuwa taasisi inayoshughulikia na usimamizi wa ardhi Zanzibar ilitangaza kusimamishwa kwa mipango yoyote ya ujenzi wa mahoteli katika visiwa vidogo vidogo visivyokaliwa na binadamu (*Moratorium on Development of Remote Islets*), lakini bado taasisi hiyo inaonekana kuruhusu baadhi ya miradi kuendelea kunako visiwa hivi hasa vile vya Ghuba ya Menai. Suala la Kisiwa cha Kwale limezua manung'uniko kutoka kwa wananchi wanaotumia maeneo hayo na kuleta mjadala katika Baraza la Wawakilishi. Hivi karibuni kuna taarifa ya kutolewa uamuzi wa kuruhusu ujenzi wa hoteli katika Kisiwa cha Nyamembe kilichopo ndani ya mlango wa Ghuba ya Kiwani, Fumba.

CUF inamini kuwa kukosekana kwa uwazi, mipango na mikakati shirikishi katika kutoa maamuzi endelevu ya matumizi ya ardhi

ndiyo chanzo cha kuzuka kwa migogoro mbali mbali ya kitaasisi na kijamii. Ikiwa mipaka ya hifadhi za baharini inajulikana na imewekwa na watawala wenyewe, kwa nini basi watawala hawa hawa wanalazimisha ujenzi wa hoteli ndani ya mipaka ya hifadhi za kimazingira?

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itaunda Sheria Mpya itakayoitwa Zanzibar Marine Protected Areas Act kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji huru wa shughuli za uhifadhi wa mazingira ya bahari ikiwemo Bodi Huru na shirikishi yenye sekta kuu na binafsi itakayosimamia masuala ya uhifadhi na mapato ya hifadhi hizi.*
- *Itahakikisha mipaka yote ya hifadhi za baharini inawekwa kwa kuzingatia unyeti wa eneo lenyewe (Environmentally Sensitive Area), haki za wananchi katika matumizi ya maliasili za baharini (User Rights), usawa wa jamii (social equity), ushirikishwaji wa jamii katika maamuzi ya ugawaji wa mipaka (community involvement & participation) uwazi na uwajibikaji wa taasisi zote husika (transparency, institutional and legal compliance), utii wa sheria za nchi (respect for the rule of law) na utaratibu wa mipaka utakaopitishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.*
- *Itasimamia sheria katika kuhakikisha kuwa uvuvi wowote haramu uliopigwa marufuku chini ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 ukiwemo wa kutumia mkuki (Spearfishing) hauruhusiwi katika mazingira yeyote yale.*
- *Itahakikisha Sheria ya Utalii kuhusiana na utoaji wa vibali kwa wakala wa utalii (tour operators) inafuatwa ili kusimamia uhifadhi wa mazingira ya baharini na kudhibiti uvuvi wa michezo (Sportfihsing) ndani ya hifadhi za baharini.*
- *Itasimamia maslahi bora ya wasimamizi wa hifadhi za mazingira za bahari (Park Rangers) na kuhakikisha utoshelezaji wa zana za ulinzi ya hifadhi hizo na vitendea kazi vingine.*
- *Itatekeleza tamko (Moratorium) la uzuiaji wa shughuli za ujenzi katika visiwa vidogo vidogo visivyokaliwa na watu kama ilivyopendekeza tangu awali na taasisi inayoshughulikia na usimamizi wa ardhi.*

9.5. MABADILIKO YA TABIA NCHI

Visiwa vyetu vinakabiliwa na janga zito la mabadiliko ya tabia nchi. Athari za mabadiliko ya misimu, mvua, joto, kupanda kwa kina cha bahari, n.k. ni moja kati ya changamoto zinazoukabili uchumi, mazingira, bioanuwai, na maendeleo ya jamii yetu. Kama nchi nyingine yeyote ya kisiwa kidogo, tunalazimika kuchukua hatua za kihistoria za kuanza kujenga uchumi na jamii inayozingatia hatari hii ya mabadiliko ya tabia nchi. Hatuwezi kutimiza haja hii peke yetu na ni lazima tupate misaada na mashirikiano ya kiufundi na taaluma, kifedha, sera na mipango, pamoja na kuwa na muundo bora na thabiti unaokidhi haja ya utekelezaji wa mikakati yetu na mipango kazi inayotakiwa ya kufikia malengo tuliyojiekea ya kujihami na mabadiliko haya.

CUF inaamini kuwa pamoja na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa hivi sasa za kuanzisha muundo wa uongozi na usimamizi wa masuala ya kujihami na mabadiliko ya tabia nchi, utafiti na utengenezaji wa mikakati na mipango kazi ya kujihami, elimu ya jamii na uwezeshaji, pamoja na ushajiishaji katika utunzaji wa mazingira, misitu, na bioanuwai, bado hatujaweza kusimamisha programu yetu sambamba na vipaumbele vya nchi ya Kisiwa kidogo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaendelea kuboresha muundo wa kitaifa wa kitaasisi wa utekelezaji wa programu za kujihami na mabadiliko ya tabia nchi wenye sura ya nchi ya Kisiwa kidogo.*
- *Itatayarisha sheria itakayopelekea kuanzishwa kwa mfuko maalum wa kujihami na masuala ya mabadiliko ya tabia nchi (Climate Change Fund) utakaosimamia matumizi ya utekelezaji wa programu za kujihami na mabadiliko hayo kwa kuzingatiwa vipaumbele vya jamii yetu ya kisiwa.*
- *Itahakikisha kuwa mipango yote ya maendeleo na uwekezaji kitaifa, inatungwa na kutekelezwa kwa kuzingatia athari za*

mabadiliko ya tabia nchi hususan katika kukabiliana na hatari za kimambile na bahari.

- *Itazidisha uwekezaji katika kuratibu na kuongoza programu za kujihami na mabadiliko ya tabia nchi, kuzidisha utafiti na utengenezaji wa mikakati na mipango kazi ya kujihami, kuongeza viwango vya elimu ya jamii na uwezeshaji, pamoja na ushajiishaji katika utunzaji wa mazingira, misitu, na bioanuwai.*
- *Itaendelea kushirikiana na washiriki wa kimaendeleo wa ndani na nje, wakiwemo wa kikanda na kimataifa katika kuisadia Zanzibar kutekeleza mpango kazi wake wa kujihami na mabadiliko ya tabia nchi.*
- *Itashirikiana kwa ukaribu zaidi na washiriki wa kikanda kama Indian Ocaean Commission (IOC) na washiriki wa kimataifa wa nchi za visiwa vidogo vidogo (SIDS) katika ngazi zote za mahusiano ili kuipa Zanzibar fursa zaidi ya maendeleo yake yanayotokana na maliasili zake ambazo sasa zipo hatarini kutoweka kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi.*
- *Itahakikisha ushirikishwa kwa ukamilifu wa Zanzibar katika Mkataba wa Umoja Mataifa wa Ukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi (United Nations Convention on Climate Change) ikiwemo kufunguliwa kwa Ofisi maalum ya "Alternate Focal Point" wa Zanzibar*

9.6. MATUMZI YA KEMIKALI HATARISHI

Ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kimaendeleo Zanzibar na hususan katika masuala ya kilimo, afya, viwanda, mahoteli, na huduma nyingine za jamii, kumepelekea ongezeko la uagizaji wa kemikali hatarishi nchini. Wananchi wengi huwa hawana ufahamu na madhara ya kemikali hizi. Wakulima hutumia kemikali za kuua wadudu bila ya elimu ya kutosha, halikadhalika wananchi hutumia kemikali majumbani kwa sababu mbali mbali za usafi, kuua wadudu kama mbu na mchwa, n.k.

Hakuna utaratibu maalumu wa kuruhusu au kudhibiti kemikali hatarishi zinazoagizwa nchini na hii imepelekea ongezeko la hatari ya madhara za kemikali. CUF inaamini kuwa wakati umefika wa kuliangalia suala zima za kemikali hatarishi – na si kwa jicho la kilimo tu – bali kuhusiana na hali halisi nzima ya matumizi yake kwa mazingira na afya ya binadamu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itafanya usimamizi bora wa uagizaji, matumizi na utupwaji au umwagaji wa kemikali hatarishi.*
- *Itazipitia kwa umakini kemikali zinazotumika kwa ajili ya masuala ya upulizaji wa dawa za kuua mbu, wadudu waharibifu wa kilimo, wadudu waharibifu wa nyumbani, pamoja na kemikali nyingine zinazotumika katika sekta mbali mbali ikiwemo za viwanda, afya, masoko, na mahoteli ili kuhakikisha usalama wa afya ya binadamu na mazingira.*
- *Itaendelea kuiboresha maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali iwe huru, inayojitegemea, isiyoingiliwa, na yenye kufanya kazi zake karibu sana na mtandao wa Stategic Approach to International Chemicals Management (SAICM) katika kuhakikisha ufanisi zaidi katika usalama wa afya ya binadamu na mazingira.*

9.7. MAZINGIRA NA SEKTA YA MAFUTA NA GESI

Uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar hautakuja bila ya athari za kijamii na kimazingira. Masuala ya matumizi ya ardhi, bahari, uvuvi, usimamizi wa taka, hatari ya janga la kuvuja mafuta au gesi asilia, na masuala mengineyo yanayohitaji sera, mipango na mikakati ya kina ya kusimamia uhifadhi wa mazingira, bioanuwai, matumizi bora ya ardhi na uwezo wa kukabiliana na majanga ya ajali.

CUF inaamini kuwa yote haya yataweza kufanyika ikiwa kutakuwepo na Serikali makini inayojali mafanikio ya kweli na kwa maendeleo na maslahi ya umma ya Sekta hii.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itaupitia muundo mpya wa taasisi inayoshughulika na usimamizi wa mazingira na kuinyanyua kufikia kiwango kinachohitajika cha taaluma za fani mbali mbali zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira katika sekta ya mafuta na gesi.*
- *Itaandaa utaratibu mpya wa kusimamiwa kwa tathmini ya kimkakati ya mazingira (Strategic Environmental Assessment) katika sekta ya mafuta na gesi ili kukidhi haja ya kuwepo kwa mipango endelevu iliyotengamana na sekta nyingine za uchumi, jamii na maendeleo katika uhifadhi wa mazingira.*
- *Itaboresha usimamizi bora wa kimazingira kwa kuunda kitengo maalum cha wataalamu wa mazingira ndani ya Wizara ya Mafuta na Gesi kitakachoratibu usimamizi wa mazingira, usalama kazini na afya ya binadamu katika sekta ya mafuta na gesi kwa mashirikiano na taasisi kuu ya usimamizi wa mazingira.*

9.8. USIMAMIZI WA TAKA

Hali yetu ya usimamizi wa taka nchi nzima imekuwa ni ya kusikitisha sana. Haiba ya mji wetu wa Zanzibar imechakaa kwa sababu ya kukosekana kwa mipango madhubuti ya usimamizi wa taka. Majaa yameachiwa kuzagaa mpaka katika mitaa wanayoishi binadamu. Fukwe zetu ambazo ni vivutio vikuu vya utalii zimekumbwa na janga la taka hatarishi mbali mbali. Usimamizi wa taka za sekta ya afya na kilimo pia sasa imekuwa ni jambo la hofu. Mifuko ya plastiki, japokuwa kwa kiasi kikubwa imedhibitiwa kutokana na jitihada za taasisi inayosimamia mazingira, bado inaendelea kuingizwa kimagendo na kutumiwa kwa njia za chini chini.

a) Misaada ya Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo

Nchi wahisani kama Umoja wa Ulaya pamoja na Benki ya Dunia zimesaidia sana katika kuboresha uwezo wetu wa kusimamia ukusanyaji, usafirishaji na utupwaji wa taka. Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNIDO na UNOPS yamekuwa mstari wa mbele katika tafiti na hata katika kusaidia miundombinu ya taka. Lakini bado hakuna sera, mipango wala mikakati madhubuti ya kitaifa ya kukabiliana na usimamizi wa taka. Kila taasisi ya Serikali inashughulika kivyake na hii haisaidii kabisa hali halisi ya sekta ya usimamizi wa taka hapa Zanzibar.

b) Hali ya Jaa Kuu la Kibele

Uamuzi wa kuweka jaa kuu la Kibele lililo bora na linaloendeshwa kwa misingi ya usafi (*Sanitary Landfill*) ulikuwa ni uamuzi ambao ungepelekea kwa kiasi kikubwa kulimaliza suala la kuwepo kwa jaa kuu la taka. Benki ya Dunia imejitolea kwa dhati katika kuisaidia Zanzibar katika kulimaliza tatizo la usimamizi wa taka. Lakini inasikitisha kuona taasisi husika za ndani zimekosa mashirikiano ya karibu na uratibu wa pamoja wa kuhakikisha malengo ya usimamizi wa jaa kuu yanafikiwa. Matokeo yake ni kukosekana kabisa kwa utaratibu wa kazi, wahudumu wa kutosha, kutokuwepo kabisa kwa miundombinu na vitendea kazi vya kutosha kwa wahusika wa jaa hili. Taka zinatupwa ovyo bila ya mpangilio mpaka kusababisha hatari kwa mazingira, pamoja na usalama wa afya za wananchi wa eneo hili ndani ya Shehia ya Tunguu.

c) Wakusanyaji wa taka wa sekta binafsi

Washiriki wa sekta binafsi bado hawajawezeshwa katika usimamizi mzuri wa masuala ya ukusanyaji, usafirishaji wa taka hususan kutoka katika mahoteli ya kitalii. Maeneo ya utupwaji wa taka za mahoteli ya kitalii yameleta changmoto kubwa na kupelekea mizozo baina ya wananchi na wenye mahoteli. Serikali ina wajibu wa kuongoza suala zima la usimamizi wa taka hata ikiwa hizo taka zinakusanywa kwa utupwaji na sekta binafsi.

d) Bidhaa zinazotokana na taka (Waste Recycling Products)

Pamoja na wananchi kushajiishwa njia za ujasirimali katika taka (*Waste Recycling*) bado sekta hii haijapewa kipaumbele kinachostahiki na Serikali ya CCM. Kuna fursa kubwa ya kuanzisha na kuendesha shughuli mbali mbali za ujasirimali katika fani hii ya uzalishaji wa bidhaa kutokana na taka.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itapitia upya muundo wa uongozaji na usimamizi wa taka.*
- *Itatengeneza mazingira bora ya uwekezaji kualika sekta binafsi kuwekeza zaidi katika usimamizi wa taka.*
- *Itaunda sera na mipango bora ya utekelezaji wa kuwepo kwa jaa kuu (Sanitary Landfill) pamoja na operesheni zake bila ya kuathiri maisha ya watu, mazingira na afya zao.*
- *Itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo wa kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, UNDP, UNIDO, na UNOPS katika kuboresha huduma na miundombinu ya usimamizi taka.*
- *Itaendelea kutoka elimu ya jamii na uwezeshaji kwa wananchi ili kuinua kiwango cha uhifadhi wa mazingira na usimamizi wa taka.*
- *Itasaidia kuwekeza katika ujasirimali wa uzalishaji wa bidhaa kutoka taka.*

9.9. MIKATABA YA KIMATAIFA YA MAZINGIRA

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini mikataba, itifaki, na makubaliano ya kimataifa zaidi ya 24 inayohusika na masuala mbali mbali ya uhifadhi wa mazingira (*Multilateral Environmental Agreements*). Mikataba na itifaki hizi ni muhimu katika shughuli za kila siku za uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu kwa ujumla kwa nchi na jamii yenyewe. Lakini inashangaza kuona kuwa hakuna *National Focal Point, Alternate Focal Point, Contact Point, Desk Officer* au mwakilishi yeyote anayetambuliwa na mkataba au itifaki yeyote ile ambayo Tanzania imesaini --- mwenye makaazi yake rasmi Zanzibar.

Hali hii imeinyima fursa kabisa Zanzibar ya kupanga mipango yake ya uchumi endelevu kwa kusaidiwa moja kwa moja kutoka katika sekretariati za mikataba na itifaki hizo. Hii imepelekea kudorora kama si kukwama kwa fursa nyingi ambazo Zanzibar ingezipata kama kungekuwapo na utambulizi wowote wa uwakilishi wa taasisi na sekta za Zanzibar ndani ya mikataba na itifaki hizi. Haya ni katika mambo ya msingi ya Muungano ambayo CUF itayasimamia kuhakikisha Muungano wa haki, heshima na usawa.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itasimamia haki ya Zanzibar katika uwakilishwaji ndani ya Mikataba na Itifaki za Kimazingira ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini ili kuhakikisha nafasi ya kudumu ya Zanzibar ndani ndani ya Mikataba na Itifaki hizo.*

9.10. UTOAJI WA ELIMU YA MAZINGIRA

Elimu ya Mazingira ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu. Pamoja na kuwepo haja ya kuendelea na jitihada mbali mbali za taasisi zetu za kushajiisha wananchi kujali na kuhifadhi mazingira na bioanuwai, bado hakuna uwekezaji wa kitaasisi katika kufanya tafiti mbali mbali za kisekta zinazohusiana na tathmini za kimazingira.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itazidisha tafiti mbali mbali ikiwemo tathmini za kimazingira ili kuhakikisha usimamizi bora wa mazingira.*
- *Itaendelea kuongeza nguvu kazi na uwekezaji katika elimu ya jamii kuhusiana na mazingira.*

10. TUTAKUZA HUDUMA NA VIWANGO VYA ELIMU KWA UHAKIKA

CUF inatambua kuwa elimu ni haki ya msingi ya binadamu. Ndio ufunguo wa maendeleo endelevu, amani na utulivu. Ndio rasilimali ya kibinadamu ya Taifa inayoamua juu ya sura na kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Umaskini mkubwa uliokithiri nchini unachangiwa kwa kiasi kikubwa na kiwango duni cha elimu. Tumefanikiwa kuhakikisha watoto wetu wanapata nafasi ya kwenda skuli (quantity) lakini bado hatujafanikiwa kabisa katika suala la viwango vya elimu (quality) inayotolewa. Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF katika mipango yake imekusudia kuinua kiwango cha elimu na kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha elimu na utamaduni katika Afrika ya Mashariki na Kati.

10.1. MSONGAMANO WA WANAFUNZI

Skuli zimefurika wanafunzi kwa wastani wa wanafunzi 60 mpaka 80 kwa darasa moja. Wengi wa wanafunzi wanakaa kwenye sakafu, na mbaya zaidi ni kwamba sakafu zenyewe zina vumbi kiasi cha kuathiri afya za wanafunzi. Badala ya kujenga maskuli yenye viwango vinavyokubalika, tumekuwa tukijenga mabanda machache tena duni na kuyafanya madarasa. Bado wananchi wetu ambao wengi ni masikini wanalazimika wajenge mabanda ya skuli katika maeneo yao na pia kulazimika kuchangia gharama za uendeshaji wa sekta ya elimu kwa michango ya moja kwa moja katika maskuli.

Idadi kubwa ya wanafunzi na uwezo mdogo wa maskuli umelazimisha maskuli kuwa na mikondo miwili au hata mitatu, jambo ambalo linapunguza muda wa kusomesha, na kupelekea kuanguka kiwango cha elimu kila mwaka. Katika miaka mitano iliopita, skuli za Zanzibar zimekuwa zikiongoza kwa kufanya vibaya katika mitihani ya Taifa. Pia idadi kubwa ya wanafunzi wanaacha skuli kabla ya kumaliza.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itajenga skuli mpya za kisasa na kuongeza madarasa kadiri inavyohitajika ili kuondoa msongamano madarasa na mfumo wa mikondo miwili haraka iwezekanavyo.*
- *Itaweka vigezo vya ukubwa wa darasa, idadi ya walimu na idadi ya vipindi kwa kila mwalimu katika viwango vinavyokubalika kimataifa na vitakavyopelekea ukuaji wa haraka wa viwango vya elimu.*
- *Itaanzisha utaratibu wa kufanya tathmini na ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ubora wa elimu inayotolewa.*
- *Itafanya jitihada maalum zitakazowavutia wanafunzi kuwa na hamu ya kuendelea na masomo ili kupunguza idadi ya wanaokimbia na kukatiza masomo.*

10.2. HALI NGUMU YA WALIMU

Walimu hawathaminiwi na mishahara, maslahi na marupurupu yao hayalingani na kazi ngumu wanayoifanya ya kulielimisha Taifa na kulijengea msingi wa maendeleo. Ingawa Wizara ya Elimu inadai kwamba asilimia 80 ya walimu wamepata mafunzo, lakini mafunzo haya hayaridhishi, hali inayodhihirika mtu anapoangalia viwango vya kufaulu mitihani na uelewa wa wanafunzi wa Zanzibar. Wahitimu wengi kutoka vyuo vya elimu wanasomesha katika madaraja makubwa kuliko uwezo wao. Hatuwezi kutegemea kiwango cha elimu kunyanyuka kutokana na mishahara na marupurupu madogo wanayolipwa walimu.

Pia kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi. Walimu wengi wenye sifa walifukuzwa kazi katika miaka ya ’90 kwa sababu za kisiasa. Walimu waliohitimu hawasambazwi kwa usawa baina ya Unguja na Pemba na baina ya mjini na mashamba. Walimu wanaohamishwa

kwenda Pemba au mashamba hawapewi posho na fursa zinazostahiki. Isitoshe, skuli nyingi za mashamba hazina nyumba za walimu na hufanya walimu wanaopelekwa na kubaki huko kuwa ni jambo gumu.

Kanuni za utumishi (Scheme of Service) hazijatekelezwa kwa zaidi ya miaka 10 kwa kisingizio cha bajeti finyu. Upandishwaji vyeo wa walimu haufanywi kwa uwazi wala haufuati mfumo wa ajira uliokubaliwa. Kwa hakika hakuna mfumo wa motisha na hilo linaangusha ari na moyo wa utendaji na kujituma na kuwanyima fursa ya kujiendeleza kielimu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itakuza uwezo wa walimu kwa kuwapatia mafunzo ya kabla na ndani ya ajira.*
- *Itaanzisha kampeni kabambe kuwaajiri watu wanaoonesha vipaji vya ualimu, na tunza zitatolewa kwa walimu ambao madarasa yao yatafanya vizuri katika mitihani ya elimu ya msingi na ya taifa kama zawadi na motisha kwa wengine.*
- *Itaweka wazi ajira ya walimu kufuatana na mahitaji ya elimu na kupitia mitihani ili kuhakikisha wanaajiriwa walimu wenye sifa zinazohitajika.*
- *Itawapa walimu uzoefu wa kufanya kazi mashamba na mijini kama sehemu ya maendeleo ya kikazi.*
- *Itahakikisha walimu wanaofanya kazi nje ya makaazi yao wanapatiwa nyumba.*
- *Itatekeleza kikamilifu Kanuni za Utumishi wa Walimu na kwa uwazi kabisa itazienzi na kuheshimu juhudi za walimu. Hizo ndizo zitakazoamua utoaji wa mafunzo zaidi na upandishwaji vyeo.*
- *Itafanya mazungumzo na nchi washirika wa maendeleo na mashirika ya kimataifa kama vile PeaceCorps na Voluntary Services Overseas kwa ajili ya kuendelea kupatiwa walimu wa kutosha wa masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi wanaopenda kuja kufanya kazi kwa kujitolea katika nchi zinazoendelea ili kuziba pengo lililopo wakati mikakati ya kusomesha na kuwaendeleza walimu wa ndani ikiwa inatekelezwa.*

10.3. VIFAA VYA KUSOMESHEA

Hali ilivyo sasa Inasikitisha sana kuona skuli nyingi za sekondari hazina maabara na hizo chache zilizo nazo hazina vifaa vya kutosha ama kukosa walimu wenye sifa. Kuna upungufu wa kutisha wa vitabu vya kufundishia katika skuli zetu. Pamoja na dunia kubadilika na kuongezeka kwa mahitaji ya elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA), bado skuli zetu nyingi hazina kompyuta wala hazijaunganishwa na mtandao wa ‘internet’ kwa lengo la kuwapa wanafunzi wetu nafasi ya kujifunza mambo hayo tokea wakiwa wadogo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inyoongozwa na CUF itafanywa yafuatayo:

- *Itahakikisha kuwa kila skuli ina vifaa vya kutosha, ikiwa ni pamoja na vitabu vya kiwango kinachotakiwa kwa mujibu wa idadi ya wanafunzi wake.*
- *Itaanzisha na kusimamia kikamilifu mpango wa kuhakikisha kuwa skuli zote za msingi na za sekondari zinakuwa na Maktaba za kisasa za kuwahudumia wanafunzi na kukuza vipaji vyao vya kujisomea na kujiendeleza.*
- *Itaiimarisha Maktaba Kuu ya Serikali kwa kuiongezea hadhi na uwezo na kuipatia vitabu na machapisho yote muhimu na pia itaanzisha na kuziimarisha Maktaba za Mikoa na Wilaya ili kusogeza huduma hizi kwa wananchi wote wakiwemo wale wa vijijini.*
- *Itahakikisha kuwa skuli zote za sekondari zinapatiwa maabara zilizotimia.*
- *Itahakikisha kuwa skuli zote za sekondari zinakuwa na maktaba ili kuanza kuwajengea uwezo wanafunzi tokea awali.*

- *Itaipatia kila skuli ya Zanzibar kompyuta za kutosha kwa ajili ya kukuza elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA).*

10.4. MITAALA

Mitaala ni mikubwa mno na haizingatii mahitaji ya mwanafunzi. Mitaala mingi inayotumika bado inazingatia mahitaji ya mfumo wa kikoloni na haiendani na mahitaji ya Zanzibar ya sasa na malengo ya kiuchumi na kimaendeleo ya jamii tunayokusudia kuijenga. Daima haikamilishwi kutokana na saa za kusomesha kupungua kwa sababu ya kuingiliwa mara kwa mara na mambo ya kisiasa na mfumo wa mikondo miwili.
Mabadiliko ya mitaala hayaendi pamoja na matayarisho ya walimu na maendeleo ya vitabu vya kusomeshea. Hakujatolewa mkazo unaostahiki wa elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA).

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inyoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itafanya mapitio na kutekeleza mageuzi ya mitaala ambayo yataangalia zaidi umuhimu (relevance) wake na muda unaowekwa kwa kila somo.*
- *Itahakikisha kuwa msingi wa mitaala unazingatia umuhimu wa yale masomo wanayosoma wanafunzi, jinsi gani wanavyosoma na yana faida gani kwao na mahitaji ya Zanzibar ya sasa na malengo ya kiuchumi na kimaendeleo ya jamii tunayokusudia kuijenga.*
- *Itahakikisha kuwa elimu na mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) vinapewa nafasi kubwa katika mitaala ya masomo kuanzia ngazi ya skuli za msingi hadi vyuo vikuu.*

10.5. UENDESHAJI WA SEKTA YA ELIMU

Katika vitu vinavyoizorotesha sekta ya elimu ni tatizo la viongozi wachache wa juu kujilimbikizia madaraka yote badala ya madaraka hayo kukasimiwa kwa viongozi wa ngazi zote. Hivi sasa zaidi ya asilimi 90 ya bajeti ya kawaida ya Wizara ya Elimu inatumika kwa malipo ya mishahara na asilimia 10 tu kwa kazi za utunzaji wa majengo, ununuzi wa vifaa vya kusomeshea na kwa kulipia huduma nyengine za kielimu darasani. Hii ni hatari.

Ukosefu wa nidhamu katika matumizi ya fedha na kutumia fedha za huduma za elimu kwa shughuli za kisiasa kumedumaza maendeleo ya elimu. Mfumo wa elimu usioeleweka wenye aina na ngazi zisizopungua kumi unachangia katika kuzorotesha maendeleo ya elimu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inyoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itafuta mazonge ya utawala mbovu katika sekta ya elimu kwa kukasimu vyema madaraka katika ngazi zote za uongozi na usimamizi wa elimu.*
- *Itaongeza bajeti ya fedha zinazotengwa na kutolewa na Serikali kwa sekta ya elimu kila mwaka hadi kufikia asilimia 15 ili kuharakisha maendeleo ya elimu visiwani Zanzibar.*

- *Itafanya marekebisho makubwa kwenye mfumo wa elimu ili uwe rahisi kwa watoto, walimu na wazazi.*
- *Itafanya utafiti kuona sababu za kufeli kwa wanafunzi na kuchukuwa hatua za kukabiliana na sababu zitakazobainika ili kuongeza kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi wetu.*

10.6. ELIMU YA JUU

Elimu ya juu kwa Taifa lolote ni muhimu kwa sababu inalenga katika kuwaandaa wataalamu wa fani tofauti kuja kukabidhiwa majukumu mbali mbali kwenye jamii. Elimu ya juu mpaka sasa ni suala la Muungano ingawa utekelezaji wake hauonekani kwenda hivyo na kupelekea kutoifaidisha Zanzibar vile inavyopaswa.

Vyuo kadhaa vya elimu ya juu kikiwemo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na vile vya binafasi – Chuo Kikuu cha Zanzibar na Chuo cha Elimu cha Chukwani – vimeanzishwa na vimeweza kiasi fulani kusaidia kuziba pengo kubwa lililokuwepo la ukosefu wa mipango ya ndani ya nchi ya kujiandalia watalamu wake. Hata hivyo, bado kazi kubwa iko mbele yetu katika kuhakikisha kuwa vyuo hivi vinakidhi mahitaji ya kuwaandaa vijana wetu kushiriki ipasavyo katika ujenzi wa Zanzibar mpya.

Kutokana na ukosefu wa mipango makini tangu awali katika kuboresha elimu kwa ujumla, Zanzibar tumekuwa na udhaifu mkubwa katika suala zima la kuwaandaa wataalamu wetu. Siyo tu kwamba idadi ya wataalamu wanaoandaliwa ni wachache ikilinganishwa na mahitaji halisi, lakini pia ubora wa maandalizi yao hauridhishi.

Waajiri wengi nchini, na hasa wale wa sekta binafsi wamekuwa na upendeleo wa wazi wa wahitimu walioandaliwa kwenye vyuo vya nje kuliko wale walioandaliwa nchini. Ni dhahiri kabisa kuwa kwa hali tuliyo nayo Zanzibar itakwama katika juhudi za kuboresha uchumi na kujiletea maendeleo iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa mapema siyo kuongeza tu idadi ya wataalamu tunaowaandaa, lakini pia kuboresha utoaji wa taaluma katika taasisi zetu za elimu ya juu

a) Hali ya Vyuo Vikuu

Vyuo Vikuu vilivyopo Zanzibar vinakabiliwa na hali ngumu ya upatikanaji wa fedha za kutosha kukidhi mahitaji yake na kuweza kuviendeleza mbele. Wasomi wakiwemo wahadhiri katika taasisi zetu za elimu ya juu wamekuwa wakiondoka na kwenda Tanzania Bara na vyuo vya nchi nyingine za Kiafrika kutokana na maslahi duni wanayopata hapa nchini. Katika vyuo vyetu vyote vya elimu ya juu, huduma za kitafiti bado zinalegalega na hazijapewa umuhimu kutokana na kushindwa kutenga fedha kwa shughuli hiyo.

b) Uchangiaji wa Gharama

Bila kujali kwamba kimsingi Zanzibar haijafikia wakati wa kuhitaji wanafunzi wetu wanaosoma katika taasisi za juu za elimu kuchangia gharama, Serikali imeulazimisha utaratibu huo kutumika bila kuzingatia mizani ya faida na hasara zake kwa jamii ambayo wananchi wake wengi ni masikini. Kumekuwa na kulazimisha kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma katika taasisi za juu kusikoendana na uboreshaji wa huduma za msingi zinazohitajika. Matokeo yake ni kwamba mazingira ya wanafunzi wanaosoma yanaendelea kuwa magumu kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita.

c) Bodi ya Mikopo

Kuundwa kwa Bodi ya Mikopo ya elimu ya juu Zanzibar hakujasaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo yao. Kundi kubwa la wahitimu wa kidato cha nne na sita limekua likikosa mikopo ya kuendelea na masomo. Utoaji wa udhamini wa mikopo kwa madaraja; vigezo vya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi hauzingatii hali halisi ya maisha na uwezo wa kifedha za wazazi wa wanafunzi na unafanywa kwa kuwapendelea watoto wa wanasiasa na jamaa zao. Sehemu kubwa ya gharama za posho wakati wa mafunzo kwa vitendo yanayokwenda kufanywa na mwanafunzi wa Chuo Kikuu yanagharamiwa na mzazi na mwanafunzi peke yake. Serikali haioni umuhimu wa mafunzo haya na ina mchango kidogo sana katika kuwezesha mafunzo bora yaitendo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

d) Makaazi ya Wanafunzi

Wanafunzi wa vyuo vikuu leo wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa makazi ya kuishi. Serikali imeliacha suala hili kuwa mikononi mwa wanafunzi na wazazi. Kinachotokea ni kuwa wanafunzi wengi wanaotoka nje ya maeneo viliko vyuo vikuu wanalazimika kuishi kwenye baadhi ya vyumba duni vya kupanga na katika maeneo ya mbali na vyuo vyao. Kiwango cha mkopo wanachopewa wanafunzi kwa ajili ya kujikimu ni kidogo na hakitoshelezi kumfanya mwanafunzi kuweza kulipia gharama za chakula, malazi, anunue madaftari, sabuni, nauli, mawasiliano, matibabu, na mahitaji mengine.

e) Intaneti

Kushindwa kuviunganisha vyuo vikuu vya ndani ya nchi na huduma ya intaneti ya uhakika pamoja na kuvipatia kompyuta za kutosha ni tatizo linaloathiri uharaka wa kujifunza na kuendana na karne ya sayansi na teknolojia.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inyoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itaweka utaratibu utakaowawezesha vijana wote wenye sifa na waliochaguliwa kujiunga katika chuo kikuu chochote ndani ya nchi kupata elimu ya juu bila vikwazo.*
- *Itagharamia mahitaji yote ya msingi ya mwanafunzi wa elimu ya juu aliyepasi vizuri zaidi katika mitihani yake ya Daraja la A-Level bila mkopo.*
- *Itatoa mchango wa kutosha na kuhakikisha kuwa wanafunzi wa elimu ya juu wanapatiwa posho zinazokidhi mahitaji wanapokuwa vyuoni na wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo.*
- *Itatengeneza mtandao mzuri wa matumizi ya intaneti katika vyuo vikuu vyote vya Serikali na kuhakikisha kuwa panakuwa na kompyuta za kutosha kwa uwiano wa kompyuta moja wanafunzi wawili au kila mwanafunzi na laptop yake.*
- *Itahakikisha kuwa kila chuo kikuu au taasisi ya elimu ya juu kinakuwa na makazi thabiti yatakayotosheleza wanafunzi wote.*
- *Makampuni binafsi yatashajiishwa na kupewa motisha na Serikali kujenga dakhalia za kisasa za wanafunzi zilizounganishwa na mtandao wa intaneti katika kila chuo au taasisi.*
- *Kila mwanafunzi atawezeshwa kupata makazi yenye mazingira bora kwa usomaji, isipokuwa kwa yule ambaye kwa sababu binafsi atataka kukaa mahali pengine.*
- *Itaanzisha, kwa kushirikiana na wataalamu mbali mbali toka kwenye vyuo vinavyohusika, programu ya kuifanyia mapitio na marekebisho mitaala inayotumika ili ilenge zaidi kwenye kuandaa wahitimu walio tayari kwa kazi.*
- *Itatoa kipaumbele kwa ongezeko la nafasi za masomo katika fani za sayansi na teknolojia. Chini ya mkakati huu madaktari, mainjinia, wanasayansi na wataalamu wa kompyuta wengi zaidi wataandaliwa kila mwaka.*
- *Itaendelea kuziunga mkono juhudi za watu binafsi, mashirika ya dini, na taasisi nyingine zenye malengo ya kuanzisha vyuo vikuu kwa ajili ya taaluma mbali mbali, lengo likiwa ni hatimaye kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha elimu na mafunzo katika eneo la Afrika Mashariki na Kati.*
- *Itaanzisha kitengo maalumu cha uratibu wa kuzifanyia kazi tafiti/vumbuzi mbalimbali zinazopatikana kutokana na jitihada zilizofanywa katika vyuo vyetu kwa lengo la kusaidia ukuzaji wa uchumi na maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake.*
- *Itahakikisha kuwa maktaba za vyuo vikuu na taasisi nyengine za elimu ya juu zinakuwa na uwezo mkubwa sawa na maktaba za nj katika utafiti na usomaji wa kutumia Teknolojia ya ICT.*
- *Itafuta utaratibu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na badala yake kuwalipia bure wale watakaotimiza sifa.*
- *Itaipitia tena sheria ya Baraza la Mitihani Zanzibar na kuingiza mitaala ya elimu ya juu.*

11. TUTAIMARISHA SEKTA YA AFYA NA KUPAMBANA NA MAGONJWA SUGU

Ni dhahiri kwamba sekta ya usimamizi na uendeshaji wa huduma ya Afya na usawa katika ufikiwaji wa tiba kwa jamii Zanzibar inazidi kudorora. Kasi na juhudi za kudhibiti ugonjwa wa malaria, japokuwa kwa kiasi kikubwa umeweza kudhibitiwa chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, sasa imepungua kwa kiasi kikubwa. Maradhi yaliyokuwa yametoweka (Eradicated Diseases) kama ya Dengue na maradhi yanayofanana, pamoja na yale yaliyodharauliwa kabisa (Neglected Tropical Diseases) kama Kichocho na Minyoo sasa yanarudi. Kama nchi ya Kisiwa, tuna tatizo kubwa la ugonjwa wa kisukari na maradhi mengine yasioambukiza (Non Communicable Diseases) ambayo yanatishia usalama wa jamii, uchumi na maendeleo yetu. Suala la mapambano na virusi pamoja na ugonjwa wa UKIMWI linakabiliwa na changamoto za vipaumbele katika udhibiti, uwazi, ufikiwaji wa walengwa, uwekezaji na matumizi ya rasilmali za utoaji wa huduma zake, pamoja na tathmini ya takwimu za mafanikio yake. Tatizo la kuongezeka kwa matatizo ya afya ya akili na hususan kwa vijana linazorotesha juhudi za maendeleo na kuongeza maambukizi ya UKIMWI. Udhibiti na usimamizi wa Tiba Asilia hauridhishi na hii inahatarisha maisha ya wananchi wetu. CUF inaamini kuwa wakati umefika wa kufanya mageuzi makubwa katika Sekta ya Afya na kuuweka mfumo wa utawala bora na unaojali siha na maslahi ya wananchi.

11.1. HUDUMA ZA KINGA NA TIBA

Sekta ya huduma ya afya imenyimwa sana fedha katika bajeti ya Serikali. Matokeo yake ni uwezo mdogo wa huduma za afya, ushughulikiaji wa wafanyakazi, upungufu wa madawa na vifaa vya afya. Mipango ya usimamizi wa fedha ni dhaifu. Taarifa ya hali ya fedha haipo. Uwezo katika upangaji matumizi na uhasibu ni mdogo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina si wa wakati na si wa kutosha.Matumizi mengine kwenye afya yamekuwa yakishuka mwaka hadi mwaka, ikisababisha huduma za afya kuzidi kuwa dhaifu.

Moyo na ari kwa watoaji wa huduma za afya umeshuka. Malipo madogo, uchelewashaji wa mishahara na mafao, na kutothaminiwa kwa wafanyakazi waliopata mafunzo nchini kunaongeza unyonge na ubadhirifu kwa kusababisha tabia ya kutowajali wagonjwa. Wauguzi na madaktari wengi waliopata mafunzo na wenye uzoefu wanaondoka kutokana na tafrani zilizopona maslahi duni. Hii husababisha upungufu mkubwa wa wafanyakazi wenye ujuzi na kuporomoka kwa huduma za afya.

Licha ya kuwepo wahitimu wengi kutoka Chuo cha Afya Mbweni, Serikali imeshindwa kuwaajiri wahitimu hao na badala yake inaendelea kuajiri vikosi kila leo.Kasi ya maradhi na vifo ni kubwa ingawa mengi ya maradhi yanayosababisha vifo yanaepukika. Matukio ya magonjwa ya kawaida yanaendelea kuzidi.Vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano vinazidi kuongezeka, hii ni kwa sababu ya uwezo mdogo wa kukabiliana na magonjwa yanayowapata watoto.

Ukosefu wa dawa katika hospitali za Serikali umezidi kuwa ni mzigo kwa wananchi na wagonjwa wanalazimika kununua dawa licha ya mapato madogo waliyo nayo.Usambazaji wa wafanyakazi hauko sawa baina ya Unguja na Pemba na baina ya maeneo ya mjini na mashamba.Uhaba, ufinyu na uchakavu wa vituo vya afya pamoja na Hospitali na vifaa vya kuchunguzia magonjwa.Kutosimamiwa vyema maadili ya afya kwa kumtendea haki mgonjwa.

Viwango vya hospitali, vituo, kliniki na dispensary katika utoaji wa huduma za afya bado ni duni. Msongamano wa wagonjwa, watabibu wasio na sifa, majengo na maeneo

ya utowaji huduma yaliyokosa sifa imekuwa ni jambo la kawaida. Serikali inayoongozwa na CCM imeshindwa hata kuhakikisha haki ya kibinadamu ya mgonjwa katika kupatiwa huduma katika mazingira salama ya maisha yake. Ni hali inayotisha kuona wodi za Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja katika hali duni na ya kukata tamaa.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mkoani zitapatiwa vifaa vya kisasa na kutafuta mbinu zaidi za kuzijengea mahusiano na na maingiliano ya kubadilishana uzoefu katika hospitali kubwa za nje na vituo vya utafiti wa matibabu vya kimataifa ili kukuza uwezo wa madaktari na wauguzi wake.*
- *Itaboresha na kuzitanua Hospitali za Makunduchi, Kivunge, Micheweni, Vitongoji, Wete na Chake chake na pia kuangalia uwezekano wa Kujenga Hospitali kuu za wilaya zilizobaki. Hospitali zote za Wilaya na Mikoa zitawekewa Madaktari wenye ujuzi ili kuweza kutoa huduma zote muhimu.*
- *Itaimarisha huduma za Afya ya Msingi kwa kuweka Vituo Vya Afya kila kwenye skuli (kwa sehemu za Mashamba Unguja na Pemba) ili kuwasogezea wananchi huduma hizo kama inavyosema sera ya afya ya kila kwenye kilomita nne kuwe na kituo cha afya.*
- *Kuweka Madaktari Bingwa wa ndani na nje ya nchi katika Hospitali za Rufaa na Hospitali za mikoa na Wilaya Unguja na Pemba.*
- *Kuanzisha mfuko wa Bima ya Matibabu kwa Wafanyakazi wote wa Serikali pamoja na Wafanyakazi wa sekta binafsi ili kuweza kulipia huduma za matibabu na kuweza kuziboresha huduma za zitolewazo katika Hospitali zote za Serikali.*
- *Kuweka wakaguzi maalum "inspectors" kuangalia na kufatilia huduma na malalamiko yanayotolewa katika Hospitali zote za Serikali na za binafsi ili kuwalinda wananchi na uzembe unaoweza kuepukika.*
- *Kuimarisha Chuo Kikuu cha SUZA ili kuweza kutoa wataalamu wa Fani zote za Tiba hapa Zanzibar.*
- *Itawapatia maslahi bora na mishahari mizuri Madaktari, Wauguzi pamoja na Wataalamu wengine Tiba.*
- *Itashajiisha sekta ya afya binafsi na kuunda mfumo madhubuti wa kuratibu shughuli zao.*
- *Itaongeza mgao wa bajeti ya fedha katika afya ili kukuza utendaji kwa kujitahidi kufikia malengo yaliyowekwa na Azimio la Abuja (Abuja Declaration) linalotaka Serikali za nchi za Afrika kutenga angalau asilimia 15 ya bajeti zake kwa masuala ya afya.*
- *Itahakikisha kuwepo kwa mfumo bora wa kukasimu madaraka katika sekta ya afya unaotilia mkazo mkubwa katika utoaji wa huduma bora vijijini na hivyo kupeleka huduma za afya karibu na watu.*
- *Itaimarisha mfumo wa kinga na kuwekeza zaidi katika kugundua na kuepusha magonjwa mapema.*
- *Itaweka mfumo mzuri wa kufuatilia na kutathmini madawa kabla hayajasambazwa kwa matumizi.*
- *Itaweka uwiano na usambazaji wa wafanyakazi baina mjini na vijijini na baina ya Unguja na Pemba.*

11.2. MARADHI YALIYODHIBITIWA

Hofu ya kurudi kwa maradhi ambayo tayari yalikuwa yamedhibitiwa kwa miaka mingi huko nyuma (*Eradicated Diseases*) kunaleta hofu kuu ya msingi kuhusu mfumo tulio nao wa udhibiti wa maradhi na uwekezaji wetu katika vipaumbele vya kinga kwa wananchi. Hii inarejesha nyuma mafanikio tuliyoyapata miaka ya nyuma na kutoa mwanya mpya kwa majanga yanayosababishwa na maradhi haya kwa wananchi wetu. Ni ukweli uisofichika

kuwa maradhi kama ya Dengue na Homa ya Manjano ni tishio kwa usalama wa afya zetu. Na katika zama hizi za ukuwaji wa sekta ya utalii, ukosefu wa kipaumbele cha kujikinga na maradhi kama haya ni kuruhusu majanga ya miaka nyuma kurudi tena leo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itahakikisha usimamizi bora wa afya ya jamii (Public Health).*
- *Itazidisha miundombinu bora kwa ajili ya afya za abiria katika viwanja na bandari zetu ili kujikinga na maradhi ya dengue na homa ya manjano.*
- *Itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo na jumuiya za kimataifa katika mapambano dhidi ya magonjwa yaliyodhibitiwa.*
- *Itazidisha utoaji wa elimu ya afya jamii kwa wananchi.*

11.3. MARADHI YALIYODHARAULIWA

Kuongezeka kwa kesi mbali mbali za maradhi yaliyodharauliwa (*Neglected Tropical Diseases*)hapa Zanzibar kama vile kichocho (*Bilharzia*) na minyoo (*Schistosomiasis*) kunaonyesha jinsi utekelezaji mzima wa sera na mipango ya kinga na mapambano ya maradhi mbali mbali yalivyokosa mwelekeo. Lakini hili ni pia suala la haki za binadamu pamoja na usawa wa jamii (*Social Equity*) kwani maradhi haya yanashamiri kunako mazingira ya umaskini, kutakuwepo kwa haki na usawa wa kweli katika kuwahudumua wananchi, na ukosefu wa usalama wa maji au chakula. Hichi ni kipimajoto muhimu cha kuona jinsi Serikali inayoongozwa na CCM ilivyokosa dira ya kweli ya kuwakomboa wananchi kutoka katika majanga kama haya yanayotishia afya, ustawi wa jamii na maendeleo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itahakikisha usimamizi bora wa afya ya jamii (Public Health).*
- *Itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo na mashirika ya kimataifa katika mapambano dhidi ya magonjwa yaliyodharauliwa.*
- *Itazidisha utoaji wa elimu ya afya ya jamii kwa wananchi kwa madhumuni ya kinga na udhibiti wa ugonjwa.*

11.4. MARADHI YASIOAMBUKIZA

Maradhi yasiyoambukiza (*Non-Communicable Diseases au NCD*) kama yale ya ugonjwa wa moyo (*cardiovascular diseases*), presha (*obstructive pulmonary diseases*), kansa (*cancers*) na ugonjwa wa kisukari (*Diabetes*) yanazidi kumung'unyua nguvu kazi ya taifa letu na kupoteza kasi ya maendeleo. Miaka ya karibuni ripoti ya sera za kimataifa za Marekani ilionyesha jinsi jamii za nchi za visiwa vidogo kote duniani zinavyokabiliwa vibaya na maradhi haya ya NCD na kufikia kutishia usalama mzima wa jamii hizi na maendeleo yao.

Kumung'unyuka kwa desturi asilia za maisha ya watu wa visiwa vidogo kama Zanzibar kunachangiwa sana na mabadiliko ya tabia ya jamii (lifestyle change) na kuongezeka kwa matumizi ya vyakula vya kuagiza (imported and processed foods), au uvutaji wa sigara, au matumizi kupita kiasi ya pombe, au ukosefu wa harakati za mazoezi kwa binadamu. Serikali inayojali maisha na siha za wananchi wake inapaswa kutambua tatizo hili na kulitangaza janga hili la maradhi ya kisukari, presha, moyo na kensa kama ni janga la taifa linalohitaji mpango kabambe wa muda mrefu wa kupambana nalo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itakiboresha kitengo kinachohusiana na masuala ya Magonjwa yasiyoambukiza au Non Communicable Diseases (NCD) kuwa taasisi kamili tiba na utafiti inayojitegemea pamoja na wataalamu wa kutosha waliojitolea kuokoa maisha ya wananchi wanokabiliwa na masuala mabli mabli ya NCD.*

- *Itaupitia mfumo mzima wa uagizaji wa madawa ya wagonjwa wa kisukari na kuhakikisha usalama wa afya zao.*
- *Itahakikisha elimu bora ya afya ya jamii (Public Health) inayoshajiisha mabadiliko ya tabia, matumizi ya dawa bora na zinazofaa, matumizi ya zana za kupimia, ziara za vipindi za kliniki, kufuata miiko, na kufanya mazoezi ili kupambana na matatizo ya kisukari.*
- *Itaendelea kushirikiana na washiriki na mashirika ya maendeleo ya kimataifa katika mapambano dhidi ya magonjwa ya NCD.*

11.5. MARADHI YA MALARIA

Ni ukweli usiofichika kuwa juhudi zilizofanywa chini ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa mashirikiano na washiriki, mashirika ya maendeleo na nchi wahisani kama Marekani, zilifana sana katika kudhibiti mripuko sugu wa ugonjwa wa malaria. Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yaliweza kudhibiti magonjwa mapya na vifo hususan vya kina mama na watoto. Lakini ukosefu wa vipaumbele katika kuziendeleza juhudi hizi kumelegeza mapambano kwa kiasi mpaka kufikia kushuhudia kesi za Malaria zikionekana kuanza kupanda tena. Hatuwezi kusubiri tena mpaka hali hii igeuke kuwa janga na ndio maana CUF inapendekeza mpango kazi mahkusi wa taifa shirikishi unaojitosheleza wenyewe kwa kiasi kikubwa ya kuendeleza na juhudi za kinga na mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria na magonjwa mengine yanayofanaa kama vile dengue na homa ya manjano.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itandelea kupambana na ugonjwa wa malaria na kuhakikisha kuwa matumizi ya madawa na Kemikali za kupulizia zinakidhi viwango vya usalama wa raia na mali zao kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) au taasisi za kimataifa za afaya za Marekani na Umoja wa Ulaya.*
- *Itahakikisha utii wa Haki za Binadamu na kupinga vitendo vya kulazimisha kuvamia nyumba za wananchi kwa askari na vitisho na kuingia ndani mwao kupulizia dawa bila ya ridhaa zao.*
- *Itachagua njia ya mazungumzo ya kistaarabu, elimu tosha ya afya ya jamii kwa wananchi, na mtindo wa kuwavutia walengwa kama njia pekee endelevu ya kumaliza ugonjwa wa malaria, na sio kwa vitisho na vikosi vya usalama.*
- *Itaendelea kushirikiana na washiriki na mashirika ya maendeleo ya kimataifa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria hususan Marekani.*

11.6. UDHIBITI WA VIRUSI NA UGONJWA WA UKIMWI

UKIMWI unaendelea kuwa tatizo kubwa kwa maendeleo ya Taifa. Pamoja na kubahatika kupata misaada mbali mbali ya kitaaluma, kifedha, zana na miundombinu ya usimamizi na kinga kutoka kwa washirika mbali mbali wa kimaendeleo, bado kuna changamoto kubwa za kitaasisi na katika ufikiwaji wa walengwa ndani ya Nchi yetu. Unyanyapaa unaendelea kushamiri wakati imani ya waathirika kuhusiana na uhifadhi wa siri zao kwa wahusika imepotea. Haki za wagonjwa wa UKIMWI makazini na katika jamii bado zingali duni na hofu ya ukoseshwaji wa fursa za ajira kwa waathirika ni tatizo linalousukuma ugonjwa huu chini kwa chini (underground).

Sera na Sheria zinazohusiana na kinga na tiba kwa ugonjwa wa UKIMWI zisiwe ni fatwa za kuwanyima waathirika haki zao za binadamu pamoja na matamko ya kimataifa ya kulinda haki na siri za waathirika.

Taasisi zianzosimamia kinga na tiba za VVU/UKIMWI zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa mipango bora ya ufikiwaji wa jamii na waathirika, matumizi ya rasilmali finyu tulizo nazo katika kupigana na ugonjwa wa UKIMWI, uwazi katika utekelezaji wa mipango ya usimamizi na ufikiaji wa walengwa, na usambazaji wa uhakika wa madawa ya kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaendelea, kuiboresha na kuimarisha Mipango ya Taifa ya Afya, udhibiti wa VVU/UKIMWI.*
- *Itahakikisha upatikanaji wa madawa muhimu ya VVU/UKIMWI bure katika hospitali zote za serikali na vituo vya afya.*
- *Itaunda mkakati mpana na shirikishi wa kitaifa na kupambana na tabia hatarishi zinazosababisha VVU/UKIMWI.*
- *Itahakikisha uboreshaji wa huduma za kinga na tiba katika VVU/UKIMWI na kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilmali zinazotokana na mifuko ya ndani na nje katika kupambana na ugonjwa huu.*
- *Itazidi kupiga vita unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya wathirika wa VVU/UKIMWI na kuunda mfumo madhubuti wa hifadhi ya siri za wagonjwa na waathirika.*
- *Italitekeleza kwa vitendo azimio la Umoja wa Mataifa kuhusiana na udhibiti wa maambukizi, vita dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu, kuwaondolea vikwazo vya usafiri waathirika wa VVU/UKIMWI, udhibiti wa madawa ya kulevya, udhibiti wa mmabukizi ya mama kwa mtoto, mapambano dhidi ya uonevu wa kijinsia kwa walioathirika, ufikiaji wa madawa, mashirikiano katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, na kuondoa unyanyapaa.*

11.7. KIPINDUPINDU NA AFYA YA JAMII

Insikitisha kuona kuwa nchi yetu imeingia katika karne ya ishirini na moja na ongezeko la maradhi ya kipindupindu na maradhi mengine ya kuharisha ambayo sababu za kuwepo kwake kimsingi ni kutokana na mfumo uliofeli (broken system) wa usimamizi wa usafi wa mazingira na afya ya jamii. Kudharauliwa kwa uwekezaji wa sekta ya jamii na kukosekana kwa mipango madhubuti ya mipango miji, huduma za maji safi na afya ya jamii, huduma za usafi wa mazingira na elimu kwa jamii, pamoja na masuala ya kinga na tiba na uendeshaji wa maisha yenye siha bora kumepelekea kuiskukuma jamii katika dimbwi la umaskini huu. CUF inaamini kuwa muundo mbovu wa usimamizi katika sekta ya afya ya jamii (Public Health), ufisadi, rushwa, na maamuzi holela yanayokwenda kinyume na afya na mazingira ndio sababu kuu ya maginjwa kama ya kipindupindu na mengineo. Wakati umefika kwa kuukarabati muundo huu na njia pekee ni kuwaondoa madarakani wahusika wote wa kadhia hii.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itahakikisha usimamizi bora wa afya ya jamii (Public Health) katika miji, vijiji, na mitaa ili kupunguza hatari ya ugonjwa wa kipindupindu.*
- *Itazidisha utoaji wa elimu ya afya ya jamii kwa wananchi kwa madhumuni ya kinga na udhibiti wa ugonjwa.*
- *Itahakikisha usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi*
- *Itashajiisha usimamizi usafi wa mazingira katika ngazi ya shehia, halmashauri hadi taifa.*

11.8. USIMAMIZI WA TIBA ASILIA

Tiba asilia ni urithi wa utamaduni wetu. Urithi huu hatuna budi kuuenzi na kuutumia kwa siha njema na afya bora. Tatizo na migogoro mkubwa wa kiafya unajitokeza pale jamii kushindwa kumudu gharama za tiba ya kisasa na kudhani kuwa matatizo yao ya magonjwa mbali mbali hatari na sugu yatapatiwa ufumbuzi unaostahiki kwa kutumia tiba asilia. Hatuna budi kwa sote kusaidiana kuielemisha jamii juu ya hatari ya dhana hii potofu bila ya kuathiri umuhimu wa tiba asilia kwa utamaduni wetu. CUF inaamini kuwa hili linawezekana pale Serikali ya kweli wa wananchi itakapounda mikakati maalum wa kitaifa wa usimamizi, viwango na ufanisi wa tiba asilia ndani ya sekta kuu ya afya Zanzibar.

- *Itaupitia tena muundo mzima wa usimamizi wa tiba asilia na kuhakikisha uangalizi wa viwango, maadili, madawa yanayotumika, na sifa za watabibu wa tiba hii asilia.*
- *Itahakikisha usalama wa wagonjwa wanaotegemea tiba asilia.*
- *Itahakikisha dawa zote za tiba asilia zina usajili halali na kumabuliwa chini ya bodi za viwango.*
- *Itasisitiza waganga wote wa tiba asilia kusajiliwa rasmi na Serikali.*

11.9.VIWANGO VYA VYAKULA NA MADAWA

Ufisadi katika uhodhi wa maamuzi ya nani mwenye haki ya kuagiza na kuuza vyakula na bidhaa mbali mbali za matumizi ya mwanadamu ndio chanzo cha kuanguka kwa maadili ya uagizaji, upasishaji, na usimamizi wa viwango vya vyakula bora, kemikali na bidhaa nyingine za matumizi ya binadamu hapa nchini. Cha kushangaza ni kuwa wahusika wa makosa haya ya jinai wanajulikana. Lakini hakuna hatua hatua yeyote inayochukuliwa kuwadhibiti wahusika kwa mujibu wa sheria. Kila mara Serikali imekuwa ikiingia hasara kubwa ya kukabiliana na janga la uingizwaji wa vyakula vibovu na madawa yasiofaa kwa matumizi ya binadamu bila ya kuwawajibisha wahusika.

CUF kamwe haiwezi kuikubali wala kuiachia hali hiyo na haitomvumilia yeyote atakaebainika kutishia afya na maisha ya wanadamu wenzake kwa kuingiza bidhaa mbovu. Kuna haja kubwa ya kupitia muundo mzima wa upasishaji, na usimamizi wa viwango vya vyakula bora, madawa na bidhaa nyingine za matumizi ya binadamu hapa nchini ikiwemo ufanisi wa Bodi ya Vyakula na Madawa na Maabara ya Mkemia Mkuu Zanzibar.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaupitia muundo mzima wa uchunguzi na upasishaji wa vyakula na madawa kutoka nje na kuhakikisha uwazi katika utekelezaji na uwajibikaji katika kuhakikisha sheria zinachukua mkondo wake unaostahiki na chakula na bidhaa nyingine zinazoagizwa kutoka ndani na nje basi ni salama kwa matumizi ya binadamu.*

11.10. KUONGEZEKA KWA MAGONJWA YA AKILI

CUF inaamini kuwa tatizo la matumizi na athari za madawa ya kulevya ni tatizo linalojumuisha afya, familia na changamoto za jamii kwa pamoja. Lakini pia ni tatizo la ubovu mkubwa uliopo wa sera zetu za ulinzi na usalama dhidi ya magendo ya dawa za kulevya na kemikali nyingine zinazofanana. Ufisadi unaondelea kufanywa na baadhi ya watu wachache wanaolindwa na washirika wao wenye ushawishi mkubwa kisiasa kwa kushirikiana na wahalifu wa madawa ya kulevya kuharibu maisha ya vijana wetu na kupelekea mitafaruku katika jamii na maendeleo ya nchi nzima, haliwezi kuvumiliwa tena.

CUF itachukua hatua za haraka na za mara moja katika kuukata mfereji huu unaoingiza madawa ya kulevya nchini na kuhakikisha kuwa wahusika wote wanawajibishwa mbele ya vyombo vya sheria za nchi.

- *Itazidisha jitihada za kuharakiza tiba kwa waathirika wa maradhi ya akili (Rahabilitation) wakati ikiziba mianya yote ya kihalifu inayotumiwa kuingiza magendo ya madawa ya kulevya nchini.*
- *Itakuwa na "Zero-Tolerance Policy" kwa yeyote atakayebainika kufanya biashara hiyo haramu hapa nchini.*

11.11. AFYA YA MAMA MZAZI

CUF inashukuru jitihada zilizochukuliwa na wafadhili mbali mbali ikiwemo wa mradi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) wa kusaidia huduma za tiba na kinga kwa akina mama wajawazito kuelekea kunako uzazi salama. Hata hivyo, sekta za ndani za nchi bado hazijaona umuhimu wa uwekezaji wa kutosha katika masuala haya na mzigo huu umekuwa mkubwa kwa hospitali na kiliniki nyingi kuweza kuzimudu.Msongamano wa kina mama wazazi katika wodi za uzazi hospitalini ni wa hali ya kutisha.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanya ifuatavyo:

- *Itaendelea kutoa huduma za uhakika kwa tiba na kinga za kwa wazazi ikiwemo uwekezaji katika miundombinu na vitende kazi kwa wahudumu, ajira bora kwa wauguzi na wakunga, dawa, na zana mbali mbali za afya kwa mama mzazi.*
- *Itazidisha juhudi za mashirikiano na wafadhili na mashirika ya maendeleo kuendeleza kuisaidia Zanzibar katika kufanikisha azma ya muda mrefu ya uzazi salama.*

Grand
Malt
uhlsport
4
8

12. TUTAYAHUDUMIAMAKUNDI MAALUM NA KUNYANYUA MAENDELEO YA JAMII

Siha ya jamii ni siha ya taifa. Zanzibar ina utajiri wa rasilmali za ubunifu kutokana na maendeleo ya kifikra ya jamii yake. Kihistoria jamii hii imetokana na mataifa na tamaduni mbali mbali zilizoipa sifa nchi hii karne kwa karne. Hivyo tunapaswa kuuenzi urithi wetu kwa kuhakikisha tuna Serikali na uongozi unaojali maslahi ya wananchi wote wakiwemo makundi maalum, vijana, wanawake, wenye ulemavu, watoto, wazee wetu, na wengineo. Uwekezaji katika usalama na maendeleo ya jamii (Social Security and Services) ni jambo la msingi katika kuleta uwiano wa kweli wa jamii yetu na kufikia maendeleo tunayoyataka. Nchi yetu inapita katika kipindi maalum cha kuhakikisha kuwa usawa wa jamii (Social Equity) unafikiwa kama ilivyoahidiwa na waasisi wa ukombozi wetu. CUF itaendeleza ahadi hizo kwa utekelezaji wa kweli na kwa maslahi ya taifa kwa ujumla.

12.1. WANAWAKE

Wanawake ni asilimia 51 ya idadi ya Wazanzibari. Hivyo, kuwawezesha wanawake kutapewa umbele na Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF. Pamoja na juhudi kubwa zinazodaiwa kufanywa kumkomboa mwanamke, wanawake bado wako nyuma kwa kila hali. Hakuna mfuko maalum wa kusaidia elimu ya juu kwa wanawake na kutetea hatua thabiti za kuongeza kuingizwa wanawake katika taasisi za masomo ya juu. Kuna uwakilishi mdogo wa wanawake katika vyombo vyote vya kutoa maamuzi ikiwa ni pamoja na Baraza la Wawakilishi. Utamaduni kisiasa uliojengeka bado haumpi nafasi anayostahiki mwanamke katika masuala ya uongozi na maendeleo ya jamii.

Serikali ya Umoja Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itaingiza masuala ya jinsia katika sera na mipango ya maendeleo ya taifa.*
- *Itatoa kipaumbele katika kuboresha mikakati ya kitaifa ya kusaidia huduma mbali mbali za kiuchumi zinazofanywa na wanawake hususan katika maeneo ya nishati, usimamizi wa maliasili, kilimo, mwani, maji, na uzalishaji wa bidhaa mbali mbali.*
- *Itatekeleza mipango ya muda mrefu ya ufikiwaji wa huduma za afya, elimu, ufikiwaji wa huduma za masoko, pamoja na ushirikishwaji kikamilifu wa wanawake katika maamuzi ya jamii.*
- *Itaongeza muamko dhidi ya tabia zinazoendeleza ubaguzi dhidi ya wanawake.*
- *Itatekeleza maazimio ya kimataifa yanayoshajihisha kulindwa na kuenziwa kwa haki za wanawake.*
- *Itahakikisha kinga ya wanawake mbele ya sheria dhidi ya aina zote za usumbufu, ukatili na unyanyasaji (Gender Based Violence au GBV).*
- *Itaongeza fursa kwa wanawake katika elimu ya sekondari na nyengine, kupuguza utokaji skuli mapema kwa wasichana na kuongeza utendaji wao.*
- *Itashajiisha mafunzo ya amali, sayansi na teknolojia ya wanawake ikiwa ni pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA).*
- *Itaandaa sera ya kitaifa kuhusu wafanyabiashara wa kike, kuwapatia huduma za ushauri na njia za kuimarisha uzalishaji, soko na kutangaza biashara zao.*

12.2. VIJANA

Pamoja na kuwa takriban asilimia 70 ya Wazanzibari ni vijana wa chini ya miaka 30, rika hili bado halijioni kuwakilishwa ipasavyo katika vyombo vya maamuzi katika nchi, iwe Serikalini na hata katika sekta binafsi. Hakujachukuliwa hatua za msingi katika kukuza vipaji vya vijana. Wengi wao wanakosa fursa za ajira jambo ambalo linawafanya waingie katika vitendo viovu. Vijana wametengwa kiasi kwamba wanahisi njia pekee ya kujiendeleza ni kuondoka nchini. Hiki ni kipingamizi kwa maendeleo ya nchi na ustawi wake. Vijana wengi, hasa mjini wamejiingiza katika tabia mbaya ikiwa ni pamoja na kutumia madawa ya kulevya.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itatoa fursa za mafunzo kwa vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo skuli ili wajiendeleze katika ujuzi kupitia mafunzo ya amali.*
- *Itaweka huduma za ushauri kwa vijana kuhusiana na mambo mbalimbali ya kimaisha ili kuwawezesha kufanikisha malengo yao.*
- *Itawaelimisha na kuwatahadharisha vijana juu ya athari za madawa ya kulevya na itachukua kila aina ya juhudi za kuyatokomeza madawa hayo kutoka katika nchi yetu ili kufikia lengo la kuiona Zanzibar bila ya Madawa ya Kulevya (Drug Free Zanzibar).*
- *Itawashirikisha viongozi wa kidini katika kuelimisha vijana kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI.*
- *Itakuza michezo ya aina mbali mbali kwa kuimarisha viwanja, kutoa mafunzo na kupunguza kodi kwenye vifaa vya michezo ili kuifanya Zanzibar iwe nchi ya mfano katika michezo mbali mbali kama ilivyowahi kuwa miaka ya nyuma.*
- *Itashajihisha uwekezaji katika michezo ikiwa ni pamoja na kukazania kukuza vipaji vya vijana na kuona inatoa kila misaada katika kukuza vipaji hivyo kwa lengo la kuwapata wanamichezo wa kulipwa wa viwango vya kimataifa.*
- *Itaondoa vipingamizi vinavyowanyima vijana uhuru na kujipangia maisha yao na kwenda popote wanapotaka duniani alimradi hawavunji sheria.*
- *Itasimamia kurejeshwa kwa maadili mema ya Wazanzibari kwa kuhuisha mila, silka na utamaduni wetu na kuwarejeshea Wazanzibari hadhi na fahari yao iliyotokana na mila, silka na utamaduni huo ambao unakataza tabia ovu kama ile ya utumiaji wa madawa ya kulevya.*
- *Katika kurejesha maadili hayo, Serikali itapambana vikali na uingizaji na uuzaji wa madawa ya kulevya ambao umekuwa ukiongezeka kwa kasi visiwani Zanzibar kwa kuhakikisha kuwa sheria zinatekelezwa na kusimamiwa ipasavyo ili kudhibiti uingizaji na uuzaji wa madawa hayo.*
- *Itatoa msukumo mkubwa kwa kuanzisha, kuviunga mkono na kuviendeleza vituo vya kuwasaidia waathirika wa madawa ya kulevya ambao wengi wao ni vijana ili waache utumiaji huo kwa kuamini kuwa jamii inayofanikiwa kuwaelimisha watu wake athari za utumiaji wa madawa hayo itakuwa imepunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hilo kwani waingizaji na wauzaji watakosa soko la biashara hiyo haramu na ovu.*
- *Itaangalia namna ya kuwasaidia vijana wanaoikiwa ni pamoja na kuwapatia ajira na shughuli nyengine za kufanya wale walioacha matumizi ya dawa za kulevya.*

12.3. WENYE ULEMAVU

CUF inadhamiria kujenga jamii inayojali na kuwawezesha watu wenye ulemavu kufurahia maisha yao kama watu wengine. Hii ni haki ya binadamu. Watu wenye ulemavu bado wanachukuliwa kama watu wanaoshindwa kudhibiti maisha yao, kama watu wa kusaidiwa sana au wagonjwa wanaohitaji kutibiwa. Dhana hii ni potofu na inahitaji kuondoshwa kwa kukuza uelewa na elimu ya jamii kuhusiana na haki na fursa wa wetu wenye ulemavu. Masuala

ya ulemavu hayajazingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya sera na kanuni za Taifa. Pamoja na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa, bado hakuna uwekezaji wa kutosha wa kibajeti wa kupanua fursa zaidi za elimu, ajira, huduma nzuri za afya, ujasirimali, na uongozi wa watu wenye ulemavu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itahakikisha sera na kanuni zote za taifa zinaingiza masuala ya ulemavu. Hili litafanywa kwa lengo pekee la kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika shughuli mbali mbali kama wananchi wengine.*
- *Itahakikisha mipango yote inayohusiana na ulemavu inapata fedha za kutosha.*
- *Itashajihisha na kuwasaidia watu wenye ulemavu kuunda vikundi vyao na itazisaidia jumuiya zao ambazo huongeza uwezo wa kujitegemea na kudai haki zao.*
- *Itajitahidi kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wote wanapata elimu rasmi na muafaka kadiri itakavyowezekana.*
- *Itaweka na kuimarisha utoaji mzuri wa huduma za afya kwa watu wenye ulemavu katika viwango vyote.*
- *Itahakikisha kuwa majengo mapya ya Serikali na yale ya binafsi yanayotoa huduma kwa raia yanajengwa katika hali inayokidhi hali za watu wenye ulemavu ili waweze kutumia huduma zake kama wafanyavyo Wananchi wengine wote.*
- *Itaifanyia mapitio kwa lengo la kuifanya iende na wakati Sheria inayowalinda watu wenye ulemavu na kuwapa haki ya kutumia fursa zote za kijamii kama wananchi wengine kwa kutumia rasimu iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa.*

12.4. WATOTO

Watoto ni mbegu ya rasilimali ya Taifa kwa kipindi kirefu kijacho. Kuwaendeleza watoto ni kitega uchumi madhubuti kwa Taifa lolote. Watoto wanahitaji mazingira mazuri yatakayokuza akili zao na uwezo wao wa kubuni. Watoto wanahitaji kupewa kipaumbele ili kujenga taifa imara na lenye nguvu siku zijazo. Watoto ndio hasa msingi wa maendeleo ya baadae. Serikali imeshindwa kuweka sera madhubuti juu ya mustakbali wa watoto. Pamoja na kuunda Wizara inayohusiana na watoto, Serikali imeshindwa kuwapa kipaumbele watoto katika mipango yake yamaendeleo. Kwa muda mrefu watoto wa Kizanzibari wamekosa maeneo ya kuchezea katika mitaa na viwanja vya kujifurahishia na maeneo mengi ya wazi yamekuwa yakichukuliwa katika njia za ajabu na kujengwa. Hakuna matunzo yanayostahili kwa watoto mayatima. Hakuna mfumo unaoeleweka wa ulipiaji wa huduma mbalimbali zinazochanganya watu wazima na watoto.

Masuala ya udhalilishaji wa watoto yamekuwa yakiripotiwa kwa wingi. Sura hii ni ya kutisha na kila Mzanzibari ana wajibu wa kumlinda mtoto kutokana na unyama na udhalilishaji wa aina yeyote anaofanyiwa popote pale alipo. CUF inaamini kuwa ulinzi na uhifadhi wa haki za watoto ni wajibu wa jamii nzima.

Watoto wa skuli bado wameendelea kutumiwa katika shughuli za siasa kwa lazima. Serikali haitilii mkazo ukatazaji wa ajira ya watoto na hivi karibuni Ripoti ya ILO imeitaja Zanzibar kuwa mojawapo ya nchi zenye utumikishaji wa watoto unaokuwa kwa kasi kubwa. Maadili ya watoto ni mzigo walioachiwa wazazi peke yao.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itahakikisha mustakbali mwema kwa mtoto kupitia sera, mipango na sheria bora za ulinzi, uhifadhi wa haki, na ukuzwaji wao wenye maadili mema.*
- *Itawekeza katika kuinua viwango vya mafunzo ya elimu ya ulinzi, usalama wa raia, na uhifadhi wa haki za mtoto pamoja na kumlinda mtoto kutokana na ukatili au udhalisihaji wowote ule anaofanyiwa.*
- *Itatoa kipaumbele kwa huduma bora za lishe, elimu, afya, kwa watoto katika mipango yake ya maendeleo ya jamii.*

- *Itahakikisha watoto wote wanapata maeneo huru ya kuchezea katika mitaa, na kwamba viwanja vya burudani vya kujifurahishia vinaendana na maadili na mila za Mzanzibari katika mji au vijiji wanavyoishi.*
- *Itasimamia na kuhakikisha watoto mayatima wanapata matunzo yanayostahili.*
- *Itahakikisha kwamba watoto hawashirikishwi kabisa katika siasa.*
- *Itahakikisha watoto hawaajiriwi wala kuachiwa kujiajiri.*
- *Itahakikisha watoto wote wanapata mahitaji na matunzo wanayostahiki ya kujenga maisha yao ya baadaye.*
- *Itaanzisha channel ya televisheni ya watoto chini ya ZBC yenye kuonyesha vipindi vya maadili mema kwa watoto.*

12.5. WAZEE NA WASTAAFU

Wazee wa Zanzibar wamejenga historia kubwa kwa kulifikisha taifa letu hapa lilipo lakini wao ndio wanaoishi maisha magumu kupita kiasi na pamoja na Serikali kuchukua hatua za kuwasaidia, bado hatua hizo hazijatosheleza kuonesha kama Taifa linajali na kuthamini kweli mchango wao. CUF inaamini kuwa ahadi yake ya kuendeleza kuwasaidia wazee na wastaafu ikiwemo kuongeza kiwango cha pensheni ni msingi mzuri wa kuanzia. Lakini wazee na wastaafu pia wanatarajia huduma bora maalum za afya, siha, na shughuli mbali mbali za kuwaunga mkono.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itaboresha pensheni ya wastaafu katika sekta zote ili kukidhi mahitaji yao.*
- *Itaendelea kuwalipa wastaafu wote malipo ya pensheni na viinua mgongo vyao kwa wakati ili kuepusha usumbufu kwao.*
- *Itaanzisha utaratibu wa kuwapatia wazee huduma muhimu za kijamii bila malipo na urasimu wowote.*
- *Itashajiisha umuhimu wa familia na jamii kuwatunza wazee na wastaafu wetu ili waweze kuishi vyema na katika hali ya kujikimu mahitaji yao.*
- *Itaimarisha Nyumba za Wazee za Sebleni Unguja na kuangalia uwezekano wa kujenga nyumba nyengine kama hizo katika kisiwa cha Pemba kwa ajili ya kuwasaidia wazee wasiojiweza na wasio na jamaa wa kuwatunza.*

12.6. WATAALAMU

Zanzibar Mpya tunayokusudia kuijenga haitaweza kupiga hatua za maendeleo iwapo wataalamu hawatapewa kipaumbele katika nyanja mbali mbali. Nchi yetu ina wataalamu wengi wa ndani na nje katika sekta za uchumi, sekta za kijamii na kiutamaduni. Lakini bado hatujaweza kuwatumia ipasavyo hapa nyumbani katika kuwakomboa Wazanzibari kutoka katika dimbwi la umasikini, ujinga, maradhi na matatizo mengine yanayotukabili.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itafanywa ifuatavyo:

- *Itaanzisha tuzo maalum kwa ajili ya wataalamu wote waliofanya kazi muhimu ya kitaalamu na ikaleta tija kwa nchi.*
- *Itawashajiisha wataalamu wa Kizanzibari waliosambaa katika nchi tofauti duniani kurejea Zanzibar kwa lengo la kuja kuungana na wananchi wenzao kubadilisha hali za maisha ya watu wetu na kuijenga upya nchi yetu.*
- *Itawapa uhuru wa kujianzishia vyama vya kitaaluma na klabu mbali mbali ili wakutane mara nyingi kadri wawezavyo na kujadiliana mambo na mbinu mbali mbali ili kuinua taaluma yao kulingana na asili ya maeneo waliyopo.*
- *Itawapeleka wataalamu wengi nje ya nchi kadri iwezekanavyo ili wakaongeze taaluma zao kwa maslahi ya nchi. Hivi sasa wataalamu wanaopelekwa nje ya nchi kuongeza mafunzo ya kitaalamu ni wachache na hakuna uzingatiaji wa vigezo sahihi katika kuwateua.*

- *Itawaongezea vivutio zaidi na kuboresha maslahi yao kiutendaji ili wataalamu wetu wasiichoke kazi yao muhimu katika kuleta maendeleo ya kweli katika nchi.*

12.7. UTAMADUNI NA MICHEZO

Pamoja na kuwa michezo haikutajwa katika orodha ya mambo ya Muungano, michezo bado imeshindwa kupewa nafasi yake ya kuijengea Zanzibar umaarufu inaostahili kutokana na vipaji vya vijana wake. Bajeti ya Serikali inatupia macho mchezo wa mpira wa miguu tu na haishughulikii michezo yote mengine. Vyama vya michezo nchini havina Ofisi, bajeti ya kutosha wala usafiri wa uhakika wa kuwawezesha kuongoza vyema shughuli za michezo.

Hakuna hata ukumbi mmoja wa michezo ya ndani (indoor games) hapa Zanzibar, tukiachilia mbali ukumbi wa mchezo wa judo ambao ulijengwa kwa juhudi za mtu mmoja kwa kuiomba Serikali ya nchi yake kufanya hivyo. Pia Serikali imeshindwa kujenga hata bwawa moja la kuogelea ambamo ndimo yangeweza kufanyika mashindano ya kuogelea.Viwanja vingi vipo katika hali mbaya. Siasa imeachwa kuingilia michezo na kufika hata kupinda sheria za michezo kwa lengo la kutumiza manufaa ya kisiasa.

Utamaduni wa Mzanzibari unaendelea kuporomoka na kupelekea kupotea kwa tunu na vionjo vinavyomtambulisha na kumtofautisha Mzanzibari. Mila, silka na desturi za watu wa Zanzibar ambazo zimekuwa ni mojawapo ya vivutio vikubwa kwa wageni wanaofika na kutembelea nchi yetu zimeachwa bila ya kuwa na mpango maalum wa kuzitunza na kuzirithisha kwa vizazi vijavyo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itafanya yafuatayo:

- *Itatoa fursa na kuvisaidia vyama vya michezo yote mengine kujiunga na Mashirikisho ya Michezo ya Kimataifa. Katika hili, itaendelea kufuatilia na kulifikisha mwisho kwa kutoa msukumo wa aina ya pekee kwa maombi ya Zanzibar kujiunga na Shirikisho la Soka la Dunia (FIFA).*
- *Itaongeza ruzuku inayotolewa kwa Baraza la Michezo Zanzibar (BMZ) ili liweze kukidhi haja ya kuvisaidia vyama vyote vya michezo hususan vile vinavyojituma zaidi na kuonekana kuiletea sifa nchi kwa madhumuni ya kukuza michezo nchini.*
- *Itakaribisha wawekezaji binafsi kujenga ukumbi wa michezo ya ndani, ikiwa ni pamoja na bwawa la kuogelea, ama peke yake au kwa kushirikiana na serikali.*
- *Itaunda Shirika litakaloendesha Viwanja vya Amani na Gombani ili kuviwezesha kuendeshwa kibiashara.*
- *Itahakikisha kuwa viwanja vya Mao Tse Tung vinabaki kuwa viwanja vya michezo kwa ajili ya umma.*
- *Itakaribisha wawekezaji binafsi kujenga viwanja vya kisasa kwa ajili ya michezo ya ndani na viwanja katika mikoa mbali mbali nchini ili kukuza michezo katika maeneo hayo.*
- *Itaipitia upya Sera ya Michezo na kuhakikisha inalingana na hali halisi ilivyo katika ulimwengu wa kisasa wa michezo.*
- *Itahakikisha kunaanzishwa vyuo maalum vya kuendeleza michezo na vipaji vya wanamichezo zikiwemo kumbi za mazoezi ya viungo kwa jinsia na rika mbali mbali.*
- *Itahakikisha kuwa itikadi za kisiasa haziingizwi katika michezo na uteuzi wa viongozi wa michezo haufuati utashi wa kisiasa.*
- *Itasimamia kurejeshwa kwa maadili mema ya Wazanzibari kwa kuhuisha mila, silka na utamaduni wetu na kuwarejeshea Wazanzibari hadhi na fahari yao iliyotokana na mila, silka na utamaduni huo.*
- *Itahimiza na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili fasaha kwa kuchukua hatua za kuzilinda lahaja za Kiswahili zinazozungumzwa Zanzibar ambazo ndizo chimbuko la Kiswahili sanifu. Juhudi*

maalum zitafanywa kulirejeshea hadhi na kulipa nguvu na uwezo Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) liweze kuisimamia vyema lugha ya Kiswahili ili isiendelee kuathiriwa kwa kupotoshwa na kuchafuliwa.

- *Itawasaidia wasanii wakongwe na chipukizi wanaojitokeza sasa kwa kuziunga mkono kikamilifu juhudi za wadhamini mbali mbali ambao wanajitokeza kukuza vipaji vya wasanii na kuwaendeleza.*
- *Itafanya marekebisho mbalimbali ya kisheria ili kulinda kikamilifu haki za wasanii wetu .*

12.8. MADAWA YA KULEVYA

Nchi yetu imeathirika sana na biashara ya madawa ya kulevya. Vijana wetu wengi wamejikuta wakiingizwa katika biashara hii pamoja na matumizi yake. Matokeo yake ni kuwepo kwa athari kubwa ya kiafya, kijamii, kiuchumi na kimaendeleo kutoka katika ngazi ya familia hadi ya taifa. Tutakuwa tunafanya makosa makubwa ikiwa tutaendelea kulichukulia suala hili kama ni la maadili peke yake tu, bali ni suala la usalama mzima wa utaifa wetu na vizazi vyetu vijavyo. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kujtolea kuwasaidia vijana wetu na wale wote walioathirika na janga hili. Lakini pia ni wajibu wetu kuwakaribisha kwa jicho la wema na upendo wale waathirika wote walioweza kupona na wakawa tayari kurejea katika katika ujenzi wa taifa letu.

CUF inaamini kuwa suluhisho endelevu la janga hilo linawea likaja kwa kutumia misingi ya aina tatu: kuwahudumia waathirika, kutoa elimu bora ya kinga na tiba kwa jamii, na kupambana kwa nguvu zote na wale wote wanaohusika na magendo, uingizaji na uuzaji wa madawa haya ya kulevya hapa Zanzibar.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua zifuatazo:

- *Itasimamia kurejeshwa kwa maadili mema ya Wazanzibari kwa kuhuisha mila, silka na utamaduni wetu na kuwarejeshea Wazanzibari hadhi na fahari yao iliyotokana na mila, silka na utamaduni huo ambao unakataza tabia ovu kama ile ya utumiaji wa madawa ya kulevya.*
- *Katika kurejesha maadili hayo, Serikali itapambana vikali na uingizaji na uuzaji wa madawa ya kulevya ambao umekuwa ukiongezeka kwa kasi visiwani Zanzibar kwa kuhakikisha kuwa sheria zinatekelezwa na kusimamiwa ipasavyo ili kudhibiti marufuku ya uingizaji na uuzaji wa madawa hayo.*
- *Itatoa msukumo mkubwa kwa kuanzisha, kuviunga mkono na kuviendeleza vituo vya kuwasaidia waathirika wa madawa hayo ya kulevya ambao wengi wao ni vijana ili waache utumiaji huo.*
- *Itatoa elimu kwa jamii kuhusu athari za utumiaji wa madawa ya kulevya ili kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo.*
- *Itaangalia namna ya kuwasaidia waathirika wa madawa ya kulevya ikiwa ni pamoja na kuwapatia ajira na shughuli nyengine za kufanya wale walioacha matumizi ya dawa za kulevya.*
- *Itahakikisha inashirikiana na wananchi katika ngazi ya Shehia kuandaa mikakati na mipango ya kupambana na madawa ya kulevya.*
- *Itatizama upya mwenendo wa kesi za madawa ya kulevya ili kuona vikwazo vinavyokwamisha kesi hizo.*
- *Itaanzisha "one stop center" katika viwanja vya ndege ili anapokamatwa mtuhumiwa wa madawa ya kulevya uchunguzi na hukumu vimalizie hapo hapo.*




CUF